NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

**Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 29 Aprili, 2022**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini

kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali; tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Ally Yahaya Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini.

Na. 118

**Hitaji la Magari ya Kubebea Wagonjwa Nanyumbu**

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA K.n.y. MHE. ALLY Y. MHATA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itapeleka magari ya kubebea wagonjwa katika Vituo vitatu vya Afya Wilayani Nanyumbu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Yahaya Mhata, Mbunge wa Jimbo la Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Nanyumbu ina magari mawili ya kubebea wagonjwa ambayo yanatumika

katika Hospitali na Vituo vya Afya. Hata hivyo, magari haya bado ni machache kwa kuzingatia uhitaji uliopo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19 itanunua magari 195 ambapo kila Halmashauri itapata gari la kubebea wagonjwa ikiwemo Halmashauri ya Nanyumbu. Ununuzi huu utaboresha huduma za afya za dharura na rufaa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Nashukuru pia kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini pamoja na majibu hayo, kuna vituo vya afya ambavyo viko mbali sana na Hospitali ya Wilaya kiasi ambacho inakuwa shida kwa wagonjwa kupelekwa katika hospitali hiyo. Kwa mfano, Kituo cha Mtambaswala ni kilomita 70 kutoka Hospitali ya Wilaya, Kituo cha Nanyumbu kilomita 40, Kituo cha Michiga kilomita 30; kwa hiyo, kwa umbali huo, naomba kupata *commitment* ya Serikali kwa sababu kama tutagawa *equally* kwa Halmashauri zote, kuna vituo vya afya ambavyo vitakuwa havifanyiwi kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, naomba pia kupata majibu ya Serikali: Ni lini Kituo cha Afya cha Mkwedu ambacho kipo katika Jimbo la Newala Vijijini kitapelekewa gari kwa ajili ya wagonjwa kwa sababu kituo kile kinahudumia kata zaidi ya tano?

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maimuna Mtanda, Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Vituo vya Afya vya Mtambaswala, Nanyumbu viko mbali sana kutoka Hospitali ya Halmashauri na Serikali inatambua kwamba vituo vya mbali sana vinahitaji kupata magari ya wagonjwa. Ndiyo maana katika mwaka huu wa fedha Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ametupa fedha TAMISEMI kwa ajili ya kununua magari 407. Magari ya wagonjwa 195 kwa kila halmashauri na halmashauri hii ya Nanyumbu itapata na magari 212 kwa ajili ya usimamizi wa huduma za afya katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, utaona tutakuwa na magari zaidi ya hayo, lakini tutaendelea kutoa kipaumbele kwenye vituo vya mbali zaidi ili vipate magari yakiwemo vituo hivi vya afya.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Kituo cha Afya cha Mkwedu, naomba nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutatafuta fedha ili tuweze kupeleka gari la wagonjwa. Nafahamu kituo hiki kiko mbali sana na kinahudumia wananchi wengi. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deo Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Jimbo la Njombe limekuwa na vituo vitatu vimekamilika muda mrefu sana; na huu mgao wa *equal* unatupa wasiwasi kwa vile vituo ambavyo vinangojea magari na vimeahidiwa miaka zaidi minne: Je, Serikali itatusaidia kwenye hilo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deo Mwanyika, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tunahitaji vituo vyetu viwe na magari ya wagonjwa kila kituo kiwe na gari la wagonjwa. Safari ni hatua. Kwa sasa tunaanza na vituo vile vya kimkakati, lakini mara nyingi uzoefu unaonesha vituo vya afya vingine vinaweza vikawa *saved* na magari ya wagonjwa yaliyo katika Hospitali za Halmashauri au katika vituo vya afya vya jirani. Kwa hiyo, tutaendelea kuangalia umbali wa kituo cha afya kutoka hospitali na pia *population* ambayo ina-*save* ili kuhakikisha kwamba tunapeleka magari katika vituo hivyo. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Geita ina majimbo mawili na hospitali mbili za wilaya. Sasa kwa maelezo ya Waziri, ina maana likija gari moja itakuwa ni ugomvi ikakae hospitali gani; aidha, likae Jimbo la Geita Vijijini au Busanda, ambapo kila jimbo lina hospitali: Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari sasa *special* kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Geita kuleta magari mawili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mbunge wa Jimbo la Geita Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, magari ya wagonjwa yatakayonunuliwa ni magari 195, nasi tuna Halmashauri 184. Kwa hiyo, utaona tuna magari 11 ya ziada na tutaangalia mazingira ambayo tuna ulazima wa kuongeza gari kwenye Halmashauri, tutaongeza. Kwa hiyo, nimhakikishie

Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafanya tathmini kuona magari yaliyopo Geita Vijijini na Mjini na uhitaji na hivyo tunaweza kufanya maamuzi. Kwa hiyo, tutafanya hivyo kwa kadri ya mazingira. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itajenga vyumba vya kuhifadhia maiti katika Vituo vya Afya vya Nzihi pamoja na Kiponzero? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kiswaga, swali linahusu magari. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jackson Kiswaga, Mbunge wa Jimbo la Kalenga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ilishatoa maelekezo ya Halmashauri zote kuanza kwa kutumia mapato ya ndani kwa ujenzi wa miundombinu ambayo iko ndani ya uwezo wao ikiwemo majengo ya kuhifadhia miili ya marehemu kwa maana ya mochwari. Kwa hiyo, naomba Halmashauri ya Wilaya ya Iringa iangalie uwezekano wa kuanza ujenzi wa mochwari kwenye vituo vya afya vya Nzihi na Kiponzero. Pia Serikali tukipata fedha, tutaunga mkono juhudi hizo za Halmashauri. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, swali la nyongeza.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Halmashauri ya Wilaya ya Same ina majimbo mawili ambayo moja ni la Mashariki na Magharibi na yako mbalimbali sana; lakini Hospitali ya Wilaya iko upande mmoja tu wa magharibi na hata kituo cha afya kilichoko mashariki

hakina gari la wagonjwa. Mheshimiwa Waziri, naomba hili aliangalie na aniambie atafanya nini hapa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna baadhi ya vituo vya afya viko mbali sana kutoka Hospitali za Halmashauri ziliko ikiwemo kituo hiki cha afya ambacho Mheshimiwa Mbunge amekitaja. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafanya tathmini na kuona uwezekano wa kupata gari la wagonjwa kwa ajili ya kituo hiki cha afya ili kuweza kusogeza huduma kwa wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kasalali Mageni, swali la nyongeza.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba mpaka sasa haina gari hata moja la uhakika la wagonjwa; na ni Halmashari ya Wilaya ambayo imeundwa na majimbo mawili; Jimbo la Kwimba na la Sumve. Mpaka sasa kwenye Jimbo la Sumve hakuna kabisa *ambulance:* Mheshimiwa Waziri huoni kwamba umefika wakati wa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba yenye majimbo mawili na Halmashauri zote zenye majimbo mawili kugawiwa *ambulance* kwa kuzingatia kwamba kila Jimbo lipate *ambulance* yake?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la

nyongeza la Mheshimiwa Kasalali Mageni Mbunge wa Jimbo la Sumve, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nipokee taarifa ya Halmashauri hii ya Kwimba kwamba haina gari la uhakika hata moja la wagonjwa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha wananchi wetu wanapata uhakika wa huduma za rufaa na dharura. Kwa hiyo, tutahakikisha tunapata gari kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kugawa magari mawili kwenye Halmashauri zenye majimbo mawili, tutafanya tathmini kulingana na uhitaji kwa kadri ya vigezo vya kitaalamu na tutaona, ziko Halmashauri zitapata magari zaidi ya moja na pia ziko Halmashauri ambazo zinaweza zikapata gari moja. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, sasa aulize swali lake.

Na. 119

**Mpango wa Serikali Kuugawa Mkoa wa Tanga**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaugawa Mkoa wa Tanga ili kuongeza ufanisi katika eneo la Utawala Bora?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi Mbunge wa Jimbo la Mlalo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuanzisha Mkoa, Wilaya na Tarafa mpya umebainishwa kupitia Sheria ya Uanzishwaji wa Mikoa na Wilaya Sura ya 397 *(The Regions and Districts Establishment Procedure) Act, 2020*) na Mwongozo wa vigezo vya Maeneo Mapya ya Utawala wa mwaka 2014.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria hii, hatua ya awali inahusisha kupata ridhaa ya Vijiji, Kamati za Maendeleo za Kata, Mabaraza ya Madiwani ya Halmashauri zilizomo katika Mkoa, Kamati za Ushauri za Wilaya, na Kamati ya Ushauri ya Mkoa Mama. Baada ya hatua hiyo, maombi hayo yanawasilishwa Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa ajili ya uhakiki na tathmini na baadaye kuwasilishwa kwa Mamlaka husika kwa maamuzi kadri itakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais TAMISEMI, haijapokea wasilisho la mapendekezo ya kugawa Mkoa wa Tanga. Hivyo, nashauri taratibu za uanzishwaji wa maeneo mapya ya utawala zifuatwe. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali ambayo sisi kule mkoani katika hatua ya *RCC* tulikaa, sasa sijui yalikwamia wapi? Nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza: Kwa kuwa mchakato huu huwa unaandaliwa na wataalamu na ambao wako chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Je, kama alivyoeleza kwamba hawajapokea wasilisho, hawaoni tu kwamba Mkoa wa Tanga ndiyo mkoa pekee nchini ambao una wilaya nane na una Majimbo ya Uchaguzi 12 na Halmashauri 11? Sasa ni lini Serikali yenyewe tu itaweza kufanya maamuzi ya kuugawa mkoa huu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, tunaposema utawala bora ni pamoja na upelekaji wa huduma kwa wananchi. Sasa

wataalamu hawa katika ngazi za elimu na afya wanapata taabu kubwa sana kwa sababu wanatumikia eneo kubwa la kiutawala: Ni lini sasa Serikali itatenda kama inavyosema kuhusu eneo zima la utawala bora?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi Mbunge wa Jimbo la Mlalo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunafahamu Mkoa wa Tanga ni miongoni mwa mikoa yenye Halmashauri nyingi na ni mkoa mkubwa na maana yake kunakuwa na changamoto za aina yake katika uendeshaji. Ila kwa mujibu wa sheria, uanzishaji ni lazima uanzie ngazi ya mkoa wenyewe kama ambavyo sheria hii inaelekeza. Kwa hiyo, pamoja na kwamba Serikali kwa maana ya Serikali Kuu inaona, lakini wajibu wa Halmashauri, mkoa wenyewe, na vijiji utekelezwe ili tuweze kuanzisha mkoa huu kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusiana na changamoto ya ukubwa wa mkoa ambao unapelekea wataalamu wa afya na elimu kushindwa kutekeleza majukumu yao ya utawala bora, tunaendelea kuwezesha kwa kadri ya ukubwa wa mkoa kwa maana ya miundombinu, usafiri na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, jambo la msingi ni kuleta hoja hiyo ili Serikali iweze kuchukua maamuzi stahiki. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii kuuliza swali la nyongeza. Mkoa wa Morogoro ni mkubwa sana ambapo maombi tulishapitisha kwenye kamati zote za mkoa mpaka

*RCC* na maombi yalishakuja mpaka TAMISEMI. Sasa ni lini Serikali itaugawa huu mkoa ambao ni mkubwa sana? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI unao uhuru wa kujibu hilo swali au uje ulijibu siku nyingine kama swali la msingi, kwa sababu linaashiria kwamba taarifa zilishakuja Wizarani. Sasa kama wewe huna hapo, una uhuru wa kujibu sasa au kuja kujibu kama swali la msingi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba lije kama swali la msingi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dunstan Kitandula swali la msingi.

**MHE. DUNSTAN KITANDULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru; naomba niulize swali moja la nyongeza. Ugawaji wa Mkoa wa Tanga ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano alipokuja kwenye Mkoa wa Tanga, na hii ilikuwa ni baada ya Wabunge wa Mkoa wa Tanga kumuomba kwamba jambo hili tumeshalijadili kwenye *RCC*.

Je, hata baada ya ahadi ya Mheshimiwa Rais bado tunatakiwa jambo hili tena kulijadili kwenye mkoa kwa mara nyingine?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, nadhani unaweza ukarejea majibu yako.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dunstan Kitandula kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kadri ya majibu yangu ya jibu la msingi, kwamba kuna taratibu ambazo zipo kwa mujibu wa sheria, na Mheshimiwa Rais alitoa ahadi hiyo, na sisi ahadi hiyo na sisi ahadi za viongozi wetu, Mheshimiwa Ris na

Mheshimiwa Makamu Rais, Waziri ni maelekezo ni maelekezo tutafanya kazi hiyo. Hata hivyo niwaombe tufuate utaratibu ule kwa kadri sheria ilivyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ni vizuri wataalam wanaowaandalia majibu Waheshimiwa Mawaziri wetu wakawa wanakumbuka majibu yanayotolewa na mawaziri katika mabunge yaliyopita. Mwaka 2021, Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Ummy Mwalimu...

**SPIKA:** Kwanza ngoja ngoja nirekebishe hapa kwa sababu hap ani Bungeni, Bunge la Kumi na Moja, maswali yake hayavuki Bunge la Kumi na Mbili, vivyo hivyo majibu yaliyotolewa hapa hayavuki, uliza swali lako la msingi.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, mwaka 2021, Mheshimiwa Ummy Mwalimu akiwa Waziri wa TAMISEMI, alijibu katika Bunge lako kuhusu swali hili lililoulizwa hapa kwamba tayari Mkoa wa Tabora, Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Tanga, mapendekezo yake ya kugawiwa yako mezani kwa Mheshimiwa Rais; na la kuzingatia ni kuwa Mheshimiwa Rais alitoa majibu kwamba tusubiri uchumi wetu utengemae ili mikoa ile igawanywe.

Kwa kuzingatia majibu hayo ambayo yalitolewa na Waziri wa TAMISEMI hapa, sisi Mkoa wa Morogoro tayari tulishamaliza huo mchakato ndiyo maana Waziri akasema kwamba yako mezani kwa Mheshimiwa Rais.

Je, ni lini Serikali itagawa Mkoa wa Morogoro?

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Asenga, si maana yake majibu ulishapewa kwamba uchumi utengemae, kwa hiyo nadhani swali lako tayari lina majibu kwa hiyo uhitaji Naibu Waziri kujibu hapa. Mheshimiwa Priscus Tarimo, swali la nyongeza.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kumuuliza Waziri ni lini Serikali itakamilisha mpango wa kupanua Mji wa Moshi na hatimaye kuwa Jiji kama ilivyokuwa kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 15 Julai, 2016?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Unao uhuru wa kujibu swali hilo kama majibu unayo kama huna, lije kama swali la msingi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Priscus Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, narejea kwenye jibu langu la msingi, kwamba Halmashauri ya Moshi, inahitaji kuleta mapendekezo kwa mujibu wa taratibu zilizoelekezwa na sheria na sisi ofisi ya Rais TAMISEMI, tutafanya tathmini na baadaye kuwasilisha kwa mamlaka husika kwa ajili ya maamuzi husika.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Daudi Protus Venant, Mbunge wa Igalula, sasa aulize swali.

Na. 120

**Serikali Kuigawa Halmashauri ya Wilaya ya Uyui**

**MHE. VENANT D. PROTAS** aliuliza:-

Je lini Serikali itaigawa Halmashauri ya Wilaya Uyui, ili itoe Halmashauri nyingine ya Igalula kwa kuwa inakidhi vigezo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daud Protas Venant, Mbunge wa Jimbo la Igalula kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, halmashauri huanzishwa kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa Sura ya 287 na 288 pamoja na Mwongozo wa Uanzishwaji wa Maeneo ya Utawala wa Mwaka 2014. Mwongozo huo umeainisha vigezo na taratibu zinazopaswa kufuatwa ili kuanzisha halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria hii, hatua ya awali inahusisha kupata ridhaa ya vijiji, Kamati za Maendeleo za Kata, Baraza la Madiwani la Halmashauri, Kamati ya Ushauri ya Wilaya *(DCC)* na Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC). Baada ya hatua hii, maombi hayo yanawasilishwa Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa ajili ya uhakiki na tathmini na kuwasilishwa kwa Mamlaka husika ili itoe uamuzi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais TAMISEMI haijapokea maombi ya kuigawa Halmashauri ya Uyui. Hivyo, nashauri taratibu za uanzishwaji wa maeneo mapya ya utawala zifuatwe. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daudi Protas Venant, swali la nyongeza.

**MHE. DAUD P. VENANT:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza nishukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri yametia moyo kwa wana Igalula. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, tulishafanya mchakato mara kwanza tukapitia mchakato wote kama alivyoutaja, tulivyofika kwenye hatua ya mwisho kwenye kikao cha *RCC*, walisema mchakato huo bado. Lakini sasa unavyosema tumepita kwenye mchakato huo huo na tayari *document* zimetayarishwa kwa ajili ya vikao hivyo, sasa Serikali kupitia

kwako Waziri hauoni haja ya kutoa maelekezo kwenye *RCC* wao sio hatua ya mwisho kutoa maamuzi waziachie document zije Wizara ili ziendelee na machakato mwingine?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Halmashauri ya Wilaya ya Uyui, ni kubwa sana na jiografia yake ni kila unapokwenda unaikuta Uyui. Sasa hamuoni kama Serikali kutoa maelekezo ya kina kwa zile halmashauri ambazo ni zenye *competition* ili kuweza kuzigawa ili kurahisisha huduma bora kwa wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Daud Protas Venant, Mbunge wa Jimbo la Igalula kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema katika swali lake, kwamba walifanya mchakato wa awali, lakini kwa namna moja ama nyingine haukukidhi vigezo lakini wamefanya mchakato wa pili ambao uko ngazi ya mkoa, kwa maana ya kufanya *RCC*. Sasa tunaelekeza, Mkoa wa Tabora kutekeleza wajibu wao kutimiza sheria hii, kwa maana ya kufanya vikao vya *RCC,* ili kupitia maombi hayo na baadaye kuwasilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kwa kadri ya mwongozo.

Mheshimiwa Spika, lakini pili, kuhusiana na maelekezo ya kugawa halmashauri hii kwa sababu ni kubwa itakuja kulingana na tathmini ambayo itafanyika baada ya *RCC* kuwasilisha maombi hayo ofisi ya Rais TAMISEMI. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anton Mwantona swali la nyongeza.

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini

Serikali itaipa hadhi Mji Mdogo wa Tukuyu kuwa halmashauri kamili hasa baada michakato yote kuwa imeshakamilisha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, unaona uhuru wa kujibu kama swali la nyongeza au swali la msingi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba swali hili lije kama swali la msingi.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Oran Manase Njeza, swali la nyongeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Mimi ningependa kujua; kwa vile mchakato wa kupandisha hadhi ya Mji Mdogo wa Mbalizi, ambao ni mamlaka kuwa halmashauri ya mji ilishapitishwa kiwilaya na mchakato vilevile ulishapitishwa kimkoa. Je, ni lini sasa Serikali itaipandisha hadhi hii Mamlaka ya Mji kuwa Halmashauri ya Mji wa Mbalizi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kama unayo, kama huna lije kama swali la msingi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)**: Mheshimiwa Spika, ahsante saa. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijiji kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge amesema katika swali lake taratibu za awali za Mbalizi kupandishwa hadhi kuwa Halmashauri ya Mji zilishafanyika, naomba tulichukue hilo tufuatilie kama lilishawasilishwa Ofisi ya Rais TAMISEMI, na baada ya hapo tutafanya tathmini kwa mujibu wa sheria na tutawapa mrejesho hatua ambayo itafuata. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omar Kigua swali la nyongeza.

**MHE. OMAR M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi, ina vijiji 102, vitongoji 611, kata 21 na tarafa nne.

Je, ni lini Serikali italigawa Jimbo hili la Kilindi? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)**: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue hoja ya Mheshimiwa Mbunge twende tukajiridhishe na takwimu ambazo amezisema, tuone vigezo na baadaye tuweze kufanya maamuzi, baada ya tathmini hizo tutawapa mrejesho nini hatua inaweza kufuata baada ya tathmini hiyo, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamisi, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 121

**Kiongozi Kupewa Nakala ya Sheria ya Maadili**

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza-:

Je, Serikali haioni umuhimu wa kutoa nakala ya Sheria ya Maadili kwa Viongozi nchini ikiwemo Wabunge na Viongozi wengine ili kuepuka kukiuka Sheria hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Deogratius Ndejembi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamisi (VITI MAALUM) kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika; Serikali imekuwa ikitoa nakala za Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na. 13 ya Mwaka 1995 kwa Viongozi. Serikali hutoa nakala hizo kupitia mikutano, warsha, semina, makongamano na maonyesho mbalimbali. Kati ya mwaka 2015 hadi 2022 Jumla ya nakala 12,400 za Sheria zilichapishwa na kutolewa kwa Viongozi na wadau wengine. Aidha, nakala tepe *(soft copy)* ya Sheria imewekwa katika tovuti ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ambayo ni *www.ethicssecretariat.go.tz*. Hivyo, Viongozi wa Umma wakiwemo Waheshimiwa Wabunge wanashauriwa kutembelea tovuti na kupata nakala ya Sheria.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, swali la nyongeza.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kujibu kwa ufasaha na umejibu vizuri kwa kweli. Lakini nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa ofisi ya maadili ni ofisi ya muungano lazima itakuwa na wafanyakazi wa muungano waliokuwepo Zanzibar nao pia wanahusika.

Je, katika hii warsha na makongamano na semina ambazo unazitoa, kwa upande wa wafanyakazi waliokuwepo Zanzibar, nao pia wamepatiwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa unahitajika lazima ofisi yako iwe na mjengo Zanzibar wa kufanyia kazi.

Je, ofisi yako unayofanyia kazi kwa Zanzibar iko sehemu gani kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamisi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi, kwamba viongozi wote wa Tanzania na Tanzania Zanzibar wamepewa semina hizi na kufanyiwa warsha mbalimbali na makongamano mbalimbali. Kati ya mwaka 2015 hadi 2022 jumla ya viongozi 28,450 wa pande zote mbili za Taifa letu wamefanyiwa semina hizi na warsha hizi wakiwemo Waheshimiwa Wabunge.

Kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, kwamba tutaendelea kutoa warsha hizi na semina hizi kwa waheshimiwa na viongozi wengine mbalimbali ili wote tuweze kuwa na uelewa mmoja kuhusiana na masuala ya maadili.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili, ofisi za maadili zipo kila mahali, kila kanda, kila mkoa. Kwa hiyo, hata upande Zanzibar ofisi hizi za maadili zipo katika kila mkoa. Ndiyo maana hata fomu zetu zile tunazozijaza za maadili tuna uwezo wa kuzirudisha katika ofisi zetu hizi zilizo maeneo mbalimbali ya Taifa letu. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 122

**Mradi wa Kuzuia Mafuriko Mto Msimbazi**

**MHE. AGNESTA L. KAIZA** aliuliza:-

Je, Serikali imefikia hatua gani katika utekelezaji wa mradi wa kuzuia mafuriko katika Mto Msimbazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu Muungano na Mazingira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Agnes Lambert Kaizer, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mradi huu kwa sasa uko katika hatua za kufanya uhakiki wa taarifa na mali za wananchi wanaopaswa kupokea fidia na kusainiwa kwa mkataba baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Benki ya Dunia. Mradi huo unategemewa kuanza rasmi mwezi Julai, 2022.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira inaamini kuwa utekelezaji wa mradi huu utawezesha kuondoa kabisa tatizo la mafuriko katika Bonde la Mto Msimbazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, swali la nyongeza.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Mradi huu umechukua muda mrefu kutekelezwa na majibu ya Serikali muda wote yamekuwa ni haya; na kipindi kutoka sasa hadi Julai, ambapo Mheshimiwa Waziri amesema mradi huu utakuwa umetekelezwa ni takribani miezi mitatu tu. Sasa swali langu, Mheshimiwa Waziri analihakikishia Bunge hili Tukufu kwamba kufikia kipindi hicho, taratibu zote ikiwa ni pamoja na kulipa fidia wananchi watakaoguswa na mradi zitakuwa zimekamilika?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; Bonde la Mto Msimbazi ni chanzo kikuu cha mafuriko katika barabara iendayo Kariakoo eneo la Jangwani. Barabara hii inaelekea

katika kitovu cha uchumi wa nchi. Sasa, swali langu kwa Serikali;

Je, ni mkakati gani wa dharura umeandaliwa kwa kipindi hiki ambacho mvua zinaendelea kwa kasi katika Jiji la Dar es Salaam?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, wa Viti Maalum, Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tunapotaka kufanya jambo lolote, hasa jambo ambalo limezunguka kwenye maeneo ya makazi ya watu si kwamba tu tunaangalia kwenye fidia lakini kuna baadhi ya mambo ya msingi huwa tunaangalia. Kwanza katika mazingira kuna kitu kinaitwa *EIA, Environment Impact Assessment*; kwa hiyo kwanza tunaziangalia athari za kimazingira. Je, tutakapofanya hilo jambo tunaweza tukawaathiri vipi wananchi kwenye hilo. Lakini pia kuna kitu tunakiita *PA property assessment*, kwamba je, mali za wananchi wanavipando vyao, wana nyumba zao wana makazi mengine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa ufupi ni kwamba hili jambo tumeshalikali kitako na tayari tathmini inaendelea ni mtoe hofu Mheshimiwa, tunalithibitishia Bunge hili pamoja na hizo tathmini ambazo ambazo zinaendelea lakini bado tunaendelea na kama tulivyoeleza kwamba miezi michache inayofuata ujenzi huu unaanza.

Mheshimiwa Spika, lakini je, tunajuhudi au jitihada gani katika kuzuia mafuriko; nimwambie tu kwamba tumeshakaa pamoja, sisi Ofisi ya Makamu wa Rais, pamoja na maafisa

wetu wa mazingira tumekaa na halmashauri tumekaa watu wa *TARURA*, tumekaa na watu wengine ili kuona namna ambavyo tunaweza tukapunguza angalau hizo athari za mafuriko, zikiwepo za kutengeneza vi-*streams* vidogovidogo vitakavyoyaondosha maji pale na kuyapeleka maeneo ya bahari ili pale yasituwame na yakapunguza athari kwa wananchi. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abbas Tarimba swali la nyongeza.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mahiri kabisa kwamba ninaamini kabisa kwamba anafahamu changamoto hizi zilivyo. Kwa kuwa mradi huu wa Bonde la Mto Msimbazi ni hoja kuu ya Jimbo la Kinondoni, na kwa kuwa sasa Serikali inakwenda kuanza mradi huu Julai, 2022. Je, Serikali iko tayari sasa kutoa mpango wa utekelezaji, kwa maana ya *program and planning of action,* ili wananchi wale wa mto Msimbazi waweze wakajua ni lini wanatakiwa wanaondoke na ni lini kabisa watatakiwa waweze kupata fidia zao pale itakapobidi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tarimba Abbas, Mbunge wa Jimbo la Kinondoni, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue fursa hii nimpongeze sana Mheshimiwa Abbas kwa kuwa Jimbo lake na yeye ni moja ya miongoni mwa Majimbo yaliyopita katika Mto Msimbazi lakini anafanya kazi kubwa ya kutusaidia kama Serikali kwa kuwaelewesha wananchi. Namwambia Mheshimiwa Tarimba Abbas kwamba aende akawaambie wananchi kwamba tathmini inaendelea. Imeshaanza kama miezi mitatu iliyopita na kwa kuwa inaendelea matokeo lazima wananchi tutawaambia. Kwa hiy,o naomba

akawaambie wananchi wa Kata za Kinondoni, Kata za Mzimuni, Kata ya Magomeni, Kata ya Kigogo na maeneo mengine yaliyopita mto huu kwamba tathmini itakapotoka majibu watapewa na lazima tuwaambie kabla ili tusije tukawavamia tukaja tukatengeneza mivutano baina ya wananchi na Serikali. Nakushukuru.*(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Simai swali la nyongeza.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi kuweza kunipa nafasi hii kuuliza swali dogo la nyongeza.

Je, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina mpango gani wa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar juu ya kuandaa mradi utakaoenda kuzuia maji ya bahari kuendelea kumeza kingo kule maeneo ya Nungwi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Simai, Mbunge na mtumishi wa wananchi wa Jimbo la Nungwi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inayompango ama ilishakuwa na huo mpango na ndiyo maana tayari kuna baadhi ya kingo kwa upande wa Zanzibar ambazo tayari zimeshajengwa na hii ni kutokana na athari kubwa ya kimazingira ambayo ilifika wakati maji ya bahari yanaingia kwenye vipando vya wananchi ikiwemo mihogo, migomba ambayo haihimili maji ya chumvi. Pia maji haya yalikuwa yanaingia kwenye maeneo ya makazi. Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakaona kuna haja ya kushirikiana katika suala hili. Tayari yako baadhi ya maeneo kwa mfano Kisiwa cha Pemba maeneo ya Wete, Micheweni

na maeneo ya Unguja pia tumeanza. Namwambia Mheshimiwa kwamba katika bajeti ambayo tumeisoma juzi tutajitahidi tutenge fungu kwa ajili ya kulipa kipaumbele Jimbo lako kwa ajili ya kujenga hizo kuta. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Jimbo la Ubungo wameathirika sana na mafuriko ya mito Gide, Mto China na Mto Ng'ombe, ninavyoongea Mtaa wa Kibangu leo nyumba za wananchi 12 zimebomolewa na mto huo. Nauliza kwa nini Serikali isichukue hatua za dharula za kujenga gambiozi katika mito hiyo ili kuokoa maisha ya wananchi wakati tunasubiri mradi huo? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Profesa Kitila kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imefika wakati na imeona athari ambazo zinajitokeza hasa zinazosababishwa na mito hii mikubwa na hasa kipindi cha mvua kubwa kama hiki ambacho tukonacho. Namwambia Mheshimiwa Profesa kwamba wazo na fikra alilolitoa ni jambo ambalo tayari tumeshakaa na tumeshalifikiria, lakini kwa heshima ya wazo lake tunalichukua na tunazidi kwenda kulifanyia kazi. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Mtemvu swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa ndani ya Jimbo la Kibamba kuna

Mto Mbezi na Mto Mpiji ambao kwa muda mrefu wananchi wamedhurika sana na mafuriko, nyumba zao lakini pia na taasisi kama shule zimekuwa zikiondoka.

Je, Serikali ina mkakati gani sasa kukabiliana na hali hiyo katika mito hiyo miwili Mto Mbezi na Mto Mpiji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mtemvu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunayo mikakati mingi kwa sababu tunafahamu athari za kimazingira zinazosababishwa na mito hii ni athari kubwa. Mwisho wa siku zinaharibu vipando, zinaharibu makazi lakini pia zinaweza kuleta hata maradhi kwa sababu maji yakija yanakuja na takataka, yakirudi yanarudi maji peke yake takataka zinabakia kwa hiyo tunajua hata maradhi yanatokea. Kwa hiyo iko mikakati mingi kama Serikali ambayo tumeamua kuifanya, ikiwemo kwanza kuhakikisha kwamba tunajenga hizo kingo lakini pia tunasaidia katika kuwaelimisha wananchi namna ambavyo wanaweza wakapunguza hizo athari na wakaepukana na hizo athari zinazosababishwa na mito hii. Nakushukuru.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Afya. Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Bahati Ndingo.

Na. 123

**Kuboresha Bima za Afya za wazee zitumike Mikoani**

**MHE. BAHATI K. NDINGO K.n.y. MHE. TASKA R. MBOGO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha Bima za Afya za Wazee ili ziweze kutumika wakiwa nje ya Mikoa ambayo wamepewa Bima hizo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Mollel majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ikiendelea na mchakato wa kukamilisha Muswada wa Bima ya Afya kwa wote, Serikali inaelekeza vituo vyote vya huduma kuwapatia huduma wazee wasio na uwezo waliotimiza vigezo hata wakiwa nje ya maeneo yao. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Bahati Ndingo swali la nyongeza.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, pamoja na kwamba huduma hizi za Wazee za kutibiwa bure zinatolewa kwenye hospitali zetu, lakini tunaona wazee wetu wanapofika kwenye hivi vituo wanakosa dawa za muhimu wakati mwingine wanapata usumbufu mkubwa kulingana na umri wao. Sasa Serikali inayo mkakati gani kuhakikisha kwamba endapo dawa zinakosekana wazee hawa wanafanyiwa utaratibu maalum wa kutafutiwa dawa hizo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali lingine ni kwamba tunao utaratibu ambao umekuwa ukisemwa na Serikali wa Bima ya Afya kwa wote. Je, ni lini sasa Serikali inaenda kukamilisha utaratibu huu ili wananchi wote, wazee na wengine waweze kupata huduma hii muhimu kwenye hospitali zao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge. Moja ni kama wazee wakifika mahali, dawa haiko hospitalini ni utaratibu gani umewekwa kuhakikisha kwamba wanapata dawa bila kusumbuliwa.

Mheshimiwa Spika, kikubwa ni kwamba kuhakikisha hakuna dawa inayokosekana kwenye hospitali zetu hicho ndiyo cha kwanza. Lakini sasa hivi tunaelekeza maduka ya Bima ya Afya ambayo yako kwenye maeneo yetu ya hospitali ambayo yanaendeshwa kama *private* yaweze vilevile kutoa huduma hiyo kwa wazee bila kuwa-*charge* wakati mchakato wa bima ya afya unakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia suala la Bima ya Afya kwa watu wote kama alivyoelezea Waziri wa Afya hapa hivi karibuni kwamba tayari limeshafika kwenye Baraza la Mawaziri na michakato mingine ya Serikali.

Sasa Serikali imeshauri lirudi Bungeni lakini lirudi vilevile kwenye chama, kwa maana linatakiwa lije kwetu sisi Wabunge, likija kwetu Wabunge tuliangalie kwa makini yake kwa sababu kupitisha ni jambo moja, lakini je litakuwa na athari gani wakati wa utekelezaji. Hilo nalo tunaenda kulifanya na likirudi litaingia kwenye Kamati ya Huduma za Jamii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge ushauri wenu sana ni muhimu wakati wa utekelezaji wake na kuangalia mambo yote ili wakati wa utekelezaji Wabunge vilevile tusiweze kulaumiwa kule na wananchi. Kwa hiyo, likirudi ushauri wenu unategemewa zaidi ili tuweze kuikamilisha mara moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, sasa aulize swali lake.

Na. 124

**Fedha za ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji ya Mgambalenga – Kilolo**

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji ya Mgambalenga Wilayani Kilolo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Justine Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imetenga fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu ya Mgambalenga yenye hekta 3,000 Wilayani Kilolo. Ujenzi huo utahusisha ukamilishaji wa mfereji mkuu wenye urefu wa kilometa 14 pamoja na maumbo yake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Justin Nyamoga swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ninayo maswali mawili ya nyongeza pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza katika skimu hizi ikiwemo hii ya Mgambalenga lakini pia skimu za Ruaha Mbuyuni na nyingine gharama za ulipiaji wa vibali katika bonde zilipanda kutoka Shilingi 70,000 hadi Shilingi 150,000 zaidi ya asilimia 100. Sasa ningependa kujua ni mpango gani wa Serikali wa kupunguza hizi gharama maana gharama za kilimo zimeongezeka kwa hiyo inakuwa ni vigumu wakulima

wale wa kujikimu kuweza kumudu kulipia vibali kwa ajili ya umwagiliaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili katika Kata ya Nyanzwa skimu ya umwagiliaji iliyoko pale ambayo ni ahadi ya Mawaziri Wakuu kadhaa bado haijatekelezwa, pamoja na juhudi kubwa za kuifatilia zilizofanywa na mimi mwenyewe hata Diwani wa kule amekuja kufuatilia. Sasa ningependa kujua kwa sababu ndiyo uhai wa watu wa kule kwenye kilimo cha vitunguu.

Je, ni lini Serikali itajenga ile skimu kwa kuzingatia pia mwaka huu hali ya umwagiliaji imekuwa ngumu na hali ni mbaya, ni lini Serikali itafanya ujenzi wa skimu ya umwagiliaji Nyanzwa? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la kwanza kuhusu gharama ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge gharama zimekuwa juu tofauti na ile gharama ya awali ambayo ilikuwepo. Tumeielekeza Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kukutana na mamlaka ya bonde husika kukaa na kuangalia uhalali wa gharama hizo ili tumpunguzie adha mkulima.

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu mradi wa Nyanzwa ni kweli mradi huu Mheshimiwa Mbunge amekuwa akiufuatilia sana na ninampongeza sana kwa hili. Tayari pale tuna miundombinu ya hekta 300 na tunachangamoto kubwa ya uhaba wa maji ya umwagiliaji, katika bajeti ya mwaka 2022/2023 Tume itafanya usanifu wa kina wa bwawa kuvuna maji ya mvua na usanifu huo pia utahusisha eneo la hekta 9,000 ili kuwahudumia wakulima wengi zaidi na baadae tutajenga kama ambavyo usanifu utakuwa umeelekeza.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, skimu ya umwagiliaji iliyopo katika eneo la Chikopelo Wilaya ya Bahi imeacha kufanya kazi kwa muda mrefu baada ya mwekezaji kuondoka. Nini kauli ya Serikali katika kuifufua skimu hii ili kuwaondolea umaskini wananchi wa eneo hilo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fatma Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Dodoma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunafahamu ya kwamba moja kati ya eneo ambalo litasaidia sana kukuza kilimo chetu katika nchi yetu ya Tanzania ni kilimo cha umwagiliaji. Namuahidi Mheshimiwa Mbunge ya kwamba Wizara tumejipanga kuhakikisha tunazipitia skimu zote ili kuweza kufahamu *status* zake kwa maana tujue ni miradi ipi haifanyi kazi, ipi inafanya kazi lakini ipi imekwamishwa na nini, ili tuitatue na kuwafanya wakulima wetu walime kilimo cha umwagiliaji. Moja wapo ya maeneo ambayo tutayapitia ni pamoja na eneo la Chikopelo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aloyce John Kamamba swali la nyongeza.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Katika Wilaya ya Kakonko ambako Jimbo la Buyungu lipo zipo skimu za Katengera, Gwanumpu, Ruhwiti na Muhwazi

ambazo miundombinu yake imeharibika na haifanyi kazi vizuri.

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu hiyo ili waweze kuendelea na kazi kama ilivyokusudiwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aloyce kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika miradi aliyoisema Mheshimiwa Mbunge ukiacha mradi wa Ruiche hii miradi mingine miwili tutaiingiza katika mipango yetu kuhakikisha kwamba inafanya kazi katika utaratibu ambao nimeuanisha awali wa kuipitia nakuona changamoto ulizonazo.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Ruiche tumeshapata *no objection* na hivi sasa tutaelekeza kazi ya usanifu ifanyike ili baadae tuanze kazi ya ujenzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Mayenga swali la nyongeza.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Katika Kata ya Itilima, Wilaya ya Kishapu kuna Kijiji cha Mwamala na katika Kata ya Mwaduiluhumbo kuna kijiji cha Nyenze, katika Wilaya hii ipo miradi ya skimu za umwagiliaji ambayo Serikali ilitoa pesa lakini baada ya kutoa pesa zile hazikutosha, katika Jimbo hili la Kishapu wakinamama katika maeneo haya wanapata shida sana kutokana na hali halisi ya ukame katika maeneo haya.

Je, ni lini Serikali itatupatia pesa katika skimu hizi mbili za Nyenze pamoja na Mwamala ili wananchi waweze kufaidika? Kwa sababu skimu hizi za umwagiliaji endapo kama zikikamilika maji yatasaidia mifugo pamoja na binadamu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Shinyanga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji amekuwa akifanya ufuatiliaji mara kwa mara ofisini kwetu na ninamuahidi kwamba katika bajeti yetu ambayo tutaisoma mwezi ujao tutaainisha miradi ambayo itafikiwa na miradi hii pia tutaifikia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswalli ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 125

**Ujenzi wa Mabwawa ya Maji - Mbulu**

**MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kujenga mabwawa katika Jimbo la Mbulu Vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Jimbo la Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya maji katika Wilaya ya Mbulu Vijijini kwa lengo la kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji. Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, ujenzi wa miradi ya maji ya visima virefu kwenye vijiji vya Ng'orati, Maretadu Juu, Labay, Genda,

Masqaroda, Mewadani, miradi ya maji ya Singu na ukarabati wa visima katika vijiji vya Domanga, Eshkesh unaendelea. Miradi hiyo itakamilika Septemba, 2022 na itaboresha huduma ya maji katika Wilaya ya Mbulu Vijijini kutoka asilimia 61 hadi kufikia asilimia 76 ifikapo Desemba, 2022.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa mabwawa hasa katika maeneo kame unalenga kukusanya maji yaweze kutumika wakati wa kiangazi ili kuhakikisha shughuli za kilimo na ufugaji zinaimarika.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali itaendelea kuainisha maeneo ya ujenzi wa malambo na mabwawa madogo katika Wilaya ya Mbulu Vijijini ili kukusanya maji kwa ajili ya shughuli za kiuchumi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mabwawa ambayo yanajengwa na tumeleta kwenye Wizara yako, Bwawa la Mungahai, Dirimu, Yaeda Chini, Masieda, Endagichani, Basodere, Eshdeshi, Getire na Haribapeti.

Je, ni lini unatujengea mabwawa haya ambayo tumeshayaleta kwenye Wizara yako?

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwa kuwa Waziri alikuja Haydom na akaahidi kwamba tusubiri wali wa kushiba unaonekana mezani, na akaahidi kisima cha Haydom.

Je, ni lini kinachimbwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Massay kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na mabwawa, mabwawa haya yapo katika ngazi mbalimbali za utekelezaji na maeneo mengi ya nchi tunafikiria kuchimba mabwawa kwa lengo la kuhifadhi maji ya mvua kutumika wakati wa kiangazi, hivyo mwaka ujao wa fedha naamini maeneo kadhaa yatapata huduma hii.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusiana na kisima alichokiahidi Mheshimiwa Waziri, ahadi ni deni lazima tutakuja kuchimba hiki kisima, tutaangalia bajeti hii kabla haijakamilika mwaka huu wa fedha na ikibidi basi mwaka ujao wa fedha kisima hiki kitapatikana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu hayo kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo, sasa aulize swali lake.

Na. 126

**Kujenga Gati Bagamoyo ili Kuvutia Watalii**

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga gati ya kuegesha boti na vyombo vya usafiri Bagamoyo ili kuvutia watalii kutembelea Mbuga ya Saadan?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu

swali la Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuendeleza miundombinu ya kisasa ya kuegesha vyombo vya usafiri katika pwani ya Wilaya ya Bagamoyo ili kuvutia watalii kutumia miundombinu hiyo kwenda kutembelea vivutio vya utalii katika mbuga ya Saadan pamoja na Visiwa vya jirani.

Mheshimiwa Spika, katika kutimiza azma hii, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari nchi kwa maana ya *TPA* iko katika hatua za mwisho za kuhuisha mpango kabambe wa kuendeleza miundombinu ya bandari nchini ambao utaainisha mahitaji sahihi ya miundombinu ya gati zinazotakiwa kujengwa kwa ajili ya kuegesha boti na vyombo mbalimbali vya usafiri katika Bandari ya Bagamoyo. Maandalizi ya Mpango Kabambe yanatarajiwa kukamilika Juni, 2022 na kufuatiwa na usanifu wa kina ili kupata taarifa za msingi ikiwa ni pamoja na gharama za utekelezaji wa mradi huo. Kazi hii itafanyika katika Mwaka wa Fedha 2022/2023. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Muharami Mkenge, swali la nyongeza.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Zanzibar inatembelewa na watalii wengi sana kwa kipindi cha mwaka mzima na wengi wanatamani kuja Bagamoyo kuja kuangalia vivutio vilivyopo pamoja na kutembelea Mbuga ya Wanyama ya Saadan, lakini kikwazo kikubwa wanachokipata ni sehemu ya kupaki boti kwa ajili ya kushuka ili waweze kufanya utalii. Je, Serikali ina mpango gani kuliingiza suala hili katika bajeti ya mwaka ujao ili kuunga mkono juhudi za Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan katika suala zima la *Royal Tour*?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa shughuli nyingi sana za usafiri kati ya Bagamoyo na Zanzibar za mizigo

pamoja na abiria zinafanyika kwa boti za kawaida na majahazi ya kawaida. Je Waziri yuko tayari kutembelea Bagamoyo ili aone shughuli zinazoendelea pale ili alitilie umuhimu suala hili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo.

Sasa napenda kujibu maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza anataka kujua nini *committent* ya Serikali katika bajeti ijayo kwa ajili ya ujenzi wa haya magati. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumekuwa na mpango kabambe wa kuainisha bandari zote nchini ikiwemo na Bandari ya Bagamoyo katika ujenzi wa hizi gati na nimhakikishie kwamba tayari kwenye mwaka wa fedha ujao, ambako tutasoma bajeti yetu, tumetenga fedha kwa ajili ya kujenga gati katika Bandari hii ya Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa, kwa mwaka huu wa fedha ambao unaendelea, tayari tumetenga kiasi cha Shilingi milioni 68 kwa kushirikiana na wenzetu wa Maliasili na Utalii ambapo tumeweka *front dock yard* kwa ajili ya kupokea majahazi, lakini pamoja na boti kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, swali la pili anataka kujua ama anaomba nitembelee Bandari ya Bagamoyo na nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na yeye mara baada ya Bunge la Bajeti, nitafika Bandari ya Bagamoyo kujiridhisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Sasa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 127

**Utaratibu wa Kukagua Magari Barabarani**

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA** aliuliza:-

Je, ukaguzi wa magari barabarani unahusisha vitu gani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali na Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi wa magari hufanywa kwa mujibu wa Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168 ya mwaka 1973 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2002 na kanuni zake. Ukaguzi wa magari uko wa aina mbili, aina ya kwanza hufanywa kwa mujibu wa Kifungu cha 81 ambao ni ukaguzi wa kawaida unaofanywa na askari barabarani. Ukaguzi huu huangalia nyaraka za gari, leseni ya dereva, uwezo wa gari, madai ya tozo za faini, pamoja na hali ya dereva.

Mheshimiwa Spika, aina ya pili ya ukaguzi hufanywa kwa mujibu wa Kifungu cha 83 ambapo Mkaguzi wa Magari hufanya ukaguzi kwenye maeneo maalum na baada ya kukagua hutoa hati ya ukaguzi kwa maana ya *PF* 93. Ukaguzi huu wa magari hufanywa ili kujiridhisha na uzima na usalama wa gari kama vile mifumo ya breki, umeme, *sterling*, matairi na kadhalika. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Angelina Malembeka, swali la nyongeza.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri yenye ufasaha zaidi, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, katika majibu yake ameelezea uwezo wa gari pia uzima na usalama wa gari. Sasa hivi kuna magari mengi yanayobeba vinywaji baridi kusambaza madukani kumekuwa na utaratibu wa makusudi kuyapanua na kuyatanua magari yale kiasi kwamba hata dereva inabidi aweke nondo ili aweze kuipata ile *site mirror* vizuri. Je, Serikali ina kauli gani kuhusiana wamiliki wa magari hayo ambao wanapanua kwa makusudi magari hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili kwa kuwa pia ameelezea uzima na usalama wa magari, tuna magari mengi yanayobeba takataka lakini magari yale yenyewe ni sehemu ya takataka. Kama ni kweli yanakaguliwa kuangalia uzima wake na usalama, Serikali ina kauli gani kuhusiana na magari yanayobeba takataka ambayo yenyewe pia ni takataka? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Malembeka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja kuhusu magari ya vinywaji baridi kupanuliwa kwa maana ya kuzidi uwezo wake wa kawaida, nadhani hili ni suala ambalo ni la viwango, tutashauriana na Wizara yenye dhamana ya Uchukuzi, na Wizara yenye dhamana ya Viwanda hili wanapokagua kwa maana ya *TBS,* magari yanavyoingia basi yazingatie uwezo na sura ya gari, sio ya upanuzi ambao unaathiri watumiaji wengine wa magari, kama alivyoeleza inatanuliwa mpaka

*site mirror* zinaongezwa kiasi ambacho kinaleta usumbufu, ili watakapotoa viwango vile basi askari wetu wa usalama barabarani wanapotimiza wajibu wao wa kuona magari yanayostahili kuwa barabarani basi watasimamia kwa mujibu wa miongozo hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu magari ya taka, ambayo amesema yenyewe ni takataka, nadhani nizielekeze mamlaka zinazoyaajiri magari haya kwa Mamlaka za Miji na Majini, wahakikishe kwamba wanateuwa wakandarasi wenye uwezo wa kutoa magari yanayofaa badala ya magari haya ya kubeba taka yenyewe yanakuwa sehemu ya uchafuzi wa miji yetu. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa tunakwenda Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 128

**Bei ya Kuunganisha Umeme**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE** aliuliza:-

Je, Serikali haioni ni kuwakandamiza Wananchi wa Itigi kwa kuondoa Miji kwenye bei ya kuweka umeme kutoka shilingi 27,000 hadi shilingi 320,000?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** aljibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali haikandamizi mwananchi yoyote, bali inawajali na kuwaunganishia huduma ya umeme kwa gharama zenye ruzuku ndani yake. Kati ya mwaka 2008 na 2013, gharama za kuunganisha umeme zilikuwa shilingi 455,104.76 ndani ya mita 30; shilingi 1,351,883.52 ndani ya mita 70; na shilingi 2,001,421.60 ndani ya mita 120 kwa maeneo ya Mijini na Vijijini. Gharama hizi ndizo zilizokuwa zinaakisi gharama halisi za kuunganisha umeme wa njia moja.

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2013, Serikali ilipunguza kwa kuweka ruzuku gharama za kuunganisha umeme kuwa shilingi 320,960.00 ndani ya mita 30, shilingi 515,617.52 ndani ya mita 70 na shilingi 696,669.64 ndani ya mita 120 kwa maeneo ya mijini. shilingi 177,000.00 ndani ya mita 30, shilingi 337,739.60 ndani ya mita 70 na shilingi 454,654.00 ndani ya mita 120 kwa maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwezi Januari, 2022 bei imerejea kwenye gharama za mwaka 2013 kwa maeneo ya mijini na shilingi 27,000 kwa maeneo ya vijijini. Gharama hizi zina ruzuku ya Serikali ndani yake. *TANESCO* inabaini eneo la miji na vijiji kwa kutumia Sheria ya Mipango Miji Namba 8 ya mwaka 2007.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE**: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu haya marefu ya Serikali na historia ambayo hapa haitusaidii sana, dhamira ya Serikali pamoja na kujenga Bwawa la Mwalimu Nyerere pamoja na kuweka mahela kwenye mafuta ya petroli ambao watumiaji wa petroli wala hawahusiki na umeme huu vijijini.

Je, ni lini sasa Serikali itaangalia namna iliyo bora ya kupatana na wananchi ambao wanahitaji kuweka umeme kama wanashindwa kupunguza bei ili wapatane naye basi alipe sehemu ya gharama na gharama nyingine azilipe polepole kulingana na makubaliano watakayokubaliana, Serikali iko tayari kufanya jambo hili?

Mheshimiwa Spika, pili, kulikuwa na bei wakati huo Mheshimiwa hapa amejibu amesema ilikuwa shilingi 177,000 na shilingi 27,000 huko vijijini kabisa, vijiji miji ambayo kama Itigi ambao wameiondoa sasa katika ile laki moja na sabini saba kuja laki tatu ishirini. Je, Serikali iko tayari kurudisha vile vijiji miji ambavyo kutokana tu kupimwa eti tayari ni mji! Je, wako tayari sasa kuturejeshea katika ile bei ya shilingi 177,000?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Yahaya Massare, Mbunge wa Manyoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kulipa gharama za kuunganishwa umeme awamu kwa awamu au taratibu, tumeshaanza kuufanyia mkakati na majadiliano yanaendelea kuona namna bora ya kuweza kufikia azma hiyo. Changamoto kubwa ni kwamba gharama za bidhaa zinabadilika mara kwa mara, kwa hiyo mtu akilipa kidogo kidogo kwa muda ambao tutakuwa tumekubaliana, akamalize ndani ya muda huo labda pengine itatusaidia, lakini akichukuwa muda mrefu na pengine kushindwa kumaliza ndani ya ule muda tuliokubaliana, tutajikuta huduma hii inakuwa ni changamoto kwa kuitekeleza.

Mheshimiwa Spika, tayari wataalam wetu wa *TANESCO* wanaendelea kuangalia namna bora ya kuweza kupunguza hizi gharama za kuunganisha umeme kwa awamu moja kwa wateja wetu ili kuweza kufika azma ya kuwaunganishia wananchi wote umeme, lakini hasa kwenye maeneo ya mijini kwa sababu gharama za vijiji tayari zimepunguzwa.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la pili, wenzetu wa *TANESCO* walishirikiana na wenzetu wa TAMISEMI kubaini na maeneo gani ya miji na ni maeneo gani ya vijiji na gharama ya vijijini ikabaki kuwa shilingi 27,000 na gharama za mijini zikasemwa hizi gharama nyingine ambazo tayari Serikali imeweka ruzuku ndani yake. Hata hivyo, Serikali ya Awamu

ya Sita ni sikivu kwa wananchi itaendelea kufanya kazi kuendelea kuona namna ambayo inaweza ikawafikishia huduma bora Watanzania hata kwa kufanya majadiliano mengine ya kuona maeneo gani ipeleke kwa gharama gani kwa ajili ya kufikisha azma ya wananchi wote kupata umeme.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na napenda niongezee kidogo kwamba ni dhahiri kwamba yapo maeneo ya miji, kwanza tafsiri yetu ya miji na vijiji inatokana na sheria ya TAMISEMI, lakini dhahiri kwamba yako maeneo ya miji na majiji manispaa ambayo yako pembezoni yana sifa zote za maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri tumebaini maeneo hayo na tumekubaliana na maombi ya Waheshimiwa Wabunge wengi pamoja na kwamba maeneo hayo yapo kwenye mipaka na miji na majiji lakini ukienda ukiona ni dhahiri kabisa kwamba yana sifa za maeneo ya vijiji kwa maana ya mazingira na hali ya kipato.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo katika bajeti ya Wizara ya Nishati tutatoa maelezo na utaratibu wa kuzingatia uhalisia wa maeneo haya katika kupanga bei ya kuunganisha. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kwa Serikali na Serikali kuweza kuwapatia Wabunge majibu, sasa nitaleta matangazo niliyonayo hapa mbele.

Kabla sijaleta matangazo nichukue fursa hii kwa niaba yenu wote, kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kuzindua ile makala maalum ya utalii maarufu kama *Royal Tour* hapa Tanzania. Siku ya jana imezinduliwa Arusha na inatarajiwa kuzinduliwa katika maeneo mengine Zanzibar na Dar es Salaam. *(Makofi)*

Kwa hiyo tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri aliyoifanya pamoja na wote walioshirikiana naye. Nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge na hapa uwa mnauliza sana maswali kwenye maeneo yenu vivutio vya utalii hata kama havimo kwenye ile Makala Maalum, lakini ni muhimu sasa kuanza kuvipa kipaumbele ili watalii wanapokuja waweze kufika katika hayo maeneo yetu pia ya uwakilishi. *(Makofi)*

Pia na sisi tuhamasike basi kufanya utalii wa ndani kama ambavyo tunaweza kuwalita wajumbe hapa Dodoma, basi tuwapeleke kwenye vivutio vya utalii hao wajumbe ili tuhamasishe utalii wa ndani. Nichukue fursa hii kuwapa pole Waheshimiwa Wabunge ambao walikuwa wameanza safari ya kuelekea Arusha, halafu ikabidi warudie njiani kwa sababu ya taarifa ambazo tulikuwa tumezipata hapa, kwa hiyo msiwe na wasiwasi Waheshimiwa Wabunge mtashiriki kwenye uzinduzi wa *Royal Tour* itakayofanyika Dar es Salaam. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, utaratibu utakapokamilika mtajulishwa, mtaenda kushiriki kikamilifu na Wabunge wote ambao watapata fursa ya kuwa Dar es Salaam siku hiyo ya tarehe 8, basi waungane na Mheshimiwa Rais kuhakikisha tunazindua kwa kishindo hapa nchini kuliko huko kwingine ambako nako imepokelewa vizuri sana. Kwa hiyo sisi kwa sababu ndio wahusika wenyewe, lazima tufanya jambo la tofauti.

Waheshimiwa Wabunge, nilete tangazo la wageni walioko Bungeni siku ya leo:-

Kwanza ni wageni wangu 10 ambao ni kikundi cha Tukuyu *Women Group* kutoka Mkoani Mbeya. Katika hawa wageni 10 yupo ndugu Liliani John Kapakala, Ndugu Fika Burtony Mkwakabungu, Ndugu Judith Godwini Mwakyusa, Ndugu Subby Nelson Mwakyusa, Ndugu Sara Katundu Sonelo, Ndugu Happy Hurbert Shao, Ndugu Ruth Fredrick Shao, Ndugu Mary Richard Mmbando, Ndugu Ruth Rodrick Mwambene na Ndugu Flora Yesaya. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunao pia wageni tisa wa Mheshimiwa Dotto Biteko ambaye ni Waziri wa Madini; katika hawa yupo Ndugu Adolf Ndunguru ambaye ni Katibu Mkuu, ndugu Msafiri Mbibo ambaye Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Abdulrahman S. Mwanga ambaye ni Kamishna wa Madini, *Professor* Idris Kikula ambaye ni Mwenyekiti wa Tume ya Madini. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo Meja Jenerali Mstaafu Michael Isamuyo, Mwenyekiti wa Bodi ya *STAMICO, Professor* Justinian Ikungura ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya *GST,* Dkt. George Mofulu ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya *TGC,* Nugu Janet Lekashingo ambaye anatoka Tume ya Madini karibu sana na *Professor* Abdulkarim Mruma ambaye ni Kamishna Tume ya Madini. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Dotto Biteko ambao ni wadau mbalimbali wa Wizara hiyo. Kwa hiyo, popote walipo wanaweza kusimama; wageni wa Mheshimiwa Dotto Biteko wengine, karibuni sana Dodoma wadau wa madini. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini kutoka Mkoa wa Manyara wakiongozwa na Meneja Manyara Ranchi, Ndugu Fidelis Ole Kashe, karibu Sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge; kwanza ni wageni wawili wa Mheshimiwa Prof. Adolf Mkenda, Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, ambao ni rafiki zake kutoka Dar es Salaam ambao ni Ndugu Santos Msimbe, Country Mnager Simba Net; na Ndugu Alice Mashiku ambaye ni *Sales Manager* wa *Airtel*. Karibuni Sana. *(Makofi)*

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, ambao ni Viongozi wa Jumuiya ya Qadiriya Jailaniya kutoka Mkoa wa Arusha wakiongozwa na Ndugu Yahaya Mkindi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni kumi wa Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga ambao ni Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Jimbo la Kilolo Mkoa wa Iringa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye Mgeni wa Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, ambaye ni Mtoto wake kutoka nchini Uingereza, Ndugu Omar Daudi Khamis. Karibu Sana. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Chistina Mnzava, ambaye ni rafiki yake kutoka Kahama Mkoa wa Shinyanga, Ndugu Joseph Frank Lubega. Karibu Sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimboni Manonga, Tabora wakiongwa na Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufaa, Nkinga, Ndugu Victor Ntundwe. Karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Dkt. Tito Chaula ambaye ni Mganga Mkuu wa Hospitali ya Nkinga; yupo pia Mjumbe wa Bodi Hospitali ya Rufaa Nkinga, Mzee Constantine Kaswalala; yupo pia Ndugu Fadhili Mashauri Kambangwa ambaye ni mfanyabiashara hapa Dodoma. Karibu Sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 32 wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambao ni wanamichezo kutoka Ruaha *Academy* ya Mkoani Iringa. Karibuni Sana. *(Makofi)*

Eh, Mheshimiwa Gulamali, mbona kama umevaa jezi za Simba! Shsante sana, karibuni sana Bungeni.

Tunao Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wageni 120 ambao ni Shirika la Mzalendo *Global Fund (MGF),* Shirika lisilo la Kiserikali linafanya utekelezaji wa miradi ya kutokomeza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto pamoja na kutoa elimu na uhamasishaji jamii, kujiandaa kikamilifu kushiriki sensa ya watu na makazi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wanafunzi 90 na walimu watano kutoka *Eugles High School* ya Bagamoyo Mkoani Pwani wakiongowa na Mwalimu Obadia Mwampapa. Karibuni sana Watoto wetu na walimu. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 30 kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe Mbeya *Campus* wakiongozwa na Ndugu Songelaeli Mkumbo. Karibuni sana wageni wetu Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo la wageni, tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu. Katibu.

**NDG. NEENA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

## MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MADINI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Waziri wa Madini Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko aje awasilishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini iliyochambua bajeti ya Wizara ya Madini, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Wizara ya Madini na Taasisi zake kwa Mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, kabla sijasema mengi, naomba hotuba yangu yenye kurasa 117 iingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ilivyoyowasilishwa kwenye Ofisi ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa

kunijalia afya njema na kunipa nafasi ya upendeleo ya kusimama kwa mara nyingine tena mbele yako na Bunge lako Tukufu kuwasilisha Mpango wa Mapato na Matumizi ya Mwaka 2022/2023. Kwa dhati kabisa naomba nitumie fursa hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuniamini kusimamia Sekta ya Madini. Naomba nimhakikishie kuwa nafasi aliyonipa nitaendelea kuitumikia kwa uaminifu na kwa uwezo nitakaojaliwa na Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba niseme, chini ya uongozi Mheshimiwa Rais wetu, tumeshuhudia uthubutu, ujasiri, uchapakazi na ubunifu wake mkubwa ambao umekuwa chachu ya mafanikio mengi ya kijamii katika kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa vituo vya afya na madarasa, uendelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati ikiwemo ujenzi wa reli na bwawa la kuzalisha umeme na miradi mingine mingi.

Mheshimiwa Spika, namshukuru tena Mheshimiwa Rais kwa hatua alizochukua kwa ajili ya kuzilinda rasilimali madini na kuvutia uwekezaji katika nchi yetu ambapo baada ya kipindi kirefu, Serikali imetoa leseni mbili kubwa za uchimbaji mkubwa wa madini na kuingia makubaliano na kampuni nne kwa lengo la kuongeza ushiriki wa Serikali katika shughuli za madini. Kupitia utendaji wake uliotukuka katika kipindi kifupi ambacho yupo madarakani, Watanzania wana imani kubwa kuwa Mheshimiwa Rais ataendelea kufanya mengi mema na mazuri kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, namshukuru kwa dhati Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, kwa miongozo yake mbalimbali yenye lengo la kuhakikisha kuwa rasilimali madini zinawanufaisha Watanzania kwa ujumla. Vilevile, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa uongozi wake makini na maelekezo anayoyatoa ili kufanikisha utendaji Serikalini, ikiwemo Wizara ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Natumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mbunge kwa kuchaguliwa pia kwa kishindo kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali, Mbunge; Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge pamoja na Wajumbe wote wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kushirikiana na Wizara yetu kwa kutupa maelekezo na kutusimamia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani na pongezi kwa Bunge lako Tukufu kwa kazi nzuri ambazo limekuwa likifanya katika kuisimamia na kuishauri Serikali, ikiwemo Wizara yetu ya Madini. Aidha, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuongoza Wizara mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa, nitumie fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Bukombe kwa kuendelea kunivumilia na kunipa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu kama Mbunge. Nawaahidi kuendelea kuwa mtumishi wao mwaminifu katika kutekeleza shughuli za maendeleo ya Jimbo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze vilevile Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Mbunge; Katibu Mkuu, Bw. Adolf Ndunguru; Naibu Katibu Mkuu, Bw. Msafiri Lameck Mbibo; Kamishna wa Madini, Dkt. Abdulrahman Shabani Mwanga kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuisimamia Sekta ya Madini. Aidha, nawashukuru viongozi wenzangu wote, Wenyeviti wa Bodi, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Madini pamoja na

wafanyakazi wote kwa ushirikiano na utendaji mzuri wanaofanya kwa ajili ya kulihudumia Taifa kupitia Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kumshukuru kwa dhati mke wangu mpenzi, Benadetha Clement Mathayo kwa maombi na upendo wake wa dhati pamoja na watoto wetu. Aidha, nawashukuru sana familia yangu yote kwa ujumla kwa ushirikiano na *support* wanayoendelea kunipatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, niungane na wenzangu kwa kutoa pole kwa wananchi wa Majimbo ya Ushetu, Ngorongoro, Konde kwa kuondokewa na waliokuwa Wabunge wao; Mheshimiwa Elias John Kwandikwa, William Ole Nasha na Khatib Said Haji, ambao walitangulia mbele ya haki. Nitoe pole kwako kwa kufuatia kifo cha Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Rukwa (CCM) kilichotokea tarehe 24 Aprili, mwaka huu. Vilevile, naomba kutoa pole ya dhati kwa wananchi wote kwa ujumla ambao walipoteza ndugu na mali zao kutokana na sababu mbalimbali. Mwenyezi azilaze roho za Marehemu wote mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nijielekeze katika maeneo mahsusi ya hotuba hii ambayo ni Mwenendo wa Biashara ya Madini Duniani; Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022; na Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, Mwenendo wa Biashara ya Madini Nchini: Uchumi wa madini nchini kwa kiasi kikubwa unatokana na madini ya dhahabu, ambayo huchangia takribani asilimia 80 ya mapato yote katika rasilimali madini. Wachambuzi wa masuala ya uchumi duniani walitarajia bei ya dhahabu kuendelea kuwa tulivu kwa mwaka 2022. Hata hivyo, bei ya madini ya dhahabu kwa wakia imepanda kutoka wastani wa Dola 1,412 Julai, 2019 hadi kufikia Dola 1,947.83 Machi, 2023.

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa bei ya dhahabu kunatokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na uwepo wa UVIKO-19. Changamoto ya vita kati ya Urusi na Ukraine inaweza kusababisha mahitaji makubwa ya madini ya dhahabu. Hii ni kwa sababu watu na taasisi duniani hupendelea kuhifadhi thamani ya fedha zao katika madini ya dhahabu kwa kuwa ni amana iliyo salama zaidi hasa nyakati wa mtikisiko wa kiuchumi. Aidha, ukuaji wa teknolojia umesababisha ongezeko la mahitaji ya madini ya *palladium, nickel, aluminium, cobalt*, *graphite, h*ivyo, bei ya madini hayo inatarajiwa kupanda na kuongeza fursa za uwekezaji hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2021 bei ya madini ya almasi katika soko la dunia iliongezeka na kufikia wastani wa Dola 241 kwa karati ikilinganishwa na wastani wa Dola 150 kwa karati mwaka 2020. Hadi Februari, 2022, bei ya almasi iliendelea kuongezeka na kufikia Dola 369 kwa karati. Ongezeko hilo lilitokana na kupungua kwa mlipuko wa UVIKO-19 na uhitaji mkubwa wa bidhaa za usonara zinazotokana na mahitaji ya almasi katika vipindi vilevile vya Sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya madini hayo huitajika zaidi. Hata hivyo, kuna viashiria vya bei ya madini ya almasi mwaka 2022 kubadilika kwa kupanda au kushuka kutokana na nchi ya Urusi ambayo ni mzalishaji mkubwa wa almasi duniani kuwa katika vita.

Mheshimiwa Spika, ili kunufaika na ongezeko la bei ya madini, Wizara inakusudia kuchukua hatua mbalimbali, ikiwemo kuweka mazingira rafiki kwa uwekezaji, kuangalia uwezekano wa kupunguzwa kwa baadhi ya kodi na tozo kwa wachimbaji, kuwaongezea wigo wa faida na kuchochea uzalishaji zaidi.

Aidha, Wizara inakusudia kuhimiza uwekezaji katika madini ya kimkakati ikiwemo *palladium, nickel, aluminium, cobalt*, *graphite* ili kunufaika na ongezeko la mahitaji ya madini hayo duniani. Vilevile, Wizara inaendelea kuhimiza uongezaji wa thamani madini nchini ikiwa ni pamoja na kuzalisha bidhaa zinazotokana na madini hayo.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wizara ilitengewa shilingi bilioni 66.8 kwa ajili ya matumizi ya Wizara pamoja na taasisi zake. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 15.0 zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 51.8 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo za matumizi ya kawaida shilingi bilioni18.5 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi bilioni 33.3 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2022, Wizara imepokea jumla ya shilingi bilioni 39 kutoka Wizara ya Fedha na Mipango. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni1.5 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 37.5 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa, shilingi bilioni 13.7 zimetumika kulipa mishahara ya watumishi na shilingi bilioni 23.8 ni matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ilipanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo: kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli; kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye pato la Taifa; kuwaendeleza wachimbaji wadogo; kuwawezesha wananchi kushiriki katika uchumi wa madini; kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani; kuhamasisha biashara na uwekezaji katika Sekta ya Madini; kusimamia mfumo wa ukaguzi wa shughuli za migodi; kuzijengea uwezo taasisi zilizo chini ya Wizara ya Madini ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi; na kuendeleza rasilimaliwatu na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza maduhuli ya Serikali na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye pato la Taifa, Wizara imeimarisha usimamizi na ukaguzi wa maeneo ya uchimbaji, mipaka ya nchi pamoja na kuanzisha na kuimarisha masoko na vituo vya uuzaji wa madini nchini. Tangu kuanzishwa kwake hadi kufikia Machi, 2022 jumla ya masoko 42 na vituo vya ununuzi wa madini 75 vimeanzishwa. Uanzishwaji na uimarishaji huo umechangia kwa kiasi kikubwa kwenye ukusanyaji wa maduhuli.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine ni kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli yalizochukuliwa ni pamoja na kuimarisha udhibiti wa biashara haramu na utoroshaji wa madini. Kazi hii hufanywa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali zikiwemo Mamlaka za Viwanja vya Ndege Tanzania, Mamlaka ya Mapato Nchini, Ofisi ya Usalama wa Taifa, Jeshi la Polisi, Idara ya Uhamiaji, Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya pamoja na raia wema wanaotoa taarifa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, madini ya aina mbalimbali yakiwemo dhahabu, vito, mchanga na madini ya viwandani yenye jumla ya thamani ya Shilingi milioni 500.1 yalikamatwa katika matukio ya utoroshaji ya biashara haramu ya madini katika Mikoa ya Mbeya, Morogoro, Manyara, Dodoma, Lindi, Geita, na Dar es Salaam pamoja na Mwanza. Kutokana na juhudi hizo, kumekuwa na ongezeko la ukusanyaji wa maduhuli ambapo katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 shilingi bilioni 461.6 zimekusanywa na kuwasilishwa kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina ikilinganishwa na shilingi bilioni 445.2 zilizokusanywa katika hicho cha mwaka 2020/2021. Ongezeko hilo ni sawa na 4%.

Mheshimiwa Spika, mchango wa Sekta ya Madini kwenye pato la Taifa umeendelea kuimarika. Katika kipindi cha Januari hadi Septemba, 2021 mchango wa sekta uliongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 7.9 kutoka wastani wa asilimia 6.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Katika robo mwaka ya Julai hadi Septemba, 2021 mchango wa sekta ya madini uliongezeka hadi kufikia asilimia 7.9 ikilinganishwa na mchango wa asilimia 7.3 katika kipindi hicho mwaka 2020. Mwenendo huu wa kukua kwa mchango huu unatoa mwelekeo chanya wa ukuaji wa sekta ambapo bila shaka ikifika mwaka 2025 mchango wa sekta ya madini utafikia asilimia 10.

Mheshimiwa Spika, mchango wa Sekta ya Madini katika kuingizia fedha za kigeni umekuwa ukiimarika vilevile. Mwaka 2021, sekta hii ilichangia asilimia 45.9 ya thamani zote

za bidhaa zilizouzwa nje ya nchi na kuliingizia Taifa Dola za Marekani milioni 3,103.20. Katika kipindi cha takribani miaka mitano mfululizo iliyopita Sekta ya Madini imeendelea kuongoza katika kuliingizia Taifa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mapato yaliyotokana na maduhuli na fedha za kigeni kupitia mauzo ya madini nje ya nchi, Sekta ya Madini pia iliiwezesha Serikali kukusanya Shilingi trilioni 1.58 kutokana na vyanzo mbalimbali vya kodi mwaka 2021 ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.34 mwaka 2020. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 17.9.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhamasisha wawekezaji katika Sekta ya Madini ili kuongeza mchango wa sekta katika pato la Taifa. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, kupitia Tume ya Madini, Serikali imetoa leseni mbili za uchimbaji mkubwa katika madini ya dhahabu ya ubia kati ya ubia wa *Sotta Mining Corporation* inayomilikiwa na Kampuni ya *Nyanzaga Mining Limited* na Serikali imetoa leseni kwa *Tembo Nickel* inayomilikiwa kwa ubia kati ya Kampuni Kabanga *Nickel* na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Serikali katika miradi yote hiyo miwili inamiliki hisa zilizoshuka zenye thamani ya asilimia 16.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha mazungumzo na kampuni ya uchimbaji wa madini ya almasi ya *Williamson Diamond* ambapo hisa za Serikali zimeongezeka kutoka asilimia 25 hadi 37. Aidha, Serikali imesaini mikataba na kampuni za uchimbaji wa madini ya Kinywe, kampuni ya *Black Rock Mining Limited* na Kampuni ya *Heavy Mineral Sands*, Kampuni ya *Strandline Resources* na kuunda Kampuni za ubia za *Faru Graphite Corporation*, *Nyati Mineral Sands* mtawalia. Serikali pia katika kampuni hizo ina ubia wa hisa asilimia 16.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji katika miradi hii unatarajia kuleta Dola za Marekani, milioni 1,672.57. Uwekezaji huu ni mkubwa kuwahi kutokea katika kipindi cha takribani miongo miwili iliyopita. Aidha, uwekezaji huu utaongeza ajira na manufaa yatokanayo na uwajibikaji wa kampuni kwa

jamii, ushiriki wa Watanzania katika uuzaji wa bidhaa na utoaji huduma katika shughuli mbalimbali kwenye sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kuwaendeleza wachimbaji wadogo na kuwawezesha wananchi kushiriki katika uchumi wa madini, Wizara imeendelea kuzisimamia taasisi za fedha na benki kutoa mikopo kwa wachimbaji hao. Miongoni mwa Benki ambazo zimeshatoa mikopo kwa wachimbaji ni pamoja na benki ya *NMB, NBC, CRDB* na *KCB.* Hadi sasa baadhi ya benki zimeridhia na kuanza kutoa mikopo ambapo jumla ya Shilingi bilioni 36 zimekopeshwa kwa wachimbaji wadogo. Aidha, Wizara inaendelea na jitihada za kuhamasisha taasisi hizo kuona uwezekano wa kuendelea kuwakopesha vifaa wachimbaji wetu.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine ya uendelezaji wachimbaji wadogo zilizochukuliwa ni pamoja na kuwapa elimu na kuwagawia nakala zipatazo 1,000 za Miongozo ya wachimbaji wadogo, kutoa mafunzo na huduma mbalimbali kwa wachimbaji wadogo wapatao 1,144 waliotembelea vituo vya mfano vya Katente, Lwamgasa, Itumbi, vikundi vitano vya wachimbaji wadogo kutoka Singida, Kilindi, Morogoro vimewezeshwa kujua jiolojia ya maeneo wanayomiliki. Aidha, Shirika la Madini la Taifa limekamilisha ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhia vilipuzi, kemikali katika vituo vya Lwamgasa.

Mheshimiwa Spika, *STAMICO* na Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania walifanya mafunzo mbalimbali kwa wachimbaji wadogo wapatao 945, wakiwemo wenye usikivu hafifu. Mafunzo hayo yalihusisha, uchimbaji salama, biashara ya madini na uchukuaji bora wa sampuli katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa shughuli za uchimbaji mdogo zinaendelea kufanyika kwa ufanisi, Serikali imeendelea kuwarasimisha wachimbaji wadogo. Hadi kufikia Machi 2022, Wizara kupitia Tume ya Madini imetoa leseni 5,937 za uchimbaji mdogo wa madini, sawa na asilimia 72.65 ya leseni zote zilitolewa ikilinganishwa na leseni 3,540

zilizotolewa katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Aidha, kufuatia kurasimishwa na kutambuliwa kwa wachimbaji wadogo, mchango wao sasa umeongezeka kutoka asilimia nne hadi asilimia 30 kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, kuanzia Julai, 2021 hadi 2022 jumla ya tani 4,235 za mbale ya dhahabu zilichenjuliwa katika vituo vya Lwamgasa, Katente, Itumbi, ambapo jumla ya wakii 3,692.77 za dhahabu zilizalishwa zikiwa na thamani ya shilingi bilioni 12.32 na kulipa tozo za Serikali milioni 696.6.

Mheshimiwa Spika, katika kuhamasisha na kuhakikisha shughuli za uongezaji madini nchini zinaimarika, Serikali imeendelea kukiimarisha Kituo cha Jemolojia Tanzania kwa kuongeza fedha katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 kwa ajili ya kuboresha miundombinu na kununua vifaa vya kujifunzia. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa vijana wengi wanapata kazi, ujuzi katika nyanja hizo na kuwaongezea fursa za kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, kupitia *STAMICO* Serikali imejenga na kusimika miundombinu na mtambo wa kuzalisha makaa ya mawe kwa ajili ya matumizi ya nyumbani katika eneo la *TIRDO,* Dar es Salaam, katika uzalishaji wa majaribio ulifanyika kwa ufanisi. Aidha, Shirika limeagiza mitambo miwili yenye uwezo wa kuzalisha tani 20 za *coal briquettes* kwa saa ili kuongeza uzalishaji. Mradi huo utawanufaisha watanzania kwa kutoa ajira zaidi ya 200 na kupunguza ukataji wa miti kwa ajili ya mkaa na hivyo kuchangia kutunza mazingira.

Mheshimiwa Spika, viwanda mbalimbali vinaendelea kutumia madini ya viwanda kama malighafi kwa ajili ya kuzalisha bidhaa mbalimbali. Kuanzia Julai, 2021 hadi Machi, 2022 kiasi cha madini ya viwandani kilichozalishwa na kutumiwa na viwanda hivyo kilikuwa tani milioni 7.6. Uzalishaji na utumiaji wa madini haya ni kwa muhimu kwa ajili ya kukuza na kuendeleza viwanda nchini.

Mheshimiwa Spika, biashara ya madini nchini imeendelea kuimarika ambapo katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 jumla ya kilogramu 39,682.94 za dhahabu,

kilogramu 7,102.96 za fedha, karati 155,117.10 za almasi, kilogramu 15,377.44 za Tanzanite ghafi, kilogramu 130,582.28 za Tanzanite za ubora wa chini, karati 81,305.42 za tanzanite iliyokatwa na kusanifiwa, tani 19,355.13 za madini ya shaba na tani 322.49 za madini ya bati zilizalishwa nchini. Vilevile, kilogramu 6,835,746 za karati, 12,863.2 za madini mengine ya vito ghafi vilikatwa na kusanifiwa hapa nchini. Tani 18,462,591 za madini ya ujenzi, tani 956,688 za makaa ya mawe, tani 7,843,634.41 za madini mengine ya viwandani na tani 51,132.33 za madini mengine ya metali zilizalishwa na kuuzwa. Katika kipindi hicho na jumla ya shilingi bilioni 429 zilikusanywa kama malipo ya mrabaha na ada ya ukaguzi kwenye maeneo yote hayo.

Mheshimiwa Spika, shughuli za uchimbaji na uchenjuaji wa madini huambatana na athari mbalimbali za afya na mazingira. Ili kuhakikisha kwamba shughuli za madini zinakuwa na tija na athari zake zinadhibitiwa, kaguzi mbalimbali zimefanyika katika maeneo mbalimbali na kuweza kudhibiti athari ambazo zingeweza kufanyika. Kutokana na kaguzi zilizofanyika, migodi mingi inaonekana kuwa inazingatia taratibu za uendeshaji migodi kwa mujibu wa Sheria. Hata hivyo, katika baadhi ya migodi, kaguzi zimebaini kuwepo kwa hali ya kutozingatiwa kwa taratibu za uendeshaji wa migodi. Kutokana na mapungufu hayo yaliyobainika baadhi ya migodi kupitia Tume ya Madini imechukua hatua kadhaa zenye lengo la kuhakikisha kuwa kasoro zilizobainika zinarekebishwa. Hatua hizo ni pamoja na kutoa maelekezo mahsusi kwa wamiliki wa migodi na kuchukua hatua ya kuondoa upungufu uliobainika kwenye kaguzi hizo.

Mheshimiwa Spika, katika kuzijengea Taasisi uwezo, Wizara imewezesha ununuzi wa vitendea kazi kwa ajili ya Maabara pamoja na kuanza ujenzi wa jengo la kuhifadhia sampuli za miamba lililopo Kizota Dodoma kwa ajili ya Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania. Aidha, ili kuimarisha usimamizi, ufuatiliaji na ukusanyaji wa maduhuli, Tume ya Madini imewezeshwa kupata fedha za kununua magari 40 ambapo hadi sasa magari saba yamepokelewa. Vilevile,

*STAMICO* iliwezeshwa kupata vifaa vya utafutaji na uchimbaji wa madini ambavyo ni *excavator, drill rig, crane, survey equipment* ili kuimarisha shughuli hizo.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuboresha mazingira ya kazi ikiwa ni pamoja na ujenzi wa majengo matatu ya Ofisi. Majengo hayo pamoja na Ofisi ya Makao Makuu katika Mji wa Serikali Mtumba, Ofisi ya Makao Makuu ya Tume ya Madini eneo la Kilimani Dodoma na Ofisi ya Afisa Madini Mkazi Geita. Aidha, vitendea kazi mbalimbali vimenunuliwa yakiwemo magari, kompyuta kwa ajili ya kuwawezesha watumishi kufanya kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 Fedha za Maendeleo zilizopokelewa ni bilioni 7.4, ambapo shilingi bilioni 1.5 kutoka kwenye bajeti ya maendeleo mwaka wa fedha unaoendelea na shilingi bilioni 5.9 ni kutoka katika Akaunti Amana. Miradi iliyotekelezwa ni pamoja na ukamilishaji wa ujenzi wa vituo vya umahiri vya Songea, Mpanda, Chunya, ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Wizara awamu ya pili katika Mji wa Serikali Mtumba, ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Tume ya Madini eneo la Kilimani Dodoma, kuanza hatua za awali za ujenzi wa jengo la Ofisi ya Afisa Madini Geita na ununuzi wa vifaa vya Maabara, vitendea kazi kwa ajili ya Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa wananchi katika ushiriki wa shughuli za uzalishaji na kufungamanisha Sekta ya Madini na sekta nyinginezo ili kuendelea kukuza uchumi wa Taifa kwa ujumla. Kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022, Wizara kupitia Tume ya Madini imepokea na kuchambua jumla ya mipango 378 kwa ajili ya ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini kutoka kwa wamiliki wa leseni na watoa huduma migodini, ambapo mipango 366 kati ya hiyo ilikidhi vigezo na kuidhinishwa. Mipango 12 iliyobaki haikukidhi vigezo na wahusika walielekezwa kuifanyia maboresho kwa mujibu wa Sheria ya Madini Sura 123.

Mheshimiwa Spika, katika ya kampuni 378 yaliwasilisha na kuidhinisha mipango ya ushirikishwaji wananchi, kampuni 10 za uchimbaji mkubwa, kampuni 14 za uchimbaji wa kati, kampuni nne za uchimbaji mdogo, saba za uchimbaji wa madini, tatu leseni ya usafishaji na kampuni 340 za watoa huduma migodini.

Mheshimiwa Spika, ushiriki wa watanzania katika shughuli ya madini umeendelea kuimarika na kuongezeka. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 idadi ya watanzania walioajiriwa katika kampuni za utafutaji wa madini na kutoa huduma imefikia 14,308 ikilinganishwa na 7,151 katika kipindi kama hicho Mwaka 2020/2021. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 100. Aidha, katika kipindi rejewa trilioni 5.2 zimetumiwa na migodi kulipa na kununua bidhaa mbalimbali zilizotolewa katika migodi hiyo ikilinganishwa na shilingi trilioni 2.4 zilizotumika katika kipindi kama hicho Mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kufuatilia na kusimamia wajibu wa kampuni kwa jamii zinazozunguka migodi. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 migodi 13 ilitoa jumla ya shilingi bilioni 16 kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya elimu, maji, barabara na katika Halmashauri za Wilaya mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika Uboreshaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo katika Sekta ya Madini. Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa wawekezaji katika Sekta ya Madini wanafanya kazi zao katika mazingira rafiki ya kisheria yenye tija kwa pande zote mbili, yaani Serikali na Wawekezaji. Katika kutekeleza hilo, maboresho mbalimbali katika Sheria, na Kanuni zinazosimamia Sekta ya Madini yamefanyika. Miongoni mwa maboresho hayo ni pamoja na marekebisho katika Kanuni za Madini ikiwemo eneo Tengefu la Mirerani. Katika marekebisho mengine yaliyofanyika katika Kanuni za Haki Madini za Mwaka 2018 ambayo imemuwezesha Waziri wa Madini kuondoa masharti ya kanuni zinazohusu haki madini kwa waombaji wa leseni ya Uchimbaji wa Kati na Leseni za Uchimbaji Mkubwa ambapo watakuwa na

makubaliano maalum ya Serikali ambayo kwa Serikali itakuwa ni mwanahisa au itakuwa wanahisa. Na Marekebisho hayo yamefanyika kupitia Tangazo la Serikali Na. 593 la tarehe 9 Julai, 2021.

Mheshimiwa Spika, katika kusimamia Baruti. Baruti ni muhimu katika shughuli za uchimbaji wa madini na hutumika kulipua miamba migumu wakati wa uchimbaji wa madini. Pamoja na umuhimu wake katika shughuli za madini, baruti ina madhara makubwa kama haitasimamiwa vizuri. Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 kuanzia Julai, 2021 hadi Machi, 2022 vibali vilitolewa katika kampuni za wafanyabiashara mbalimbali vilikuwa vibali 225 vya kuingiza baruti na vibali 21 vya kufanya biashara ya baruti, vibali 21 vingine kwa ajili ya kusafirisha baruti kwenda nje ya nchi na vibali 37 kwa ajili ya kupitisha baruti kwenda nchi nyingine kama *transit*. Aidha, vibali saba vya kutengeneza baruti vimetolewa kwa kampuni tatu ambazo zimepata leseni hizo.

Mheshimiwa Spika, leseni tatu za viwanda vya kutengeneza baruti zimetolewa kwa kampuni mbili ambazo ni Mbogo *Mining and General Supply Limited* na kampuni ya *Solar Nitrochemicals Limited*. Aidha, leseni sita za kutengeneza baruti kwa kutumia magari maalum zilitolewa kwa makampuni mawili. Leseni 18 za maghala ya kuhifadhia baruti zilitolewa kwa kampuni na wafanyabiashara wa baruti. Vibali vya leseni za baruti vilitolewa zimeipatia Serikali jumla ya shilingi milioni 453.5. Kutolewa kwa leseni za viwanda vya kuzalisha baruti nchini ni hatua muhimu katika kukuza viwanda hapa nchini kuongeza uzalishaji wa bidhaa hiyo hapa nchini na kuhakikisha upatikanaji wake na kupatikana kwa kodi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na madhara yanayoweza kusababishwa na matumizi yasiyokuwa sahihi ya baruti, kaguzi mbalimbali zilifanyika katika utengenezaji na utunzaji na uhifadhi wa baruti kwenye makampuni matatu. Katika kaguzi nyingine baruti zilizofanyika kwenye ujenzi wa maghala ya kuhifadhia baruti kwa kampuni za *Zem Development* ya mkoani Shinyanga na Ilolo *Investment*

mkoani Lindi. Leseni hizo zilizotolewa zilibainika kuwa ujenzi wa kutengeneza baruti ya kampuni ya *Tan Nobel Nickle* katika Kijiji cha Makombe Bagamoyo, kibali kilitolewa kwa kampuni hiyo baada ya kuwa imekidhi matakwa ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, kaguzi tatu zilizofanyika kwenye maeneo ya ujenzi wa maghala ya kuhifadhia baruti katika vijiji vya Kinzagu, Makombe, Wilaya ya Bagamoyo na kijiji cha Makanga Vigoli, Wilaya ya Ulanga. Kupitia kaguzi hizo vibali vya ujenzi wa maghala ya kuhifadhia baruti vilitolewa na wahusika na baada ya kujiridhisha kuwa katika maeneo yaliyopendekezwa yanafaa kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, sasa nieleze kuhusiana na shughuli zilizotekelezwa kwenye Taasisi za Wizara. Wizara inazo Taasisi tano ambayo ni Tume ya Madini, Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania, Shirika la Madini la Taifa, Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia na Kituo cha Jemolojia Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2021/ 2022 pamoja na kutekeleza majukumu yake Tume ya Madini ina wajibu wa kukusanya maduhuli kama ilivyoanishwa hapo awali. Tume ya Madini imetekeleza majukumu yafuatayo; utoaji wa leseni na usimamizi wa masoko ya madini. Vilevile katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 thamani ya biashara ya madini katika masoko ya madini imeongezeka na kufikia takribani trioni 1.782 kutokana na biashara hiyo Serikali imekusanya mrabaha kwenye masoko hayo na ada ya ukaguzi ya takribani bilioni 123.58 ikilinganishwa na bilioni 109.23 katika kipindi kama hicho Mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 13.4. Shughuli nyingine ya Tume ya Madini ni utambuzi na uthaminishaji wa madini yanayosafirishwa nje ya nchi, ukaguzi wa hesabu za kodi mbalimbali kwenye Makampuni mbalimbali. Na katika hili baada ya kukamilika kwa kaguzi Kampuni tano za ujenzi wa barabara ilibainika kuwepo kwa malipo pungufu ya maduhuli mbalimbali ya Serikali kiasi cha shilingi bilioni 2.21. Kampuni hizo zimekubali kulipa maduhuli hayo ya awali ambayo yalikuwa hayajalipwa.

Mheshimiwa Spika, shughuli nyingine inayofanywa na Tume ya Madini ni utoaji wa huduma za Maabara, ambapo Tume ya Madini kupitia Maabara yake ya Dar es Salaam imefanya uchunguzi wa sampuli 1,398 za mikuo ya dhahabu 45 na sampuli 851 za madini ya shaba kutoka katika migodi mikubwa hapa nchini. Uchunguzi huo ulilenga kupata kiasi halisi na thamani ya madini kwa ajili ya kuhakiki tozo na kiasi cha fedha kitakachokusanywa. Shughuli nyingine ya Tume ya Madini ni uendelezaji na usimamizi wa Mifumo ya TEHAMA, ambapo Tume ya Madini imeendelea kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na madini ya ujenzi ya viwanda kwa kutumia mashine za *Point of Sale (PoS).* Utaratibu huu utatumia *PoS* unaonyesha matokeo chanya katika ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali. Takwimu zinaonesha kuwa, kabla ya matumizi ya *PoS* wastani wa makusanyo kwa kipindi cha Oktoba, 2020 hadi Februari, 2021 makusanyo yaliyotokana na madini ya ujenzi yalikuwa shilingi bilioni 5.85 ikilinganishwa na shilingi bilioni 6.49 baada ya matumizi ya *PoS* kwa kipindi kama hicho Mwaka 2021/2022 ikiwa ni ongezeko la asilimia 9.3. Kutokana na mafanikio hayo, Tume ya Madini imeendelea kuimarisha matumizi ya mashine za *PoS* katika vyanzo vyote vya uzalishaji wa madini ya ujenzi kwa kutumia mashine za *PoS*.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Madini la Taifa. *STAMICO* imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kutafuta, kuchimba, kuchenjua, kusafisha na uuzaji wa madini pamoja na kutoa huduma mbalimbali kwenye Sekta ya Madini, ikiwemo uchorongaji na utoaji wa ushauri wa kitaalam. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 *STAMICO* imetekeleza shughuliz zifuatazo;

Kwanza, kuanzisha na kuendeleza miradi ya makaa ya mawe, shirika limetekeleza miradi mitatu kupitia vyanzo vyake vya mapato mbalimbali, Mradi wa makaa ya mawe Kaburo Kiwira, Mradi wa makaa ya kupikia *Coal briquettes* na Mradi wa kuuza kemikali na vilipuzi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2021 katika mradi wa Kabulo, tani 17,324 za makaa ya mawe zilichimbwa

ambapo tani 12,792 zenye thamani ya shilingi bilioni 1.06 ziliuzwa na kulipa Serikali shilingi milioni 174.19, ikiwa ni mrabaha na ada ya ukaguzi. Aidha, shirika limeingia makubaliano ya awali na *TANESCO* ya kuendeleza mradi wa Kiwira ambapo shirika litakuwa na jukumu la kuchimba makaa ya mawe na *TANESCO* kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza changamoto ya uharibifu wa mazingira, shirika limeanza kuzalisha mkaa wa kupikia kama nilivyoeleza. Shirika vilevile limeanzisha kuuza kemikali za baruti na vilipuzi kwa wachimbaji wadogo. Mradi huu utatekelezwa katika vituo vya mfano vya Lwamgasa, Katente, Itumbi na mgodi wa *STAMIGOLD*. Aidha, shirika linategemea kuanza kuuza kemikali na vilipuzi katika migodi mingine ya kati na mikubwa nchini ili kuongeza wigo wa wateja wake na kusogeza huduma hiyo karibu na wachimbaji. Shirika limeanza hatua za ununuzi wa baruti, vilipuzi na kemikali ili kuwawezesha wachimbaji wadogo kupata zana hizo karibu na maeneo yao na kwa bei nafuu. Hadi Machi, 50 2022 shirika limepata mapato ya shilingi milioni 568.98 kutokana na mauzo ya vilipuzi.

Mheshimiwa Spika, huduma nyingine inayotolewa na shirika ni huduma za uchorongaji na ushauri wa kitaalam, ambapo hadi hadi Machi, 2022 *STAMICO* ina mitambo tisa ya uchorongaji. Na Shirika limenunua mitambo mingine mitano ya uchorongaji ambayo inatarajiwa kuwasili nchini kabla ya Juni, 2022 na kufanya shirika kuwa na mitambo 14. Ongezeko la mitambo hiyo litawezesha shirika kutekeleza kandarasi za uchorongaji kwa mfumo wa *RC* na *DD* kwa ufanisi. Vilevile, katika kipindi cha Mwaka 2021/2022 shirika limepata kandarasi kubwa tatu za uchorongaji zenye thamani ya shilingi bilioni 17.5. Mafanikio haya yanatokana na maboresho ya kimuundo pamoja na usimamizi wa Shirika unaofanywa na Serikali kupitia Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Spika, kampuni tanzu ya *STAMIGOLD* katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 mgodi umezalisha wakia 7,106 za dhahabu na wakia 1,059 za madini ya fedha zote zikiwa na thamani ya shilingi bilioni 29.84

kutokana na mauzo hayo ambapo Serikali imepata mrabaha wa bilioni 2.09.

Mheshimiwa Spika, katika mradi wa ubia unaotekelezwa wa kiwanda cha kiwanda cha kusafisha dhahabu Mwanza. Kiwanda cha Mwanza *Refinery* kina uwezo wa kusafisha dhahabu kwa kiwango asilimia 999.9 *purity*. Kiwanda hicho bado kinafanya kazi kwa kiwango cha chini ikilinganishwa na uwezo wake wa kuzalisha. Ili kukabiliana na changamoto zilizopo na kuongeza uzalishaji kiwanda kimetenga dola za Marekani milioni 150 ikiwa ni mtaji wa kununua malighafi ya dhahabu.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Dhahabu wa Buhemba. Mradi wa Buhemba ni wa ubia kati ya *STAMICO* inayomiliki kwa asilimia 35 na kampuni ya *GOODFIELD International DMCC* ya Dubai inayomiliki hisa asilimia 65 kupitia leseni ya madini ML 646/2021. Mgodi uliingia makubaliano ya kuchoronga awamu ya kwanza ya mita 4,000 kwa njia ya *RC* na mita 1,200 kwa *DD* yenye thamani ya shilingi bilioni 1.25 ili kuongeza kiasi cha mashapo. Aidha, Februari, 2022 shirika lilisaini makubaliano kwa ajili ya awamu ya pili ya uchorongaji wa mita 40,000 katika mgodi wa Buhemba yenye thamani ya shilingi bilioni 11.1. Mradi *Buckreef*, shirika limeingia ubia na mbia mwenza *TANZAM* 2000. Katika mradi huo shirika lina asilimia 45 na *TANZAM* 2000 ana asilimia 55. Thamani ya uwekezaji ya mradi huu ni dola za Marekani milioni 19.6. Mgodi huu umeanza uzalishaji mkubwa wa dhahabu kwa kutumia mtambo wenye uwezo wa kuchakata tani 15 za mbale kwa saa.

Mheshimiwa Spika, kuanzia Novemba, 2021 hadi 2022 *Buckreef* imezalisha kilo za dhahabu 60.98 zenye thamani ya Shilingi Bilioni 7.11 na kulipa mrabaha na tozo zingine kwa Serikalini Shilingi Milioni 497.9. Aidha, kwa sasa mtambo mkubwa wenye uwezo wa kuchakata tani 30 za mbale umefika nchini na usimikaji wake unaendelea. Usimikaji huo utakapokamilika mgodi utakuwa na uwezo wa kuchakata tani 45 za mbale kwa saa. Vilevile, shirika limeanza kutekeleza kandarasi ya uchorongaji yenye thamani ya Shilingi Bilioni 4.3.

Mheshimiwa Spika, mgodi pia umelipa fidia ya shilingi bilioni 5.6 ambayo ni sawa na asilimia 96 ya fidia yote kwa wananchi 960 walio katika eneo la mradi lenye ukubwa wa kilomita za mraba 9.4. Eneo hilo linahusisha vijiji vya Lwamgasa, Mnekezi na Lubanda. Aidha, Januari, 2021 mgodi uliingia makubaliano na Halmashauri ya Geita kwa kutekeleza mpango wa uwajibikaji kwa wananchi na ambapo mgodi umetoa fedha shilingi 321,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu hayo.

Mheshimiwa Spika, Taasisi nyingine ni Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania *(GST)*. Taasisi hii ilikusudia kufanya shughuli mbalimbali:

(i) Kufanya Tafiti za Jiosayansi na Kuboresha Kanzidata ya Taifa ya Taarifa za Miamba.

(ii) Kuboresha huduma za Maabara ambapo *GST* ina maabara ya kisasa ya madini ambayo inaendelea kuimarisha shughuli zake na imeshapata *ISO accreditation* katika uchunguzi wa sampuli za dhahabu kwa njia ya uyeyushaji kwa kutumia kemikali.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe rai kwa watafiti na wachimbaji wa madini ya dhahabu nchini na makaa ya mawe kutumia maabara ya *GST* ili kupata majibu yenye uhakika kwa ajili ya sampuli zao.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Jiolojia pia ina ratibu majanga ya asilia ya jiolojia na kuelimisha wanachi namna bora ya kupunguza athari za majanga hayo. Moja kazi ya majukumu haya ni kuratibu majanga ya asilia ya jiolojia kama vile matetemeko ya ardhi, milipuko ya volkano na maporomoko ya ardhi kwa lengo la kutoa ushauri wa namna bora ya kupunguza madhara hayo yanayoweza kuleta majanga kwa watu.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Jiolojia pia imeendelea kuimarisha uwezo wa taasisi kwa kusogeza huduma kwa wananchi. Katika kufika hatua hiyo au azma hiyo *GST*

imefungua ofisi ndogo katika Mkoa wa Geita. Aidha, *GST* imenunua mashine na vifaa mbalimbali kwa ajili ya maabara ili kuimarisha huduma zinazotolewa na uchunguzi wa sampuli.

Mheshimiwa Spika, mashine hizo ni pamoja na mashine za kuzalisha vyungu vya kuyeyushia sampuli za madini, tanuru la kisasa kwa ajili ya kuchunguza sampuli za dhahabu, mashine *XRD* kwa ajili ya kuchunguza sampuli.

Mheshimiwa Spika, *GST* vilevile ilifanya utafiti wa Ki-*geophysics* kwa Kampuni za Uchimbaji ya Madini wa Kati kama vile *MMG* uliopo Mkoani Mara, ambapo matokeo ulibaini uwepo wa mkondo unaobeba dhahabu. Pia, utafiti wa Geo-*physics* ulifanyika kwa wachimbaji wadogo wa eneo la Pemba Wilaya ya Mvomero na kubaini uwepo wa madini ya dhahabu.

Mheshimiwa Spika, taasisi nyingine ni Taasisi ya Uhamasishaji, Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia *(TEITI)*. Taasisi hii imekwisha kutoa taarifa zake ambazo zilikuwa nyuma kwa muda mrefu. Katika ripoti hiyo iliweka wazi taarifa mbalimba zikiwemo uzalishaji wa usafirishaji wa madini mafuta asilia na gesi, umiliki wa hisa na taarifa za usafirishaji wa Watanzania. Taarifa hiyo ilibaini kuwa sekta ya madini imechangia kwa asilimia 67.75 na sekta ya mafuta na gesi imechangia asilimia 28.43. Kampuni zinazotoa huduma kwenye sekta ya uziduaji asilimia 4.03; mapato ya Serikali kwenye kampuni 41 zilizofanyiwa ulinganishi. Aidha, taarifa iliainisha thamani ya madini yaliyozalisha mwaka 2018/2019 ilikuwa na thamani ya Shilingi Trilioni 4.7.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Jiolojia. Kuanzia Julai, 2021 kituo hiki kimedahili wanafunzi 95 kwa mfululizo kwa muda mrefu katika ngazi ya Stashahada katika fani ya Teknolojia ya Madini na Usonara. Aidha, wanafunzi 43 walidahiliwa na kujiunga na mafunzo ya muda mfupi katika ngazi ya Astashahada kwenye fani ya utambuzi wa madini.

Mpango wa Makadirio na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, katika kuandaa Mpango na Bajeti wa Mwaka 2022/2023, Wizara imezingatia miongozo mbalimbali ya Kitaifa, ukiwemo Mwongozo wa Kitaifa wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti, Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi wa Mwaka 2025, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026, Sera ya Madini ya Mwaka 2009, Dira ya Maendeleo 2025, Maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan na Viongozi wengine wa Kitaifa waliyoyatoa katika nyakati tofauti na Maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2022 Tume ya Madini itaendelea kutekeleza majukumu yake kama nilivyoeleza hapo juu. Taasisi ya Jiolojia Tanzania itaendelea nayo kutekeleza majukumu yake pamoja na Shirika la Madini la Taifa – *STAMICO*, *TEITI* pamoja na Kituo cha Jiomolojia.

Mheshimiwa Spika, shukrani. Kwa dhati kabisa napenda kukiri kuwa Awamu ya Sita imefanya juhudi kubwa katika kuhakikisha kuwa uchumi wa nchi yetu unaimarika. Ni imani yangu kuwa kasi kubwa ya utendaji kazi unaofanywa na anaoendelea kufanya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, nchi yetu itaendelea kupiga hatua kubwa katika kuimarisha ustawi wa kila Mtanzania na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kumshukuru tena Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa miongozo yake mizuri anayotupatia katika kusimamia sekta ya madini. Naomba nitumie fursa hii kumshukuru Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, kwa ajili ya miongozo wanayotupatia katika kusimamia sekta yetu ya madini.

Mheshimiwa Spika, kipekee nitumie fursa hii kumshukuru Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa Mbunge, kwa namna anavyonipa ushirikiano katika kusimamia Sekta ya Madini, amekuwa mstari

wa mbele katika kuhakikisha kuwa sekta ya madini inakuwa na tija kubwa. Katika kipindi kifupi toka ameteuliwa Mheshimiwa Kiruswa amekuwa mfuatiliaji wa karibu wa masuala mbalimbali kwenye sekta ya madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa ninamshukuru Katibu Mkuu Ndugu Adolf Ndunguru, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Msafiri Lameck Mbibo kwa namna wanavyosimamia vyema utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, niwashukuru Kamishna wa Madini, Dkt. Abdulrahman Shabani Mwanga, Mwenyekiti wa Tume ya Madini na Mtendaji wa Tume ya Madini Profesa Idris Suleiman Kikula na Injinia Yahaya Samamba Mwenyekiti wa Bodi ya *GST,* Mtendaji wa *GST* Profesa Justinian Rwezaula Ikingura pamoja na Dkt. Budeba Mwenyekiti wa Bodi ya *STAMICO*. Meja Jenerali (Mstaafu) Michael Wambura Isamuhyo pamoja na Mwenyekiti wa Bodi ya TGC, Dkt. George Mofulu, Makamishna wa Tume ya Madini na Wajumbe wa Bodi zote kwa kusimamia kwa umakini na weledi uendeshaji wa shughuli za Wizara.

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru pia wadau wa Sekta mbalimbali wakiwemo watafutaji, wachimbaji, wamiliki wa mitambo ya uchenjuaji wa madini, wafanyabiashara wa madini kwa kuendelea kutekeleza shughuli zao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za nchi yetu.

Aidha, ninazishukuru Taasisi za Serikali hususan mabenki kwa kuendelea kuwapa mikopo wachimbaji wetu, vyombo vya ulinzi na usalama kwa kutuhakikishia usalama kwenye maeneo yenye shughuli za madini bila kusahau vyombo vya habari ambapo kwa kweli kwa kiwango kikubwa wametupa ushirikiano mkubwa kuitangaza sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowashukuru tena wananchi wa Bukombe ambao wao ndiyo walionichagua na kunifanya kuwa mwakilishi wao. Nawashukuru sana na ninaomba niwape ahadi hii kama ambayo kwa muda wote tumekuwa tukiambiana tutaijenga Bukombe yetu kwa kushirikiana kwa pamoja.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake na malengo yaliyopangwa, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liridhie na kupitisha makadirio ya shilingi 83,445,260,000.00 kwa ajili ya matumizi ya Wizara na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kwa mchanganuo ufuatao: -

Shilingi 22,000,000,000.0) ikiwa ni fedha za maendeleo, na shilingi 61,445,260,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 20,609,600,000.00 ni kwa ajili ya Mishahara na shilingi 40,835,660,000.00 ikiwa ni matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Majedwali na viambatanisho vyote vya hotuba hii yameunganishwa na kuwekwa kwenye tovuti ya Wizara. Hotuba hii vilevile inapatika katika tovuti ya Wizara ya Madini kwa anuani ya www.madini.go.tz.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

## HOTUBA YA WAZIRI WA MADINI, MHESHIMIWA DKT. DOTO MASHAKA BITEKO (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### A. UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini iliyochambua bajeti ya Wizara ya Madini, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Wizara ya Madini na Taasisi zake kwa Mwaka 2022/2023.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee sana ninamshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, kwa kunijalia afya njema na kunipa nafasi ya upendeleo ya kusimama kwa mara nyingine tena mbele ya Bunge lako Tukufu nikiwa Waziri wa Madini kuwasilisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2022/2023.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa dhati kabisa naomba nitumie fursa hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kuniamini kuendelea kusimamia Sekta ya Madini. Namhakikishia kuwa nafasi aliyonipa nitaendelea kuitumikia kwa uaminifu na kwa uwezo alionijalia Mwenyezi Mungu ili kufikia matarajio ya Watanzania ya kuona Sekta ya Madini ikiboresha maisha yao na kuongeza mchango wake kwenye Pato la Taifa.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** chini ya uongozi makini wa Rais wetu tumeshuhudia uthubutu, ujasiri, uchapakazi na ubunifu wake mkubwa ambao umekuwa chachu ya mafanikio makubwa ya kijamii na kiuchumi kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali kama ujenzi wa vituo vya afya na madarasa, uendelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati ikiwemo ujenzi wa reli mpya ya *standard gauge* na mradi wa bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere (*JNHP*).

5. ***Mheshimiwa Spika***, ninamshukuru tena Mheshimiwa Rais, kwa hatua madhubuti anazoendelea kuchukua katika kuzilinda rasilimali madini na kuvutia uwekezaji katika shughuli za uchimbaji madini ambapo baada ya kipindi kirefu, Serikali imetoa leseni mbili (2) kwa kampuni za uchimbaji mkubwa na kuingia makubaliano na kampuni nne (4) kwa lengo la kuongeza ushiriki wake katika shughuli za madini. Kupitia utendaji wake uliotukuka katika kipindi kifupi ambacho yuko madarakani, Watanzania wanaimani kubwa kuwa Rais wetu mpendwa ataendelea kufanya mengi mema na mazuri kwa taifa letu.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** ninamshukuru kwa dhati Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt.

Philip Isdor Mpango, kwa miongozo yake mbalimbali yenye lengo la kuhakikisha kuwa rasilimali madini zinawanufaisha Watanzania na Taifa kwa ujumla. Vilevile, napenda kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake makini na maelekezo anayoyatoa ili kufanikisha utendaji kazi Serikalini, ikiwemo Wizara ya Madini. Viongozi hawa wamekuwa tayari kutusikiliza na kutupa miongozo na maelekezo mbalimbali na hivyo busara zao zimekuwa ni msaada mkubwa katika kufanya maamuzi.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nichukue fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kwa kishindo kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, ninatumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mussa Azan Zungu (Mb.) kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ushindi huo unaashiria imani kubwa tuliyonayo waheshimiwa wabunge kwenu. Ni imani yetu kuwa mtaendelea kuliongoza Bunge kwa umahiri na busara katika kufanya maamuzi kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba niwapongeze Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula (Mb.), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali (Mb.), Makamu Mwenyekiti wa Kamati pamoja na wajumbe wa Kamati hiyo kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutoa ushauri na maelekezo mbalimbali ambayo yanasaidia kuongeza ufanisi wa utendaji kazi wa Wizara. Naahidi kuendelea kuwapa ushirikiano wa dhati katika kuhakikisha kuwa Sekta ya Madini inaendelea kuwanufaisha watanzania.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kutoa shukrani na pongezi kwa Bunge lako Tukufu kwa kazi nzuri ambazo limekuwa likifanya katika kuisimamia na kuishauri Serikali, ikiwemo Wizara ya Madini. Kupitia kwako, naliomba Bunge liendelee kutupatia ushirikiano ili kuiendeleza Sekta hii muhimu katika kujenga uchumi imara na maendeleo endelevu ya Taifa letu. Aidha, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri na

Naibu Mawaziri wote kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuongoza Wizara mbalimbali. Kadhalika, niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya kusimamia Sekta ya Madini.

**10. *Mheshimiwa Spika***, kipekee kabisa, nitumie fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Bukombe kwa kuendelea kunivumilia na kunipa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu kama Mbunge wao. Najua kuna wakati wananikosa jimboni kama Mbunge wao kutokana na majukumu ya kitaifa kama Waziri wa Madini, lakini kwa wema wao wanaendelea kunivumilia na kunipa ushirikiano mkubwa. Nawaahidi kuendelea kuwa mtumishi wao mwaminifu katika kutekeleza shughuli za maendeleo ya Jimbo letu kwa ufanisi.

**11. *Mheshimiwa Spika,*** napenda niwapongeze Dkt. Steven Lemomo Kiruswa (Mb.), Naibu Waziri, Bw. Adolf Hyasinth Ndunguru, Katibu Mkuu, Bw. Msafiri Lameck Mbibo, Naibu Katibu Mkuu na Dkt. Abdulrahman Shabani Mwanga, Kamishna wa Madini, kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuisimamia Sekta ya Madini katika nyadhifa zao. Aidha, nawashukuru viongozi wenzangu, Wenyeviti wa Bodi, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Madini pamoja na wafanyakazi wote kwa ushirikiano na utendaji kazi mzuri katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

**12. *Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie fursa hii kumshukuru mke wangu kipenzi Benadetha Clement Mathayo kwa maombi na upendo wake wa dhati kwangu na watoto wetu. Amekuwa mvumilivu kipindi chote ninapokuwa natekeleza majukumu ya ubunge na uwaziri na kukubali kubeba baadhi ya majukumu yangu ya kifamilia. Aidha, nawashukuru watoto wangu pamoja na familia yangu kwa ujumla kwa upendo, uvumilivu, ushirikiano na maombi yao wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu. Namuomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwabariki na kuwalinda.


**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa masikitiko makubwa niungane na wenzangu kutoa pole kwa wananchi wa Majimbo ya Ushetu, Ngorongoro na Konde kwa kuondokewa na waliokuwa Wabunge wao Waheshimiwa Elias John Kwandikwa, William Ole Nasha na Khatib Said Haji mtawalia. Aidha, nitoe pole kwako kufuatia kifo cha Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa (CCM) kilichotokea tarehe 24 Aprili, 2022. Vilevile, natoa pole za dhati kwa wananchi kwa ujumla wao ambao walipoteza ndugu na mali zao kutokana na ajali, maafa na maradhi yaliyotokea sehemu mbalimbali hapa nchini. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi. Amina.

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kutoa shukrani na pole naomba sasa nijielekeze katika maeneo mahsusi ya hotuba hii ambayo ni: Mwenendo wa biashara ya madini duniani; Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022; na Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023.

## B. MWENENDO WA BIASHARA YA MADINI DUNIANI

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** uchumi wa madini nchini kwa kiasi kikubwa unatokana na madini ya dhahabu, ambayo huchangia takriban asilimia 80 ya mapato yatokanayo na rasilimali madini. Wachambuzi wa masuala ya uchumi duniani walitarajia bei ya dhahabu kuendelea kuwa tulivu kwa mwaka 2022. Hata hivyo, bei ya madini ya dhahabu kwa wakia imepanda kutoka wastani wa dola za Marekani 1,412.98 Julai 2019 hadi kufikia 1,947.83 Machi, 2022 (*Kielelezo Na. 1)*. Kuongezeka kwa bei ya dhahabu kunatokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na uwepo wa UVIKO-19.

*Kielelezo Na1: Mwenendo wa bei ya dhahabu Julai 2019 hadi Machi 2022*




*Chanzo: London Bullion Metal Association – LBMA*

**16. *Mheshimiwa Spika,*** changamoto ya vita kati ya Urusi na Ukraine inaweza kusababisha mahitaji makubwa ya madini ya dhahabu. Hii ni kwa sababu watu na taasisi duniani hupendelea kuhifadhi thamani ya fedha zao katika madini ya dhahabu kwa kuwa ni amana iliyo salama zaidi hasa wakati wa mitikisiko ya kiuchumi. Kwa upande mwingine, ukuaji wa teknolojia umesababisha ongezeko la mahitaji ya madini ya *palladium, nickel, aluminium, cobalt* na madini ya kinywe *(graphite).* Hivyo, bei ya madini hayo inatarajiwa kupanda na kuongeza fursa za uwekezaji.

**17. *Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2021 bei ya madini ya almasi katika soko la dunia iliongezeka na kufikia wastani wa dola za Marekani 241 kwa karati ikilinganishwa na wastani wa dola za Marekani 150 kwa karati mwaka 2020. Hadi Februari 2022, bei ya almasi iliendelea kuongezeka na kufikia wastani wa dola za Marekani 369 kwa karati. Ongezeko hilo limetokana na kupungua kwa mlipuko wa *UVIKO-19* na uhitaji mkubwa wa bidhaa za usonara zinazotumia almasi *(diamond jewellery)* uliojitokeza katika kipindi cha sikukuu za krismasi na mwaka mpya. Hata hivyo, kuna viashiria vya bei ya madini ya almasi kwa mwaka 2022 kubadilika kwa kupanda au kushuka kutokana na nchi ya Urusi ambayo ni mzalishaji mkubwa wa almasi duniani kuwa katika vita na Ukraine.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kunufaika na ongezeko la bei za madini, Wizara inakusudia kuchukua hatua mbalimbali, ikiwemo kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji na kuangalia uwezekano wa kupunguzwa kwa baadhi ya kodi na tozo kwa wachimbaji ili kuwaongezea wigo wa faida na kuchochea uzalishaji zaidi. Aidha, Wizara inaendelea kuhimiza uwekezaji katika madini ya kimkakati ikiwemo *palladium, nickel, aluminium, cobalt* na kinywe *(graphite)* ili kunufaika na ongezeko la mahitaji ya madini hayo duniani. Vilevile, Wizara inaendelea kuhimiza uongezaji thamani madini nchini ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa bidhaa zinazotokana na madini.

## C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

### I. Mapato

***19. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2021/2022, Wizara ya Madini ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 696.4 kutoka katika vyanzo mbalimbali. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 650.0, sawa na asilimia 93.3 zilipangwa kukusanywa na kuwasilishwa Hazina na shilingi bilioni 46.4, sawa na asilimia 6.67 zilipangwa kukusanywa na kutumiwa na taasisi zilizo chini ya Wizara.

***20. Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi, 2022, Wizara ya Madini imekusanya jumla ya shilingi bilioni 484.6, sawa na asilimia 70 ya lengo la mwaka. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 461.6 zilipelekwa Hazina na shilingi bilioni 23.0 zimekusanywa na taasisi zilizo chini ya Wizara kwa ajili ya matumizi ya taasisi husika.

### II. Matumizi

***21. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2021/2022 Wizara ilitengewa bajeti ya shilingi bilioni 66.8 kwa ajili ya matumizi ya Wizara na taasisi zake. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 15.0 zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 51.8 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida, shilingi bilioni18.5 ni kwa ajili ya

mishahara ya watumishi na shilingi bilioni 33.3, kwa ajili ya matumizi mengineyo.

***22. Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Machi, 2022, Wizara imepokea jumla ya shilingi bilioni 39.0 kutoka Wizara ya Fedha na Mipango. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni1.5 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 37.5 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa, shilingi bilioni 13.7zimetumika kulipa mishahara ya watumishi na shilingi bilioni 23.8 ni matumizi mengineyo.

## III. Utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara vya Mwaka wa Fedha 2021/2022

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2021/2022, Wizara ilipanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo: kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa; kuwaendeleza wachimbaji wadogo na kuwawezesha wananchi kushiriki katika uchumi wa madini; kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini; kuhamasisha biashara na uwekezaji katika Sekta ya Madini; kusimamia mfumo wa ukaguzi wa shughuli za migodi; kuzijengea uwezo taasisi zilizo chini ya Wizara ili ziweze kutekeleza majukumu kwa ufanisi; na kuendeleza rasilimaliwatu na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi.

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza maduhuli ya Serikali na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa, Wizara imeimarisha usimamizi na ukaguzi kwenye maeneo ya uchimbaji, mipaka ya nchi pamoja na kuanzisha na kuimarisha masoko na vituo vya uuzaji wa madini. Tangu kuanzishwa kwake hadi kufikia Machi, 2022 jumla ya masoko 42 na vituo vya ununuzi wa madini 75 vimeanzishwa. Uanzishaji na uimarishaji huo umechangia kwa kiasi kikubwa kwenye ukusanyaji wa maduhuli.

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** hatua nyingine za kuimarisha ukusanyaji maduhuli zilizochukuliwa ni pamoja na kuimarisha udhibiti wa biashara haramu na utoroshaji wa madini. Kazi hii hufanywa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali

wakiwemo Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Ofisi ya Usalama wa Taifa, Jeshi la Polisi, Idara ya Uhamiaji, Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya pamoja na raia wema. Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022, madini ya aina mbalimbali yakiwemo dhahabu, vito, mchanga na madini ya viwandani yenye jumla ya thamani ya shilingi milioni 501.2 yalikamatwa katika matukio ya utoroshaji na biashara haramu ya madini katika mikoa ya Mbeya, Morogoro, Manyara, Dodoma, Lindi, Geita, Kilimanjaro, Dar es Salaam na Mwanza.

**26. *Mheshimiwa Spika***, kutokana na juhudi hizo kumekuwa na ongezeko la ukusanyaji wa maduhuli ambapo katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 shilingi bilioni 461.6 zimekusanywa na kuwasilishwa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ikilinganishwa na shilingi bilioni 445.2 zillizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2020/2021, sawa na ongezeko la asilimia 4.

**27. *Mheshimiwa Spika***, mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa umeendelea kuimarika. Katika kipindi cha Januari hadi Septemba, 2021 mchango wa sekta uliongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 7.3 kutoka wastani wa asilimia 6.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Aidha, katika robo mwaka ya Julai hadi Septemba 2021 mchango wa sekta uliongezeka hadi kufikia asilimia 7.9 ikilinganishwa na mchango wa asilimia 7.3 kwa kipindi kama hicho mwaka 2020. Mwenendo huu wa mchango unatoa mwelekeo chanya kuwa Sekta ya Madini itaweza kuchangia hadi asilimia 10 kwenye Pato la Taifa ifikapo mwaka 2025 kama ilivyotarajiwa kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Mpango wa Taifa wa Maendeleo 2021/22-2025/26.

**28. *Mheshimiwa Spika***, mchango wa Sekta ya Madini katika kuliingizia Taifa fedha za kigeni umekuwa ukiimarika. Mwaka 2021, sekta hii ilichangia asilimia 45.9 ya thamani ya bidhaa zote zilizouzwa nje ya nchi na kuliingizia Taifa dola za Marekani milioni 3,103.20. Kwa kipindi cha takribani miaka mitano (5) iliyopita Sekta ya Madini imeendelea kuongoza katika kuliingizia taifa fedha za kigeni.

**29. *Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mapato yaliyotokana na maduhuli na fedha za kigeni kutokana na mauzo ya madini nje ya nchi, Sekta ya Madini pia iliiwezesha Serikali kukusanya shilingi trilioni 1.58 kutoka vyanzo mbalimbali vya kodi mwaka 2021 ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.34 mwaka 2020. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 17.9.

**30. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuhamasisha wawekezaji kuwekeza katika Sekta ya Madini ili kuongeza mchango wa sekta katika Pato la Taifa. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Wizara kupitia Tume ya Madini imetoa leseni mbili (2) za uchimbaji mkubwa wa madini ya dhahabu kwa kampuni ya *Sotta Mining Corporation Limited* inayomilikiwa na *Nyanzaga Mining Company Limited* na Serikali na leseni ya madini ya nikeli kwa kampuni ya *Tembo Nickel Corporation Limited* inayomilikiwa kwa ubia kati ya *Kabanga Nickel Limited* na Serikali. Serikali inamiliki hisa asilimia 16 zisizoshuka thamani (*non-dilutable*) katika kila kampuni.

**31. *Mheshimiwa Spika***, Serikali imekamilisha mazungumzo na kampuni ya uchimbaji wa madini ya almasi ya Williamson *Diamond Limited* ambapo hisa za Serikali zimeongezeka kutoka asilimia 25 hadi asilimia 37. Aidha, Serikali imesaini mikataba na kampuni za uchimbaji wa madini ya graphite kwa kampuni ya *Mahenge Resources Limited (Black Rock Mining Ltd)* na madini ya *heavy mineral sands* Kampuni ya *Jacana Resources Limited (Strandline Resources Ltd)* na kuunda Kampuni za ubia za *Faru Graphite Corporation* na *Nyati Mineral Sands Ltd* mtawalia. Serikali ni mbia katika kila kampuni kwa kumiliki hisa asilimia 16 zisizoshuka thamani.




*Picha Na. 1: Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akishuhudia utiaji saini wa miradi ya uwekezaji ya uchimbaji wa madini tarehe 13 Desemba 2021*

**32. *Mheshimiwa Spika***, thamani ya uwekezaji katika miradi hii unatarajiwa kuwa na thamani ya kiasi cha takriban dola za Marekani milioni 1,672.57. Aidha, uwekezaji huu ni mkubwa kuwahi kutokea katika kipindi cha takriban miongo miwili iliyopita. Vilevile, uwekezaji huu utaongeza ajira na manufaa yatokanayo na uwajibikaji wa kampuni za *madini* kwa jamii *(CSR)* na ushiriki wa watanzania katika uuzaji wa bidhaa na utoaji huduma katika shughuli za madini *(Local Content)*.

**33. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuwaendeleza wachimbaji wadogo na kuwawezesha wananchi kushiriki katika uchumi wa madini, Wizara imeendelea kuzihamasisha taasisi za fedha na benki nchini zikiwemo *NMB, NBC, CRDB* na *KCB* kutoa mikopo. Hadi sasa baadhi ya benki hizo zimeridhia na kuanza kutoa mikopo ambapo jumla ya shilingi bilioni 36 zimekopeshwa kwa wachimbaji wadogo. Aidha, Wizara inaendelea na jitihada za kuzihamasisha taasisi hizo pia kuona uwezekano wa kuwakopesha vifaa wachimbaji hao.

**34. *Mheshimiwa Spika,*** hatua nyingine za uendelezaji wachimbaji wadogo zilizochukuliwa ni pamoja na: kuwapa elimu na *kuwagawia* nakala zipatazo 1,000 za Mwongozo wa Wachimbaji Wadogo; kutoa mafunzo na huduma mbalimbali kwa wachimbaji wadogo wapatao 1,144 waliotembelea

vituo vya mfano vya Katente, Lwamgasa na Itumbi; na vikundi vitano (5) vya wachimbaji wadogo kutoka Singida, Kilindi na Morogoro vimewezeshwa kujua jiolojia ya maeneo wanayomiliki. Aidha, Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)* limekamilisha ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhia vilipuzi na kemikali katika kituo cha Lwamgasa.

**35. *Mheshimiwa Spika,*** *STAMICO* na Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (*GST)* walitoa mafunzo mbalimbali kwa wachimbaji wadogo wapatao 945, wakiwemo *wenye* usikivu hafifu. Mafunzo hayo yalihusisha, uchimbaji salama, biashara ya madini na namna bora ya uchukuaji sampuli na yaliendeshwa katika maeneo ya Nh'oli (Dodoma), Mirerani, Chunya, Simiyu, Geita na Mwanza. Aidha, *GST* ilifanya utafiti maalumu wa jiolojia, jiofizikia na jiokemia katika maeneo ya wachimbaji wadogo wilayani Biharamulo ambapo matokeo yalibaini uwepo wa madini ya kaolini na dhahabu.



*Picha 2: GST ikitoa mafunzo ya nadharia na vitendo kwa wachimbaji wadogo wa madini juu ya namna bora ya uchukuaji wa sampuli za uchunguzi na uchenjuaji - Geita*

**36. *Mheshimiwa Spika,*** *STAMICO* imeendelea kusimamia na kuimarisha vituo vya mfano na kutoa huduma mbalimbali kwa wachimbaji wadogo. Kuanzia Julai, 2021 hadi Machi, 2022 jumla ya tani 4,235.80 za mbale za dhahabu zimechenjuliwa katika vituo vya Lwamgasa, Katente na Itumbi, ambapo jumla ya wakia 3,692.77 za dhahabu

zilizalishwa zikiwa na thamani ya shilingi 12,321,425,618.65 na kulipa serikalini tozo za shilingi 969,607,414.32.

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa shughuli za uchimbaji mdogo zinaendelea kufanyika kwa ufanisi, Serikali imeendelea kuwarasimisha wachimbaji wadogo. Hadi kufikia Machi 2022, Wizara kupitia Tume ya Madini imetoa leseni 5,937 za uchimbaji mdogo wa madini, sawa na asilimia 72.65 ya leseni zote zilitolewa ikilinganishwa na leseni 3,540 zilizotolewa katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Aidha, kufuatia kurasimishwa na kutambuliwa kwa wachimbaji wadogo, mchango wao umeendelea kuongezeka kutoka asilimia 4 kabla ya marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura 123 hadi asilimia 30 kwa sasa.

**38.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhamasisha na kuhakikisha shughuli za uongezaji thamani madini nchini zinaimarika, Serikali imeendelea kukiimarisha Kituo cha Jemolojia Tanzania *(TGC)* kwa kuongeza fedha katika Mwaka wa fedha 2022/23 kwa ajili ya kuboresha miundombinu na kununua vifaa vya kujifunzia. Kituo hicho kinatoa mafunzo ya uongezaji thamani madini ikiwemo utambuzi, ukataji, uchongaji, ung'arishaji madini ya vito na utengenezaji wa bidhaa za usonara katika ngazi ya Astashada na Stashahada. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa vijana wengi wanapata ujuzi katika nyanja hizo na kuwaongezea fursa za kupata ajira au kujiajiri.

**39.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia *STAMICO* imejenga na kusimika miundombinu na mtambo wa kuzalisha makaa ya mawe kwa matumizi ya nyumbani *(coal briquettes)* katika eneo la *TIRDO* - Dar es Salaam. Uzalishaji wa majaribio ulifanyika kwa ufanisi. Aidha, Shirika limeagiza mitambo miwili (2) yenye uwezo wa kuzalisha tani 20 za *coal briquettes* kwa saa ili kuongeza uzalishaji. Mradi huo utawanufaisha watanzania kwa kutoa ajira zaidi ya 200 na kupunguza ukataji miti kwa ajili ya mkaa hivyo kuchangia kutunza mazingira. Picha Na. 3 inaonesha makaa ya mawe kwa ajili ya matumizi ya nyumbani *(Rafiki Briquettes)*.




*Picha Na. 3: Makaa ya mawe kwa ajili ya matumizi ya nyumbani (Coal briquettes)*

**40. *Mheshimiwa Spika,*** viwanda mbalimbali nchini vimeendelea kutumia madini ya viwandani kama malighafi kwa ajili ya kuzalisha bidhaa mbalimbali. Kuanzia julai 2021 hadi Machi 2022 kiasi cha madini ya viwandani kilichozalishwa na kutumiwa na viwanda vya ndani kilikuwa tani milioni 7.6. Uzalishaji na utumiaji wa madini hayo ni muhimu katika kukuza na kuendeleza viwanda vya ndani.

**41. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliandaa na kushiriki maonesho, makongamano na mikutano katika majukwaa mbalimbali. Tarehe 21 hadi 23 Februari 2022, Wizara iliandaa na kushiriki Mkutano wa Nne wa Kimataifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Madini uliofanyika Dar es Salaam; Septemba, 2021 Wizara ilishiriki katika Maonesho ya Teknolojia ya Madini yaliyofanyika mkoani Geita; maonesho kuelekea sherehe za miaka 60 ya Uhuru yaliyofanyika Zanzibar tarehe 03 hadi 09 Desemba, 2021; maonesho ya 45 ya Kimataifa ya biashara ya Sabasaba, 2021; na tarehe 31 Agosti, hadi 2 Septemba, 2021 Wizara ilishiriki warsha kuhusu rasilimali madini katika Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu (*ICGLR*) iliyofanyika Khartoum, Sudan.



*Picha Na. 4: Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa akiwa kwenye banda la maonesho la Wizara ya Madini katika Maonesho ya Teknolojia na Uwekezaji katika Sekta ya Madini Mkoani Geita*

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia Wizara ilishiriki katika jukwaa la uwekezaji kati ya Tanzania na Uingereza lililofanyika Dar es Salaam Novemba, 2021; maonesho ya *Dunia ya Expo 2020* yaliyofanyika Dubai Novemba, 2021; jukwaa la biashara na uwekezaji kati ya Tanzania na Italia lililofanyika Roma nchini Italia Desemba, 2021; na kongamano la madini ya teknolojia nchini Saudi Arabia lililofanyika tarehe 12 hadi 13 Januari, 2022. Ushiriki huo umekuwa na mafanikio ikiwa ni pamoja na kusainiwa kwa mkataba wa ushirikiano katika utafiti na uendelezaji wa leseni za madini kati ya *STAMICO* na Kampuni ya *ACME Consultancy Engineers Pte. Ltd* wenye thamani ya takriban dola za Marekani milioni 300.




*Picha Na. 5: Waziri wa Madini Dkt. Doto Biteko akishuhudia utiaji saini wa makubaliano kati ya STAMICO na kampuni ya ACME Consultant*

**43. *Mheshimiwa Spika,*** biashara ya madini nchini imeendelea kuimarika ambapo katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi 2022 jumla ya kilogramu 39,682.94 za dhahabu, kilogramu 7,102.96 za fedha, karati 155,117.10 za almasi, kilogramu 15,377.44 za Tanzanite ghafi, kilogramu 130,582.28 za Tanzanite za ubora wa chini *(beads)*, karati 81,305.42 za tanzanite iliyokatwa na kusanifiwa, tani 19,355.13 za madini ya shaba na tani 322.49 za madini ya bati zilizalishwa.

**44. *Mheshimiwa Spika,*** vilevile, kilogramu 6,835,746.73 na karati 12,863.29 za madini mengine ya vito ghafi na vito vilivyokatwa na kusanifiwa mtawalia, tani 18,462,591.96 za madini ya ujenzi, tani 956,688.08 za makaa ya mawe, tani 7,843,634.41 za madini mengine ya viwandani, na tani 51,132.33 za madini mengine ya metali zilizalishwa na kuuzwa. Katika kipindi hicho shilingi 429,191,348,141.87 zilikusanywa kama malipo ya mrabaha na ada ya ukaguzi kutoka kwenye madini hayo yenye thamani ya shilingi 6,439,691,493,817.11. makusanyo hao ni ongezeko la asilimia 2.5 ikilinganishwa na shilingi 418,727,438,816.59 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2020/2021.

**45. *Mheshimiwa Spika***, shughuli za uchimbaji na uchenjuaji wa madini huambatana na athari mbalimbali za afya na mazingira. Ili kuhakikisha shughuli za madini zinakuwa na tija na athari zake zinadhibitiwa, kaguzi mbalimbali hufanyika kwa ajili ya kuhakikisha usalama wa watu na mazingira katika maeneo yenye shughuli za madini. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, ukaguzi umefanyika katika migodi mikubwa ya *Geita Gold Mine (GGM), Williamson Diamond Limited (WDL)* na *North Mara (NMGM).*

**46. *Mheshimiwa Spika***, pia ukaguzi ulifanyika katika migodi ya kati sita (6) ambayo ni: migodi ya dhahabu ya Shanta *(*Singida *Gold Project); PU BO Mining Ltd*; *Sunshine* (Singida), *ZEM (T) Co. Ltd; Cata Mining Co. Ltd* (Mara) na Busolwa *Mining Ltd* (Geita). Aidha, leseni 5,246 za uchimbaji mdogo zilikaguliwa katika mikoa mbalimbali ya kimadini nchini.

**47.** ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na kaguzi zilizofanyika, migodi mingi imeonekana kuwa inazingatia taratibu za uendeshaji migodi kwa mujibu wa sheria. Hata hivyo, katika baadhi ya migodi, kaguzi zilibainisha kuwepo kwa hali ya kutozingatiwa kwa taratibu za uendeshaji wa migodi. Hali hiyo ni pamoja na: uwepo wa makazi na shughuli za uchimbaji mdogo karibu na migodi, kutozingatiwa kwa utaratibu wa utunzaji wa mazingira, kutokuwepo kwa wataalamu na wasimamizi wa masuala ya usalama wa wafanyakazi na mazingira migodini, ukosefu wa vifaa vya usalama kwa wafanyakazi na kutokuwepo kwa stoo za kuhifadhia baruti.

**48.** ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na mapungufu yaliyobainika katika baadhi ya migodi, Wizara kupitia Tume ya Madini imechukua hatua kadhaa zenye lengo la kuhakikisha kuwa kasoro zilizobainika zinarekebishwa. Hatua hizo ni pamoja na kutoa maelekezo mahsusi kwa wamiliki wa migodi hiyo kuchukua hatua za kuondoa upungufu uliobainika wakati wa kaguzi.

**49.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara pia imeandaa mpango wa kutoa mafunzo kwa ajili ya uchimbaji salama, utunzaji wa mazingira, usalama wa wafanyakazi pamoja na usimamizi salama wa baruti kwa wachimbaji wadogo na utekelezaji wake umeanza. **Nitoe wito kwa wachimbaji madini wote hapa nchini kufanya shughuli zao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia Sekta ya Madini ili kuhakikisha shughuli za uchimbaji zinakuwa endelevu kwa kuzingatia afya, usalama wa watu na mazingira katika maeneo ya migodi**.

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuzijengea uwezo taasisi zake, Wizara imewezesha ununuzi wa vitendea kazi kwa ajili ya maabara pamoja na kuanza ujenzi wa jengo la kuhifadhia sampuli za miamba *(coreshed)* linalojengwa eneo la Kizota – Dodoma kwa ajili ya Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (*GST*). Aidha, ili kuimarisha usimamizi, ufuatiliaji na ukusanyaji wa maduhuli, Tume ya Madini iliwezeshwa kupata fedha za kununua magari 40 ambapo hadi sasa magari saba (7) yamekwishapokelewa (Picha Na. 6). Vilevile, *STAMICO*

iliwezeshwa kupata vifaa vya utafutaji na uchimbaji wa madini ambavyo ni *excavator, drill rig, crane na survey equipment* ili kuimarisha shughuli hizo.



*Picha Na. 6: Waziri wa Madini Mhe. Dkt. Doto Biteko akizindua Magari kwa ajili ya Tume ya Madini*.

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** watumishi ni rasilimali muhimu zaidi katika taasisi yoyote kwa sababu ndiyo inayowezesha rasilimali nyingine kutumika kwa tija na kuleta mafanikio katika sekta zote za uchumi ikiwemo Sekta ya Madini. Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, watumishi 400 wa Wizara na taasisi zake wamepandishwa vyeo. Aidha, watumishi 94 wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu na Watumishi 55 wamewezeshwa kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi katika nyanja mbalimbali nje na ndani ya nchi.

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuboresha mazingira ya kazi ikiwa ni pamoja na ujenzi wa majengo matatu (3) ya ofisi. Majengo hayo ni ofisi za Makao Makuu ya Wizara katika Mji wa Serikali - Mtumba, ofisi ya Makao Makuu ya Tume ya Madini – eneo la Kilimani Dodoma na ofisi ya Afisa Madini Mkazi *(RMO)* - Geita. Aidha, vitendea kazi mbalimbali vimenunuliwa vikiwemo magari na kompyuta kwa ajili ya kuwawezesha watumishi kufanya kazi kwa ufanisi.

## IV. Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

***53. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Fedha za Maendeleo kwa ajili ya utekelezaji

wa miradi mbalimbali zilizopokelewa ni shilingi bilioni 7.4, ambapo shilingi bilioni 1.52ni kutoka kwenye bajeti ya maendeleo ya mwaka wa fedha unaoendelea na shilingi bilioni 5.9 ni kutoka katika Akaunti ya Amana. Miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: ukamilishaji wa ujenzi wa vituo vya umahiri vya Songea, Mpanda na Chunya; ujenzi wa ofisi za Makao Makuu ya Wizara awamu ya pili katika Mji wa Serikali – Mtumba; ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Tume ya Madini – eneo la Kilimani Dodoma; kuanza hatua za awali za ujenzi wa jengo la ofisi ya Afisa Madini Mkazi – Geita na ununuzi wa vifaa vya maabara na vitendea kazi kwa ajili ya Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (*GST*).

## V. Utekelezaji katika Maeneo Mengine

### (a) Utekelezaji wa Ushirikishwaji wa Watanzania na Wajibu wa Kampuni kwa Jamii katika Sekta ya Madini

***54. Mheshimiwa Spika*****,** Serikali inatambua umuhimu wa wananchi kushiriki katika shughuli za uzalishaji kwa kuzifungamanisha Sekta ya Madini na nyingine ili kuendelea kukuza uchumi wao na wa Taifa kwa ujumla. Ili kulitekeleza hilo, Serikali imeweka Sheria na Kanuni za Mpango wa Ushirikishaji wa Watanzania (*Local Content)* na wajibu wa kampuni kwa jamii *(Corporate Social Responsibility)*. Kwa mujibu wa Sheria ya Madini Sura 123, kila mgodi unapaswa kuajiri wataalam wa ndani na kutumia bidhaa na huduma kwa kadri zinavyopatikana nchini. Suala hili linasimamiwa kwa kuzitaka kampuni zote zinazojishughulisha na utafutaji, uchimbaji, usafishaji na biashara ya madini kuwasilisha Mipango ya Ushirikishwaji wa Watanzania katika shughuli zao.

***55. Mheshimiwa Spika*****,** kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022, Wizara kupitia Tume ya Madini ilipokea na kuchambua jumla ya mipango 378 ya ushirikishwaji wa watanzania katika Sekta ya Madini kutoka kwa wamiliki wa leseni za madini na watoa huduma migodini, ambapo mipango 366 kati ya hiyo ilikidhi vigezo na kuidhinishwa. Mipango 12 iliyobaki haikukidhi vigezo na wahusika walielekezwa kuifanyia maboresho kwa mujibu wa Sheria ya Madini Sura 123.

***56. Mheshimiwa Spika*****,** kati ya kampuni 378 zilizowasilisha na kuidhinishiwa mipango ya ushirikishwaji wa watanzania, kampuni 10 ni za uchimbaji mkubwa, 14 uchimbaji wa kati, 4 uchimbaji mdogo, 7 za utafutaji wa madini, 3 leseni ya usafishaji na kampuni 340 za watoa huduma migodini.

***57. Mheshimiwa Spika*****,** ushiriki wa Watanzania katika shughuli za madini umeendelea kuimarika na kuongezeka. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, idadi ya watanzania walioajiriwa katika kampuni za utafutaji, uchimbaji, usafishaji na watoa huduma imefikia 14,308 ikilinganishwa na 7,151 katika kipindi kama hicho Mwaka wa Fedha 2020/2021. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 100. Aidha, katika kipindi rejewa shilingi trilioni 5.2 zimetumiwa na migodi kulipia bidhaa na huduma mbalimbali zinzozalishwa nchini zilizotolewa katika migodi hiyo ikilinganishwa na shilingi trilioni 2.4 zilizotumika katika kipindi kama hicho Mwaka wa Fedha 2020/2021.

***58. Mheshimiwa Spika*****,** Serikali imeendelea kufuatilia na kusimamia wajibu wa kampuni kwa jamii zinazozunguka migodi *(CSR)*. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, migodi 13 ilitoa jumla ya shilingi 16,078,138,114.00 kwa ajili ya miradi ya afya, elimu, maji, barabara, na miradi ya kiuchumi katika Halmashauri za Wilaya ya Tarime, Msalala, Nyang'hwale, Kahama, Songwe, Geita na Geita Mji. Miradi hii imeboresha hali za maisha ya wananchi wa maeneo hayo na kuleta maendeleo katika Halmashauri zinazozunguka migodi.

### (b) Uboreshaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo katika Sekta ya Madini

***59. Mheshimiwa Spika*****,** Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa wawekezaji katika Sekta ya Madini wanafanya kazi zao katika mazingira ya kisheria yenye tija kwa pande zote mbili yaani Serikali na Wawekezaji. Katika kutekeleza hilo, maboresho mbalimbali katika Sheria, na Kanuni zinazosimamia Sekta ya Madini yamefanyika. Miongoni mwa maboresho hayo ni pamoja na marekebisho katika Kanuni za Madini (Eneo

Tengefu la Mirerani), *(The Mining (Mirerani Controlled Area*) (*Amendment) Regulations, 2021*).

***60. Mheshimiwa Spika*,** marekebisho hayo yanaelekeza kuwa biashara ya madini ya Tanzanite pamoja na shughuli zote za ukataji, ung'arishaji au shughuli za uongezaji thamani madini kufanyika ndani ya Eneo Tengefu la Mirerani au eneo lolote la Mirerani litakaloidhinishwa kwa maandishi. Kanuni hizo zilizoanza kutumika tarehe 9 Julai, 2021 zilitangazwa katika Tangazo la Serikali Na. 592 la tarehe 9 Julai, 2021.

***61. Mheshimiwa Spika,*** marekebisho mengine yamefanyika katika Kanuni za Madini (Haki Madini) za Mwaka 2018 ambayo yanamwezesha Waziri kuondoa masharti ya kanuni zinazohusu haki madini kwa waombaji wa leseni za Uchimbaji wa Kati *(Mining Licence)* na Leseni za Uchimbaji Mkubwa *(Special Mining Licence)* ambao watakuwa na makubaliano maalum na Serikali ambayo kwayo Serikali ni mwanahisa au itakuwa mwanahisa. Marekebisho hayo yamefanyika kupitia Tangazo la Serikali Na. 593 la tarehe 9 Julai, 2021. Lengo la marekebisho hayo ni kuiwezesha Serikali kushiriki kikamilifu kama mbia katika uendeshaji wa shughuli za uchimbaji wa madini.

**(c) Kuelimisha Umma Kuhusu Sekta ya Madini**

***62. Mheshimiwa Spika*,** katika kutoa elimu kwa umma kuhusu Sekta ya Madini, masuala yanayopewa kipaumbele ni pamoja na: uelewa kuhusu Sera na Sheria; wajibu wa kampuni kwa jamii; ushiriki wa watanzania; matumizi ya teknolojia bora katika uchimbaji na uchenjuaji wa madini; uhifadhi na matumizi bora ya baruti; taratibu za utoaji wa leseni za madini; umuhimu wa masoko ya madini; fursa za uwekezaji; na usalama, afya na utunzaji wa mazingira. Katika kutoa elimu kwa umma njia mbalimbali hutumika ikiwa ni pamoja na mikutano, maonesho, redio, runinga, magazeti, tovuti na mitandao ya kijamii.

**(d) Uendelezaji na Uboreshaji wa Eneo Tengefu la Mirerani**

***63. Mheshimiwa Spika*,** kufuatia kukamilika kwa ujenzi na usimikaji wa miundombinu ikiwemo taa, kangavuke, kamera

za ulinzi na barabara inayozunguka ukuta kwa ndani katika Eneo Tengefu la Mirerani, hivyo udhibiti wa utoroshaji wa madini ya Tanzanite umeimarika. Hatua zilizochukuliwa na Serikali zimeboresha upatikanaji wa tozo stahiki zinazotokana na biashara ya madini hayo. Kabla ya ujenzi na usimikaji wa miundombinu, uzalishaji ulikuwa kilogramu 1,964.75 kwa mwaka 2018/2019 ikilinganishwa na kilogramu 3,198.65 za tanzanite zilizozalishwa kipindi cha kuanzia Julai 2021 hadi Machi 2022.

**(e) Kusimamia Shughuli za Baruti na Utekelezaji wa Sheria ya Baruti.**

***64. Mheshimiwa Spika***, baruti ni muhimu katika shughuli za uchimbaji wa madini na hutumika kulipua miamba migumu wakati wa uchimbaji wa madini. Pamoja na umuhimu wake katika shughuli za madini, baruti ina madhara makubwa ikitumika au kuhifadhiwa isivyo salama. Ili kuhakikisha kuwa baruti haileti madhara kwa jamii na mazingira, Serikali imeweka utaratibu wa utoaji wa vibali vya uagizaji, utengenezaji, usafirishaji, utunzaji na utumiaji wa baruti.

***65. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 vibali vya baruti vilitolewa kwa kampuni na wafanyabiashara mbalimbali kama ifuatavyo: vibali 225 vya kuingiza baruti nchini; vibali 21 vya kufanya biashara ya baruti; vibali 21 vya kusafirisha baruti kwenda nje ya nchi; na vibali 37 vya kupitisha baruti nchini kwenda nchi nyingine. Aidha, vibali saba (7) vya kutengeneza baruti vimetolewa kwa kampuni tatu ambazo ni *Dangote Company Limited* (Mtwara), *Mbogo Mining and General Supply Limited* (Pwani na Mbinga) na *Orica (T) Limited* (Geita).

***66. Mheshimiwa Spika***, leseni tatu (3) za viwanda vya kutengeneza baruti zimetolewa kwa kampuni mbili (2) ambazo ni *Mbogo Mining and General Supply Limited* (Leseni ya kutengeneza *detonator explosives* Wilaya ya Magu - Mwanza) na kampuni ya *Solar Nitrochemicals Limited* (Leseni ya kutengeneza *ANFO na Emulsion* na leseni ya kutengeneza *detonators explosives* Kisarawe – Pwani). Aidha, leseni sita

(6) za kutengeneza baruti kwa kutumia magari maalum *(Mobile Manufacturing Unit - MMU)* zilitolewa kwa kampuni mbili (2) za *Solar Nitrochemicals Limited na Nitro explosive (T) Limited. Solar Nitrochemicals Limited* imepewa leseni nne (4) na *Nitro explosive (T) Limited* imepewa leseni mbili (2). Pia, leseni 18 za maghala ya kuhifadhia baruti zimetolewa kwa kampuni na wafanyabiashara wa baruti. Vibali na leseni za baruti vilivyotolewa zimeipatia Serikali jumla ya shilingi 453,053,800.0.

***67. Mheshimiwa Spika***, kutolewa kwa leseni za viwanda vya kuzalisha baruti nchini ni hatua muhimu kiuchumi kwani viwanda hivyo vitakapoanza uzalishaji vitakuwa na manufaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoa ajira, kulipa kodi Serikalini na uhakika wa upatikanaji wa baruti kwa wakati na kwa gharama nafuu.

***68. Mheshimiwa Spika***, kutokana na madhara yanayoweza kusababishwa na matumizi yasiyokuwa sahihi ya baruti, ukaguzi ulifanyika ili kufuatilia utengenezaji na utunzaji wa baruti katika viwanda vya kutengeneza baruti katika kampuni tatu (3) ambazo ni Mbogo *Mining & General Supply Limited mkoani Mwanza, Solar Nitrochemical Limited* mkoani Pwani na *Nitro Explosive (T) Limited* mkoani Lindi ambapo kampuni ya Mbogo *Mining & General Supply Limited* na *Solar Nitrochemicals Limited* zilikidhi vigezo na kupewa leseni. Aidha, kampuni ya *Nitro Explosive (T) Limited* haikupewa leseni kwa kuwa ujenzi wake haukukidhi matakwa ya Sheria ya Baruti.

***69. Mheshimiwa Spika****,* kaguzi nyingine za baruti zilifanyika kwenye ujenzi wa maghala ya kuhifadhia baruti kwa kampuni za *Zem Development Co. Limited* Mkoa wa Shinyanga na *Ilolo Investment Limited* Mkoa wa Lindi na leseni za maghala ya kuhifadhia baruti zilitolewa kwa kampuni hizo. Aidha, ukaguzi ulifanyika kwenye eneo la ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza baruti cha kampuni ya *Tan Nobel Company Limited* katika kijiji cha Makombe – Bagamoyo. Kibali kilitolewa kwa kampuni hiyo baada ya kukidhi matakwa ya Sheria ya Baruti na Kanuni zake.

***70. Mheshimiwa Spika***, kaguzi tatu (3) zilifanyika kwenye maeneo ya ujenzi wa maghala ya kuhifadhia baruti katika vijiji vya Kinzagu na Makombe, Wilaya ya Bagamoyo na kijiji cha Makanga Vigoli, Wilaya ya Ulanga. Kupitia kaguzi hizo vibali vya ujenzi wa maghala ya kuhifadhia baruti vilitolewa kwa wahusika baada ya kujiridhisha kuwa maeneo yaliyopendekezwa yanafaa kwa mujibu wa Sheria ya Baruti.

**(f) Masuala Mtambuka**

***71. Mheshimiwa Spika***, moja ya masuala mtambuka yanayotekelezwa na Wizara ni pamoja na kutoa elimu na huduma kwa waathirika wa *UKIMWI* na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa (*MSY*). Wizara imeendelea kutoa huduma kwa watumishi waliojitokeza wanaoishi na Virusi vya *UKIMWI* kwa kutoa fedha kwa ajili ya lishe bora, dawa na vifaa kinga ili kuimarisha afya zao. Aidha, mafunzo kuhusu udhibiti wa *MSY* kwa watumishi na upimaji wa hiari umekuwa ukifanyika mara kwa mara.

***72. Mheshimiwa Spika***, kwa lengo la kuboresha afya za watumishi na kuimarisha ushirikiano mahali pa kazi, Wizara imeshiriki katika mabonanza na michezo mbalimbali iliyofanyika nchini, ikiwemo SHIMIWI. Pia, Wizara imeendelea kuhamasisha watumishi kujua afya zao na kujikinga na magonjwa yanayoambukizwa ukiwemo UVIKO-19.

**VI. Utekelezaji wa Shughuli za Taasisi Zilizo Chini ya Wizara**

***73. Mheshimiwa Spika***, Wizara inasimamia taasisi tano (5), ambazo ni Tume ya Madini; Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (*GST*); Shirika la Madini la Taifa (STAMICO); Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia (*TEITI*) na Kituo cha Jemolojia Tanzania (*TGC*).

***74. Mheshimiwa Spika***, taasisi hizi zimekasimiwa majukumu mbalimbali kama ifuatavyo: Tume ya Madini ina jukumu la kusimamia na kudhibiti shughuli zote zinazohusiana na Sekta ya Madini zikiwemo utafutaji, uchimbaji, uongezaji thamani na biashara ya madini; Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)*

lina majukumu ya kuwekeza katika miradi ya kimkakati kwa niaba ya Serikali na kuwaendeleza wachimbaji wadogo; *GST* ina jukumu la kutoa takwimu na taarifa za jiosayansi na majanga asili ya jiolojia ili kuwezesha kufanya maamuzi sahihi katika uwekezaji endelevu; *TEITI* ina jukumu la kuhakikisha uwazi na uwajibikaji katika uvunaji wa rasilimali madini, mafuta na gesi asilia; na *TGC* ina jukumu la kutoa mafunzo ya uongezaji thamani madini ikiwa ni pamoja na utambuzi, ukataji, uchongaji, ung'arishaji wa madini ya vito na utengenezaji wa bidhaa za usonara.

Utekelezaji kwa kila taasisi ni kama ifuatavyo: -

**(a) Tume ya Madini**

***75. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022 pamoja na kutekeleza jukumu la kusimamia uzalishaji wa madini na ukusanyaji wa maduhuli kama ilivyoainishwa hapo awali, Tume ya Madini imetekeleza kazi zifuatazo: -

**(i) Utoaji wa Leseni za Madini**

***76. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Tume ya Madini imetoa jumla ya leseni 8,172 ikilinganishwa na leseni 6,314 katika kipindi kama hicho Mwaka wa Fedha 2020/2021, sawa na ongezeko la asilimia 17.3. Leseni hizo zinajumuisha leseni mbili (2) za uchimbaji mkubwa, leseni 5 za uchimbaji wa kati, leseni 282 za utafutaji wa madini, leseni 5,937 za uchimbaji mdogo, leseni 49 za uchenjuaji wa madini, leseni mbili (2) za usafishaji wa madini na leseni 1,895 za biashara ya madini.

**(ii) Usimamizi wa Masoko ya Madini Nchini**

***77. Mheshimiwa Spika,*** tangu kuanzishwa kwa utaratibu wa kuwa na masoko ya madini mwaka 2019, idadi ya masoko na vituo vya ununuzi vilivyoanzishwa hadi kufikia Machi, 2022 ni 42 na 75 mtawalia. Kwa mwaka 2021/2022 yameanzishwa masoko mawili (2) na vituo 17 vya ununuzi wa madini. Masoko na vituo hivi vimeongeza ufanisi na tija kwenye usimamizi wa

biashara ya madini na ukusanyaji wa maduhuli hapa nchini. Aidha, utaratibu huo umechangia kupunguza utoroshaji na biashara haramu ya madini. **Niendelee kuwasihi wananchi na wadau wote kuuza na kununua madini katika masoko na vituo vinavyotambulika.**

***78. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 thamani ya biashara ya madini katika masoko ya madini imeongezeka na kufikia takribani shilingi trilioni 1.782. Kutokana na biashara hiyo Serikali imekusanya mrabaha na ada ya ukaguzi ya takribani shilingi bilioni 123.58, ikilinganishwa na shilingi bilioni 109.23 katika kipindi kama hicho Mwaka wa Fedha 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia 13.14.

**(iii) Utambuzi na Uthaminishaji wa Madini Yanayosafirishwa Nje ya Nchi**

***79. Mheshimiwa Spika,*** ili Serikali iweze kupata mapato yake stahiki kutokana na madini yanayosafirishwa nje ya nchi, Sheria inaitaka Tume ya Madini kufanya utambuzi na uthaminishaji wa madini pamoja na kutoa vibali vya usafirishaji.
Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 madini yaliyosafirishwa nje ya nchi yalihusisha dhahabu, almasi, madini ya vito ghafi, vito vilivyokatwa na kusanifiwa, madini ya ujenzi, madini ya bati *(tin)*, madini ya shaba, makaa ya mawe na mengineyo yenye jumla ya thamani ya takribani shilingi trilioni 8.3 na kuipatia Serikali mapato ya shilingi bilioni 597.53.

**(iv) Ukaguzi wa Hesabu za Fedha na Kodi**

***80. Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Madini ina jukumu la kukagua hesabu za fedha za migodi mikubwa na ya kati ili kubaini gharama za uwekezaji na uendeshaji kwa madhumuni ya kukusanya taarifa za kikodi na kuziwasilisha Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* na mamlaka nyingine zinazohusika. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 Tume ya Madini ilifanya kaguzi za hesabu za fedha na mapitio ya kodi kwa

kampuni nane (8). Kati ya hizo, kaguzi tano (5) zilihusu miradi ya barabara inayotumia madini ujenzi na kaguzi tatu (3) zilihusu migodi ya kati ya uchimbaji wa madini ya dhahabu ambayo ni *CATA Mining Company Ltd, Zem Tanzania Company Ltd* na *MMG Gold Limited* zilizopo mkoani Mara.

***81. Mheshimiwa Spika,*** kaguzi hizo zilibaini kutolipwa ipasavyo kwa mrabaha pamoja na ada ya ukaguzi; kujumuishwa kwa gharama zisizostahili katika ukokotoaji wa kodi; na kuwepo kwa baadhi ya watoa huduma ambao hawakutozwa kodi ya zuio. Aidha, ilibainika kuwa kuna utekelezaji hafifu wa matakwa ya Sheria ya Madini kuhusu uwajibikaji wa kampuni kwa jamii na ukiukwaji wa baadhi ya kanuni za ushirikishwaji wa watanzania na hatua stahiki zilichukuliwa.

***82. Mheshimiwa Spika,*** baada ya kukamilika kwa ukaguzi kwa kampuni tano za ujenzi wa barabara, ilibainika uwepo wa malipo pungufu ya maduhuli mbalimbali ya Serikali kiasi cha shilingi 2,214,129,611.72. Kampuni hizo zimekubali kulipa maduhuli hayo ambayo awali hayakulipwa.

**(v) Huduma za Maabara**

***83. Mheshimiwa Spika***, Tume ya Madini ina maabara moja iliyopo jijini Dar es Salaam. Maabara hiyo hutumika katika uchunguzi wa ubora, kiasi cha madini na aina za madini yaliyozalishwa na wachimbaji wakubwa, wa kati na wadogo hapa nchini. Hadi Machi 2022, sampuli 1,398 za mikuo ya dhahabu *(gold bars)* na sampuli 851 za madini ya shaba kutoka katika migodi mikubwa na ya kati zilifanyiwa uchunguzi katika maabara hiyo. Uchunguzi huo ulilenga kupata kiasi halisi na thamani ya madini kwa ajili ya kuhakiki kiasi cha tozo ambacho Serikali inapaswa kulipwa kutokana na thamani halisi ya madini hayo.

***84. Mheshimiwa Spika,*** maabara hii pia inatoa huduma kwa wadau mbalimbali wa madini ambapo katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 imefanya uchunguzi wa sampuli 2,267 na kukusanya ada ya huduma kiasi cha shilingi 195,524,000.

**(vi) Uendelezaji na Usimamizi wa Mifumo ya TEHAMA**

***85. Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Madini imeendelea na ujenzi wa mfumo mpya wa utoaji na usimamizi wa leseni za madini. Hadi Machi, 2022 ujenzi wa mfumo huo umefikia asilimia 52. Ujenzi na uendelezaji wa mfumo huo unafanywa na wataalamu wa ndani ya nchi.

***86. Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Madini imeendelea kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na madini ya ujenzi na viwandani kwa kutumia mashine za *Point of Sale (PoS)*. Utaratibu wa kutumia *PoS* umeonesha matokeo chanya katika ukusanyaji wa maduhuli. Takwimu zinaonesha kuwa, kabla ya matumizi ya *PoS* wastani wa makusanyo kwa kipindi cha Oktoba 2020 hadi Februari 2021 makusanyo yatokanayo na madini ya ujenzi yalikuwa shilingi 5,852,566,156.38 ikilinganishwa na shilingi 6,489,501,216.12 baada ya matumizi ya *PoS* kwa kipindi kama hicho Mwaka 2021/2022 ikiwa ni ongezeko la asilimia 9.3. Kutokana na mafanikio hayo, Tume ya Madini inaendelea kuimarisha matumizi ya mashine za *PoS* katika vyanzo vyote vya ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na madini ya ujenzi na ya viwandani.

**(b) Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)***

***87. Mheshimiwa Spika,*** *STAMICO* imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji, usafishaji na uuzaji wa madini pamoja na kutoa huduma mbalimbali katika Sekta ya Madini ikiwemo uchorongaji na utoaji wa ushauri wa kitaalam. Utekelezaji wa majukumu hayo unafanyika kupitia njia tatu (3) ambazo ni: kuanzisha na kuendeleza miradi yake yenyewe ikiwa ni pamoja na kutoa huduma za uchorongaji na ushauri wa kitaalam; kuendeleza na kusimamia kampuni tanzu; na kuendesha kampuni za ubia.

**(i) Kuanzisha na Kuendeleza Miradi yake Yenyewe**

***88. Mheshimiwa Spika,*** Shirika linatekeleza miradi mitatu (3) kupitia vyanzo vyake vya mapato mbalimbali. Miradi hiyo ni:

mradi wa makaa ya mawe wa Kabulo-Kiwira; mradi wa makaa ya kupikia (*coal briquettes*); na mradi wa kuuza kemikali na vilipuzi.

***89. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, katika mradi wa Kabulo, tani 17,324 za makaa ya mawe zilichimbwa ambapo tani 12,792 zenye thamani ya shilingi 1,063,312,091.0 ziliuzwa na kulipa serikalini shilingi 174,191,290.87 ikiwa ni mrabaha na ada ya ukaguzi. Aidha, shirika limeingia makubaliano ya awali na *TANESCO* ya kuendeleza mradi wa Kiwira ambapo shirika litakuwa na jukumu la kuchimba makaa ya mawe na *TANESCO* kuzalisha umeme wa *MW 200* na kuusambaza.

***90. Mheshimiwa Spika,*** shirika limeanza kutekeleza Mpango Mkakati wa Uchimbaji wa Makaa ya Mawe kwa wingi *(Massive Coal Mining Plan – 1,200,000 tons/year)* ambao unalenga kuongeza ubora na uzalishaji ili kumudu ushindani katika soko na kuongeza mauzo. Ili kufikia lengo hilo *STAMICO* imekamilisha ukarabati wa mgodi wa chini wa Kiwira na inaendelea na matengenezo ya barabara kupitia mto Mwalisi ambayo inaunganisha mgodi wa Kabulo na Kiwira. Ukarabati wa barabara unaendelea na matengenezo ya daraja yamekamilika na linapitika. Barabara hiyo itapunguza gharama ya usafirishaji wa makaa ya mawe kutokana na kupungua kwa umbali kutoka kilometa 38 mpaka kilometa 7.



*Picha Na. 7: Daraja la Mto Mwalisi*

***91. Mheshimiwa Spika,*** ili kupunguza changamoto ya uharibifu wa mazingira, STAMICO imeanzisha mradi wa makaa ya kupikia *(Coal briquettes)*. Kwa kuanzia shirika limenunua na kusimika mtambo wa majaribio wenye uwezo wa kuzalisha tani 2 kwa saa ambao umejaribiwa na kuonesha mafanikio. Aidha, shirika limeagiza mitambo miwili mingine yenye uwezo wa kuzalisha tani 20 kwa saa kwa kila mmoja inayotegemewa kuwasili nchini ifikapo Juni, 2022. Tayari *TBS* wameshawapatia *STAMICO* cheti cha ubora wa makaa hayo na hivyo uzalishaji mkubwa unatarajia kuanza.

***92. Mheshimiwa Spika,*** shirika limeanzisha mradi wa kuuza kemikali, baruti na vilipuzi kwa wachimbaji wadogo. Mradi huu unatekelezwa kwenye vituo vya mfano vya Lwamgasa, Katente na Itumbi na katika mgodi wa *STAMIGOLD*. Aidha, shirika linategemea kuanza kuuza kemikali na vilipuzi katika migodi mingine ya kati na mikubwa nchini ili kuongeza wigo wa wateja wake na kusogeza huduma hiyo karibu na wachimbaji. Shirika limeanza hatua za ununuzi wa baruti, vilipuzi na kemikali ili kuwawezesha wachimbaji wadogo kupata zana hizo karibu na maeneo yao ya kazi. Hadi Machi, 2022 shirika limepata mapato ya shilingi 568,983,500 kutokana na mauzo ya kemikali na vilipuzi.

**(ii) Huduma za Uchorongaji na Ushauri wa Kitaalam**

***93. Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2022 *STAMICO* ina mitambo tisa (9) ya uchorongaji. Aidha, shirika limenunua mitambo mitano (5) ya uchorongaji ambayo inatarajiwa kuwasili nchini kabla ya Juni, 2022 na kufanya shirika kuwa na jumla ya mitambo 14. Ongezeko la mitambo hiyo litawezesha shirika kutekeleza kandarasi za uchorongaji kwa mfumo wa *RC* na *DD* kwa ufanisi. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa mafanikio hayo yanatokana na maboresho ya kimuundo pamoja na usimamizi wa shirika yaliyofanywa na Serikali kupitia Wizara ya Madini. Vilevile, kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/2022 shirika limepata kandarasi kubwa tatu (3) za uchorongaji zenye thamani ya shilingi bilioni 17.5.

**(iii) Kampuni Tanzu ya *STAMIGOLD***

***94. Mheshimiwa Spika,*** kampuni ya *STAMIGOLD* inamilikiwa na *STAMICO* kwa hisa asilimia 99 na Ofisi ya Msajili wa Hazina inamiliki asilimia 1 ya hisa. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 mgodi umezalisha wakia 7,106 za dhahabu na wakia 1,059 za madini ya fedha zote kwa pamoja zikiwa na thamani ya shilingi bilioni 29.84. kutokana na mauzo hayo, shilingi bilioni 2.09 zimelipwa Serikalini kama mrabaha, ada ya ukaguzi, tozo mbalimbali na kutoa huduma kwa jamii inayozunguka mgodi.

***95. Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kuongeza uhai wa mgodi, STAMIGOLD ilifanya utafiti kwenye eneo la mgodi na kubaini uwepo wa akiba ya tani 2,769,919 za mashapo ya dhahabu zenye kiwango cha 1.00*g/t* ambazo ni sawa na wakia 88,800. Uwepo wa mashapo hayo utaongeza uhai wa mgodi kwa miaka mitano (5) kuanzia Juni, 2021. Aidha, mgodi bado una mashapo dhaniwa *(Inferred Resource)* ndani ya *SML157/2003* yenye wakia 106,854 za dhahabu ambazo utafiti wake bado unaendelea. Inakadiriwa kwamba matokeo ya utafiti huo yataongeza uhai wa mgodi kwa miaka 7 na hivyo kufanya maisha ya mgodi kuongezeka hadi miaka 12.

***96. Mheshimiwa Spika***, mgodi wa *STAMIGOLD* umekuwa na changamoto ya gharama kubwa za uzalishaji kutokana na kutumia nishati ya mafuta katika kuzalisha umeme. Ili kuondoa changamoto hiyo, kazi ya kuunganisha mgodi katika gridi ya Taifa kupitia *TANESCO* imeendelea ambapo umeme umeshafika katika eneo la mgodi na hatua ya kukamilisha kituo kidogo cha kupozea umeme *(sub station)* ili uanze kutumika inaendelea. Mgodi unatarajiwa kuokoa takribani shilingi milioni 700 kwa mwezi baada ya kuanza kutumia umeme wa *TANESCO*.

***97. Mheshimiwa Spika***, mgodi pia umeendelea kulipa deni la wazabuni na watoa huduma ambapo hadi Desemba, 2021 kampuni ya STAMIGOLD ilikuwa inadaiwa shilingi bilioni 21.032. Deni hilo lilianza kulipwa Januari, 2022 kwa mujibu wa makubaliano yaliyofanyika ya kulipa shilingi 572,000,000 kila

mwezi ambapo hadi Machi, 2022 malipo ya shilingi 1,716,000,000 yamefanyika. *STAMIGOLD* itaendelea kulipa deni kulingana na makubaliano.

### (iv) Miradi inayotekelezwa kwa Ubia

### Kiwanda cha Kusafisha Dhahabu - Mwanza

***98. Mheshimiwa Spika,*** kiwanda cha *Mwanza Precious Metal Refinery* kina uwezo wa kusafisha dhahabu kwa kiwango cha kimataifa cha 999.9 *purity.* Kiwanda hiki bado kinafanya kazi kwa kiwango cha chini ikilinganishwa na uwezo wake wa uzalishaji. Ili kukabiliana na changamoto hiyo na kuongeza uzalishaji kiwanda kimetenga dola za Marekani milioni 150 ikiwa ni mtaji wa kununua dhahabu ghafi.

***99. Mheshimiwa Spika,*** kiwanda pia kimeanzisha kampuni ya *Aurun Pinnacle Company Ltd (APCL)* kwa lengo la kuwasaidia wachimbaji wadogo kuongeza uzalishaji na kukiuzia kiwanda dhahabu ghafi. Vilevile, *STAMICO* imesaini mkataba wa makubaliano wenye thamani ya dola za Marekani milioni 300 na kampuni ya *ACME* kwa ajili ya kufanya utafiti. Utafiti huo utahusisha uchorongaji katika leseni mbalimbali ili kuongeza uzalishaji wa dhahabu ghafi kwa ajili ya kiwanda hicho. Kadhalika, ili kuwezesha dhahabu iliyosafishwa kutambulika kimataifa kiwanda kinaendelea na taratibu za kupata ithibati *(ISO Accreditation).*




*Picha Na. 8: Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akizindua kiwanda cha kusafisha madini ya dhahabu cha Mwanza Precious Metals Gold Refinery kilichopo jijini Mwanza.*

## Mradi wa Dhahabu wa Buhemba

***100. Mheshimiwa Spika,*** mradi wa Buhemba ni wa ubia kati ya *STAMICO* inayomiliki hisa asilimia 35 na kampuni ya *GOODFIELD International DMCC* ya Dubai inayomiliki hisa asilimia 65 kupitia leseni ya uchimbaji madini *Na. ML 646/2021*. Mgodi uliingia makubaliano ya uchorongaji ya awamu ya kwanza na *STAMICO* (mita 4,000 kwa njia ya *RC* na mita 1,200 DD) yenye thamani ya shilingi bilioni 1.25 ili kuongeza kiasi cha mashapo. Aidha, Februari, 2022 shirika lilisaini makubaliano kwa ajili ya awamu ya pili ya uchorongaji wa mita 40,000 (mita 10,000 *DD* na mita 30,000 *RC*) katika mgodi wa Buhemba yenye thamani ya shilingi bilioni 11.5.

***101. Mheshimiwa Spika***, uanzishwaji wa mradi huo utakuwa na manufaa makubwa kwa Taifa kupitia malipo ya mrabaha na tozo mbalimbali ikiwemo ushuru wa huduma kwa Halmashauri ya Wilaya ya Butiama na ajira zaidi ya 300. Mgodi katika mwaka 2022, unatarajia kutoa kiasi cha dola za Marekani 200,000 kwa jamii inayoishi maeneo ya jirani na mgodi.

## Mgodi wa Dhahabu wa Buckreef

***102. Mheshimiwa Spika,*** shirika na mbia mwenza *TANZAM2000* wanamiliki mradi wa uchimbaji dhahabu wa *Buckreef* uliopo Mkoa wa Geita chini ya kampuni ya ubia ya *Buckreef Gold Company (BGC).* Katika ubia huu *STAMICO* inamiliki hisa asilimia 45 na mbia mwenza hisa asilimia 55. Thamani ya uwekezaji katika mradi huu ni dola za Marekani milioni 19.6. Mgodi wa *Buckreef* ulikamilisha uzalishaji wa majaribio Novemba, 2021. Kufuatia kukamilika kwa majaribio hayo, mgodi wa *Buckreef* umeanza uzalishaji mkubwa wa dhahabu kwa kutumia mtambo wenye uwezo wa kuchakata tani 15 za mbale kwa saa.

***103. Mheshimiwa Spika,*** kuanzia Novemba, 2021 hadi Machi, 2022 *Buckreef* imezalisha kilo 60.98 zenye thamani ya shilingi 7,112,327,740.68 na kulipa mrabaha na tozo nyingine Serikalini zenye jumla ya shilingi 497,862,941.85. Aidha, kwa sasa

mtambo mkubwa wenye uwezo wa kuchakata tani 30 za mbale kwa saa umefika nchini na usimikaji wake unaendelea. Usimikaji huo utakapokamilika mgodi utakuwa na uwezo wa kuchakata tani 45 za mbale kwa saa. Vilevile, shirika limeanza kutoa huduma ya uchorongaji wa miamba kwa kandarasi ya uchorongaji yenye thamani ya shilingi bilioni 4.3 ikiwa ni uendelezaji wa uchimbaji mkubwa.



*Picha Na. 9: Shughuli za Uchorongaji zikiendelea katika Mgodi wa Buckreef.*

**104. *Mheshimiwa Spika,*** mgodi pia, umelipa fidia ya shilingi 5,639,262,063.82 ambayo ni sawa na asilimia 96 ya fidia yote kwa wananchi 960 walio ndani ya eneo la mradi lenye ukubwa wa kilomita za mraba 9.4. Eneo hilo linahusisha vijiji vya Lwamgasa, Mnekezi na Lubanda. Aidha, Januari, 2022 mgodi uliingia makubaliano na Halmashauri ya Geita ya utekelezaji wa mpango wa wajibu wa kampuni kwa jamii zinazozunguka mgodi (*CSR*) wenye thamani ya shilingi 321,000,000.

**(c) Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania *(GST)***

**105. *Mheshimiwa* Spika,** kazi zilizotekelezwa na *GST* katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 ni kama ifuatavyo:

**(i) Kufanya Tafiti za Jiosayansi na Kuboresha Kanzidata ya Taifa ya Taarifa za Miamba na Madini**

**106.** ***Mheshimiwa* Spika,** *GST* ilifanya ugani wa jiolojia kwa lengo la kubaini miamba na madini yanayopatikana kwenye *QDS* 278 na 290 zilizopo kwenye Hifadhi ya Taifa ya Mwalimu Nyerere na Pori la Akiba la Selous kwenye Mikoa ya Lindi (Liwale), Morogoro (Ulanga) na Ruvuma (Tunduru na Namtumbo).



*Picha Na. 10: Wataalam wa GST wakiendelea na ugani wa jiolojia katika Pori la Akiba la Selous.*

**107.** ***Mheshimiwa Spika***, Matokeo ya utafiti huu yalibaini uwepo wa madini ya urani, chuma na *heavy minerals*. Aidha, utafiti katika eneo la *QDS* 316 ulibaini uwepo wa madini ya dhahabu katika Kijiji cha Lukwika Wilaya ya Nanyumbu na utafiti katika *QDS* 264 ulibaini uwepo wa madini ya dhahabu kwenye eneo la Lumbanga Wilaya ya Malinyi.



*Picha Na. 11: Wataalamu wa GST wakitoa mrejesho wa utafiti wa madini uliofanyika katika Wilaya ya Malinyi kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya.*

**108. *Mheshimiwa Spika,*** *GST* ilitoa ushauri elekezi *(consultancy)* wa jiosayansi kwa taasisi za Serikali kuhusu maeneo salama kwa ajili ya ujenzi wa ofisi. Taasisi za Serikali zilizofanyiwa ushauri elekezi ni pamoja na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kwenye eneo la mradi wa ujenzi Njedengwa; Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa ya Kulevya kwenye viwanja vya Njedengwa – Dodoma na Tume ya Nguvu za Atomiki kwenye eneo la Kikombo - Dodoma.

**109. *Mheshimiwa Spika,*** *GST* ilikusanya taarifa 260 kutoka kwa wamiliki wa leseni za utafiti na uchimbaji madini ambazo zinaendelea kuchakatwa. Utafiti na uhakiki wa taarifa za uwepo wa madini *(Mineral Occurrences)* katika mikoa ya Arusha, Manyara, Lindi, Mtwara na Kilimanjaro ulifanyika. Lengo la utafiti huo ni kuandaa ramani za uwepo wa madini katika kila mkoa na kuboresha kanzidata ya madini na Kitabu cha Madini Yapatikanayo Tanzania. Aidha, utafiti wa madini ya viwandani ulikamilika na jumla ya ramani 28 za kuonesha uwepo wa madini mbalimbali ya viwandani zilichorwa. Vilevile, *GST* ilifanya utafiti na kutoa ushauri elekezi kuhusu madini ya kinywe *(graphite)* katika Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa.

**(ii) Kuboresha Huduma za Maabara**

**110. *Mheshimiwa Spika,*** GST ina maabara ya kisasa ya madini ambapo imeendelea kuimarika na majibu ya uchunguzi wa sampuli zinazofanywa na maabara hiyo yanatambulika kimataifa. Katika kuimarisha huduma za maabara hiyo *GST*imeongeza wigo wa ithibati *(ISO Accreditation)* katika uchunguzi wa sampuli za dhahabu kwa njia ya uyeyushaji kwa kutumia kemikali *(Aqua Regia)* na uchunguzi wa makaa ya mawe *(ash content)* kwa njia ya utofauti wa uzito *(gravimetric)*.

**111. *Mheshimiwa Spika***, ithibati hizo zinawezesha majibu ya uchunguzi wa sampuli kupitia njia hizo kutambulika na kuaminika kimataifa. **Nitoe rai kwa watafiti na wachimbaji wa madini ya dhahabu na makaa ya mawe kutumia maabara ya *GST* ili kupata majibu yenye uhakika kwa sampuli zao**.



*Picha Na. 12: Wataalam wa GST wakifanya uchunguzi wa sampuli za miamba na udongo katika maabara*

**112.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 maabara ya *GST* imefanya uchunguzi wa jumla ya sampuli 12,525 za miamba na udongo zilizowasilishwa na wateja mbalimbali sawa na asilimia 83.5 ya lengo la mwaka. Aidha, *GST* ilitengeneza vyungu *(crucibles)* 7,930 vya kuyeyushia sampuli za miamba na udongo kwa ajili ya matumizi ya maabara yake. Pia, majaribio ya kupima ubora na uimara wa miamba *(geotechnical)*, petrolojia, jiokemia na uchenjuaji yanaendelea kufanyika kwenye sampuli zinazowasilishwa na wateja mbalimbali.

**(iii) Majanga ya Asili ya Jiolojia na Kuelimisha Wananchi Namna Bora za Kupunguza Athari za Majanga Hayo**

**113.** ***Mheshimiwa Spika,*** moja kati ya majukumu ya *GST* ni kuratibu majanga ya asili ya jiolojia kama vile matetemeko ya ardhi; milipuko ya volkano na maporomoko ya ardhi kwa lengo la kutoa ushauri wa namna bora ya kupunguza madhara yanayoweza kutokana na majanga hayo.

**114.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza jukumu hilo, *GST* ilifanya uchunguzi wa mvuke uliokuwa ukitoka ardhini katika Kijiji cha Kale, Wilaya ya Kalambo, Mkoa wa Rukwa. Matokeo ya uchunguzi huo yalibaini kuwa tukio hilo la mvuke kutoka ardhini linatokana na mabadiliko ya jiolojia

yanayosababishwa na nguvu za asili hasa kwa kuzingatia kwamba Mkoa wa Rukwa upo katika ukanda wa bonde la ufa. Baada ya uchunguzi huo, GST ilitoa taarifa kwa umma kuwa tukio hilo halikuwa na madhara yoyote.

**115. *Mheshimiwa Spika,*** *GST* ilifanya uchunguzi wa chanzo cha joto kali kutoka chini ya ardhi lililokuwa likisadikiwa kuwa ni dalili za mlipuko wa volkano ambalo lilisababisha tabaka la juu la udongo kuwaka moto katika Kijiji cha Momwe, Wilaya ya Rombo, Mkoa wa Kilimanjaro. Matokeo ya uchunguzi huo yalionesha kwamba tukio hilo halina uhusiano na mlipuko wa volkano bali ni *peat fire* iliyosababishwa na mabaki ya mimea (*biomass*) yenye uozo hafifu (*partial decomposition*) yaliyojikusanya kwa muda mrefu na kutengeneza tabaka la udongo lenye kiwango kikubwa cha oksijeni, na hivyo kuhifadhi joto linaloweza kusababisha moto kuwaka. Baada ya uchunguzi huo, *GST* ilitoa taarifa kwa umma juu ya tukio hilo na kushauri wananchi waendelee na shughuli zao kwa kuwa tukio hilo halikuwa na uhusiano na mlipuko wa volkano.

**116. *Mheshimiwa Spika,*** uchunguzi mwingine ulihusu tukio la kububujika kwa tope lililokuwa likitoka ardhini katika Kijiji cha Mpinga, Wilaya ya Bahi, Mkoa wa Dodoma. Matokeo ya uchunguzi huo yalibainisha kuwa tukio hilo lilikuwa ni mabadiliko ya jiolojia ambalo kitaalamu linajulikana kama *liquefaction.* Tukio hilo husababishwa na mabadiliko ya jiolojia ambayo husababisha kuwepo kwa msukumo au mgandamizo kwenye tabaka la udongo unaoweza kutokea kutokana na nguvu za asili kama vile matetemeko ya ardhi na kusababisha kuvurugika kwa uwiano uliopo kati ya chembechembe za udongo na maji yaliyopo kwenye nafasi wazi katikati ya udongo na hatimaye kutengenezwa kwa tope ambalo hububujika juu ya ardhi na siyo volkano kama ilivyodhaniwa kabla ya uchunguzi.

**(iv) Kuimarisha uwezo wa Taasisi na Kusogeza Huduma kwa Wananchi**

**117. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utekelezaji wa majukumu yake, *GST* imefungua ofisi ndogo katika mkoa wa Geita kwa lengo la kusogeza huduma za taasisi karibu na

wadau. Hatua hii ni ya kihistoria kwa kuwa *GST* haikuwahi kuwa na ofisi nje ya Dodoma tangu kuanzishwa kwake mwaka 1925. Ofisi zitaendelea kufunguliwa katika maeneo mengine kulingana na upatikanaji wa rasilimaliwatu na fedha.



*Picha Na. 13: Mhe. Dkt. Doto M. Biteko (Mb.) Waziri wa Madini akiwa kwenye picha ya pamoja na viongozi na wadau mbalimbali katika uzinduzi wa ofisi za GST – Geita.*


**118. *Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha utekelezaji wa majukumu yake, *GST* imenunua mashine na vifaa vya maabara ikiwemo mashine kubwa ya kisasa ya kuzalisha vyungu vya kuyeyushia sampuli za dhahabu (*crucibles*). Mashine hiyo itaiwezesha *GST* kuwa mzalishaji mkubwa pekee wa vyungu hivyo Afrika Mashariki na Kati. Uzalishaji huo utakapoanza, *GST* itaongeza mapato yake kwa kuuza vyungu hivyo ndani na nje ya nchi. Picha Na. 14 inaonesha mashine ya kisasa ya utengenezaji wa vyungu hivyo.




*Picha Na. 14: Mashine ya kisasa ya kutengeneza vyungu (crucibles) vya kuyeyushia sampuli za miamba na udongo.*

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** *GST* imenunua tanuru kubwa la kisasa la uchunguzi wa sampuli za dhahabu lenye uwezo wa kuchunguza sampuli 50 kwa mkupuo mmoja na hivyo kuhudumia wateja wengi zaidi kwa muda mfupi. Picha Na. 15 ni tanuru lilionunuliwa kwa ajili ya kuyeyushia sampuli. Aidha, *GST* imenunua mashine mbalimbali za uchunguzi ikiwemo *XRD* kwa ajili ya uchunguzi wa sampuli za udongo, madini na madawa; na mashine aina ya *magnetometer* zinazotumika katika tafiti za madini ambazo zitaongeza uwezo wa taasisi kuwahudumia wadau wengi zaidi hasa wachimbaji wadogo wa madini na kutatua changamoto za uchimbaji madini wa kubahatisha. Aidha, *GST* imenunua magari manne (4) mapya kwa ajili ya kuimarisha kazi za ugani.

**120.**
***Mheshimiwa Spika,*** *GST* imetoa ushauri elekezi kwa kampuni ya uchimbaji wa kati wa madini ya dhahabu ya *MMG* iliyopo Mkoa wa Mara. Utafiti huo ulibaini uwepo wa mkondo unaobeba dhahabu. Pia, ushauri elekezi ulitolewa kwa wachimbaji wadogo wa eneo la Pemba Wilaya ya Mvomero. Matokeo ya utafiti huo yalibaini uwepo wa madini ya dhahabu.



*Picha Na. 15: Tanuru la kisasa la kufanyia uchunguzi wa sampuli za miamba na udongo.*

**(d) Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia *(TEITI)***

**121.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza jukumu lake la msingi la kuhamasisha uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali madini, mafuta na gesi asilia, *TEITI* imeendelea kutoa kwa umma taarifa zake kwa kila mwaka. Tarehe 30 Juni, 2021, Kamati ya *TEITI* ilikamilisha na kuweka wazi kwa umma Ripoti ya 11 ya *TEITI* kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Pamoja na mambo mengine ripoti hii iliainisha mapato yaliyopokelewa na Serikali kiasi cha shilingi bilioni 623.2 na malipo ya kampuni kwa Serikali kiasi cha shilingi bilioni 626.1. Mapato hayo ni kutoka kwenye kampuni 41 zilizofanyiwa ulinganishi ambapo kampuni 22 zilikuwa za madini; kampuni 7 za gesi asilia na mafuta; na kampuni 12 ni zilizotoa huduma katika Sekta ya Madini, Mafuta na Gesi Asilia.

**122.** ***Mheshimiwa Spika***, kati ya shilingi bilioni 623.2 ambazo Serikali ilikiri kupokea, asilimia 42.75 zilipokelewa na Tume ya Madini, asilimia 38.97 na Mamlaka ya Mapato Tanzania na asilimia 15.41 zilipokelewa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania. Kiasi kilichobaki sawa na asilimia 2.88 kilipokelewa na Mamlaka nyingine ambazo ni Mamlaka za Serikali za Mitaa (asilimia 2.26), Msajili wa Hazina (asilimia 0.56) na Wakala wa Misitu (asilimia 0.06).

**123.** ***Mheshimiwa Spika***, tofauti kati ya malipo na mapato ni shilingi bilioni 2.97pungufu ya kiasi ambacho Serikali ilikiri kupokea kutoka kwa kampuni hizo. Tofauti hiyo ni asilimia 0.48 ikiwa ni chini ya asilimia 1 ya mapato hayo ambayo kwa mujibu wa Sheria ya *TEITA*, 2015 kiwango cha tofauti hiyo siyo lazima kufanyiwa ukaguzi na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)*. Hata hivyo, Kamati ya *TEITI* ina uwezo wa kisheria wa kufanya uamuzi kuwa ukaguzi wa tofauti hiyo ufanyike.

**124.** ***Mheshimiwa Spika***, ripoti hiyo pia iliweka wazi taarifa mbalimbali zikiwemo za uzalishaji na usafirishaji wa rasilimali madini, mafuta na gesi asilia; umiliki wa hisa; na taarifa za ushirikishwaji wa watanzania *(Local Content)*. Taarifa hiyo

ilibainisha kuwa Sekta ya Madini ilichangia asilimia 67.54, Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia asilimia 28.43 na kampuni zilizotoa huduma kwenye Sekta ya Uziduaji asilimia 4.03 ya mapato ya Serikali kwa kampuni 41 zilizofanyiwa ulinganisho. Aidha, taarifa iliainisha thamani ya madini yaliyozalishwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 kuwa ni shilingi trilioni 4.7. Thamani hiyo ilikuwa ni ongezeko la asilimia 27 ikilinganishwa na shilingi trilioni 3.7 za Mwaka wa Fedha 2017/2018. Sehemu kubwa ya uzalishaji huo ilitokana na madini ya dhahabu ambayo yalikuwa ni asilimia 71.9 ya thamani ya madini yote yaliyozalishwa.

**125. *Mheshimiwa Spika***, *TEITI* imebuni na kuanzisha njia mbadala ya kuhakikisha takwimu na taarifa zinawafikia wadau kiurahisi kupitia mfumo wa kieletroniki. Takwimu hizo huwekwa kupitia kwenye *dashboard* iliyopo katika tovuti ya *TEITI* kwa kutumia vielelezo mbalimbali ikiwemo chati na grafu. Hadi Julai, 2021, takwimu na taarifa zilizopo katika Ripoti ya 11 ya *TEITI* zimeingizwa katika mfumo huo ambao unapatikana kupitia *https://www.teiti.go.tz/dashboard/*.

**126. *Mheshimiwa Spika***, *TEITI* imeendelea kuhamasisha na kuelimisha umma kuhusu matumizi ya takwimu zinazopatikana katika ripoti zake kwa njia mbalimbali ikiwemo maonesho, makongamano, warsha, mafunzo, semina, vyombo vya habari na mitandao ya kijamii. Uelimishaji huo umejenga uwezo wa taasisi na wananchi kwa ujumla kuhoji na kuhamasisha mijadala kuhusu manufaa ya uchimbaji wa rasilimali madini, mafuta na gesi asilia.

**(e) Kituo cha Jemolojia Tanzania *(TGC)***

**127. *Mheshimiwa Spika,*** *TGC* hutoa mafunzo ya utambuzi, usanifu, ukataji na ung'arishaji wa madini ya vito. Mafunzo hayo ni ya muda mrefu katika fani za teknolojia ya madini na usonara *(gem and jewellery technology)* kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada; na mafunzo ya muda mfupi katika fani za *gemology, gem identification, synthetic and treated gem identification, coloured gem grading and pricing, diamond* grading *and pricing, lapidary, gem and rock carving and jewellery design and manufacturing*.

**128. *Mheshimiwa Spika,*** *TGC* hutoa huduma za usanifu madini ya vito na miamba, huduma za maabara kwa madini ya vito na bidhaa za usonara na kutoa vyeti vya uthibitisho *(*Certificate *of Authenticity)*. Aidha, *TGC* hutengeneza bidhaa za mapambo na urembo. Pia, *TGC* hutoa ushauri elekezi kwenye tafiti za uongezaji thamani madini na kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini nchini na matumizi ya bidhaa zinazotokana na madini ya vito.

**129. *Mheshimiwa Spika***, kuanzia Julai, 2021 hadi Machi, 2022, *TGC* imedahili wanafunzi 95 kwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya stashahada (*NTA Level* 4, *NTA Level* 5 na *NTA Level* 6) katika fani ya teknolojia ya madini na usonara. Aidha, wanafunzi 43 walidahiliwa kujiunga na mafunzo ya muda mfupi (miezi sita na mitatu) katika ngazi ya astashahada kwa fani za utambuzi wa madini, ukataji na usanifu madini ya vito.

**130. *Mheshimiwa Spika***, ili kuhakikisha wanafunzi wanaosoma *TGC* wanapata elimu stahiki, *TGC* iliratibu mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi 73 katika fani ya teknolojia ya madini na usonara ambayo yalifanyika Arusha *Gemological Laboratory* na katika ofisi za madini za Mikoa ya Arusha, Dar es salaam, Shinyanga, Mirerani-Manyara. Aidha, wanafunzi wa fani ya ukataji na ung'arishaji wa madini ya vito walipatiwa mafunzo kwa vitendo katika kampuni zinazojishughulisha na uongezaji thamani madini ya vito kwenye miji ya Arusha, Dar es Salaam na Mirerani.

**131. *Mheshimiwa Spika***, pamoja na kutoa elimu na huduma za ushauri, *TGC* inazalisha na kuuza bidhaa mbalimbali zikiwemo vinyago, bidhaa za usonara kama vile vidani, *key holders*, mikufu, bangili, pete, na vito vilivyokatwa. Bidhaa hizi zinapatikana kwenye ofisi za *TGC* zilizoko Arusha na kwenye mabanda ya *TGC* yanayokuwa kwenye maonesho mbalimbali. Aidha, *TGC* inatengeneza bidhaa hizo kwa mujibu wa mahitaji ya mteja. **Ni wito wangu kwa watanzania wenzangu na taasisi za umma pale tunapohitaji bidhaa za zawadi au kumbukumbu *(souvenir)* kununua bidhaa zinazozalishwa na *TGC*.** Baadhi ya bidhaa zinazozalishwa na *TGC* ni kama zinavyoonekana katika Picha Na. 16.

*Picha Na. 16: Baadhi ya bidhaa zinazozalishwa na kuuzwa na TGC.*

**132. *Mheshimiwa Spika*,** *TGC* imeendelea kujitangaza na kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini kwa kushiriki katika Maonesho ya Kitaifa na Kimataifa ya Sabasaba ya mwaka 2021 na *SADC* yaliyofanyika jijini Dar es Salaam, ... za Uhuru wa ... utano wa Nne ... anyika Dar es ... wadau kuhusu ... i.




*Picha Na. 17: Mhe Waziri wa Madini Dkt. Doto Biteko alipotembelea banda la TGC wakati wa Maonesho ya Sabasaba - Dar es Salaam 2021.*

## D. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2022/2023

**133*. Mheshimiwa Spika,*** katika kuandaa Mpango na Bajeti wa Mwaka wa Fedha 2022/23, Wizara imezingatia miongozo mbalimbali ya kitaifa. Miongozo iliyozingatiwa ni pamoja na: Mwongozo wa Kitaifa wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti wa Mwaka 2022/2023; Ilani ya CCM kwa Ajili ya Uchaguzi wa Mwaka 2020; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26; Sera ya Madini ya Mwaka 2009; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Maelekezo ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na viongozi wengine wa kitaifa waliyoyatoa kwa nyakati tofauti; na Maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini yaliyotolewa kwa nyakati tofauti.

### I. Vipaumbele vya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**134. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Madini kwa mwaka 2022/2023 itatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo: kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa; kuwaendeleza wachimbaji wadogo na kuwawezesha wananchi kushiriki katika uchumi wa madini; kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini; kuhamasisha biashara na uwekezaji katika Sekta ya Madini; kusimamia mfumo wa ukaguzi wa shughuli za migodi; kuzijengea uwezo taasisi zilizo chini ya Wizara ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi; na kuendeleza rasilimaliwatu na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi.

#### a) Kuimarisha Ukusanyaji wa Maduhuli na Kuongeza Mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa

**135. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali, Wizara imepanga kutekeleza mikakati ifuatayo: kuimarisha udhibiti na usimamizi wa uchimbaji mkubwa na wa kati wa madini ili uweze kufaidisha Taifa na wawekezaji kwa usawa; kutekeleza mikakati itakayowezesha

kudhibiti vitendo vya utoroshaji wa madini kwenda nje ya nchi na biashara haramu ya madini nchini; kuimarisha masoko ya madini nchini; na kuanzisha na kuimarisha soko la dhahabu la Kalema, Mkoa wa Katavi.

**136.** ***Mheshimiwa Spika,*** mikakati mingine itakayotekelezwa ni: kufungua na kusimamia migodi ya uchimbaji mkubwa na kuweka msisitizo katika uchimbaji wa madini ya kinywe *(graphite)* na madini mengine; kuendeleza na kuimarisha usimamizi wa madini ya ujenzi, soko la Tanzanite na vito vingine hapa nchini ili kuongeza mapato yatokanayo na madini hayo na madini mengine ya vito; kuhakikisha migodi yote mikubwa inaajiri watanzania na kununua huduma na bidhaa kutoka hapa nchini kwa kiwango cha kuridhisha kwa kadiri ya upatikanaji wake; na kutoa huduma za kijamii katika maeneo husika.

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia mikakati hiyo, Wizara, katika mwaka 2022/2023, inapanga kukusanya jumla ya shilingi bilioni 894.3. Kiasi hiki ni ongezeko la asilimia 22.12 ikilinganishwa na shilingi bilioni 696.4 zilizopangwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Kati ya fedha zitakazokusanywa, shilingi bilioni 822.0, sawa na asilimia 91.9 zitakusanywa na kuwasilishwa Hazina na shilingi bilioni 72.3, sawa na asilimia 8.1 zitakusanywa na kutumika na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

**b) Kuwaendeleza Wachimbaji Wadogo na Kuwawezesha Wananchi Kushiriki katika Uchumi wa Madini**

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza kipaumbele hiki, Wizara itafanya yafuatayo: kubuni na kuimarisha utekelezaji wa mipango ya kuwawezesha wachimbaji wadogo ili waweze kufanya shughuli zao kwa tija kwa kuwatengea maeneo au kuwapatia leseni kwenye maeneo ambayo yana taarifa za msingi za kijiolojia; kutoa huduma za utafiti kwa gharama nafuu; kuwaendeleza wachimbaji wadogo kuwa wa kati na hatimaye kuwa wachimbaji wakubwa; kuwapa mafunzo yanayohitajika kuhusu uchimbaji, uchenjuaji na biashara ya madini; kuzifuta leseni ambazo hazijaendelezwa kwa mujibu wa sheria na maeneo ya leseni hizo kutolewa

kwa wachimbaji wengine, hususan wachimbaji wadogo; na kusimamia utekelezaji wa sheria inayoitaka migodi yote mikubwa kuajiri, kununua huduma na bidhaa kutoka hapa nchini na kuwasilisha mpango wa ushirikishwaji wa watanzania katika mnyororo wa uchumi wa Madini *(Local Content).*

**c) Kuhamasisha Shughuli za Uongezaji Thamani Madini**

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani, Wizara itaendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya uchenjuaji, uyeyushaji, usafishaji na utengenezaji wa bidhaa za madini; na kusimamia na kuhamasisha uwekezaji katika shughuli za uongezaji thamani madini.

**d) Kuhamasisha Biashara na Uwekezaji katika Sekta ya Madini**

**140.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza kipaumbele hiki, Wizara itafanya yafuatayo: kuweka mazingira yatakayohamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini bila ya kuathiri ustawi na matarajio ya nchi kutokana na uwekezaji huo; kubuni na kutekeleza mikakati ya kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini kwa kufanya tafiti za madini ya kimkakati, madini ya viwandani na madini ya metali; kujenga imani kwa biashara ya madini nchini kwenye uwanja wa kimataifa kwa kutekeleza wajibu wa nchi yetu kama mwanachama wa *Extractive Industries Transparency Initiative (EITI)*; na kushiriki mikutano, maonesho ya madini na makongamano mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa lengo la kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo katika Sekta ya Madini.

**e) Kusimamia Mfumo wa Ukaguzi wa Shughuli za Migodi**

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza kipaumbele hiki, Wizara itaimarisha kaguzi katika masuala ya afya, usalama na utunzaji wa mazingira kwa lengo la kudhibiti athari za

kiafya, kiusalama na kimazingira zinazoweza kujitokeza katika shughuli za utafiti, uchimbaji na uchenjuaji wa madini. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha ukaguzi wa uzalishaji wa madini, hesabu za uwekezaji ikiwa ni kiasi cha mitaji na gharama za uendeshaji *(Capex and Opex)* pamoja na ulinganifu wa malipo ya kodi na tozo kwenye shughuli za madini ili kuhakikisha nchi inapata mapato stahiki.

**f) Kuzijengea uwezo Taasisi Zilizo Chini ya Wizara ili Ziweze Kutekeleza Majukumu yake kwa Ufanisi**

**142. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara itatekeleza kipaumbele hiki kwa kufanya yafuatayo: kuendelea kuimarisha Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*) ili lishiriki kikamilifu kwenye shughuli za madini; kuiimarisha Tume ya Madini ili iendelee kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kukusanya maduhuli na takwimu za madini kwa lengo la kuongeza mapato ya Serikali; kuimarisha *GST* ili iendelee kufanya utafiti mkubwa wa shughuli za madini na kuendana na mabadiliko ya teknolojia; kuimarisha *TGC* ili iendelee kutoa mafunzo ya uongezaji thamani madini na kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini nchini; na kuiimarisha *TEITI* kwa lengo la kuendeleza uwazi na uwajibikaji katika sekta ya uziduaji.

**143. *Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza kipaumbele hiki, Wizara itafanya yafuatayo: kuajiri watumishi wenye sifa na ujuzi unaostahili; kuboresha mazingira ya kufanyia kazi; kuwawezesha watumishi kupata mafunzo ya muda mrefu na mfupi; kuboresha maslahi na stahili za watumishi; kutoa elimu na vifaa kinga kwa ajili ya kuzuia maambukizi mapya ya VVU na kuwahudumia watumishi waliothibitika wanaishi na VVU waliojitokeza; kuendelea kutoa elimu, ushauri na huduma dhidi ya Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY); kuendelea kukabiliana na janga la UVIKO 19; na kuendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Wizara dhidi ya Rushwa wa Mwaka 2017 - 2022.

## II. Kazi Zitakazotekelezwa na Taasisi Zilizo Chini ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

### (a) Tume ya Madini

#### Kuimarisha Usimamizi wa Sekta ya Madini na Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali

**144.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2022/2023, Tume itaendelea kuboresha ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na rasilimali madini nchini kwa kufanya yafuatayo: kusimamia uzalishaji wa madini ujenzi kwa kuhakikisha Mfumo wa Ukusanyaji wa Maduhuli yatokanayo na Madini (*MiMS*) unafanya kazi kikamilifu nchi nzima; kuongeza kasi ya utoaji wa leseni kwa kuimarisha mfumo wa utoaji na usimamizi wa leseni; kugawa maeneo yaliyotengwa kwa wachimbaji wadogo ili wafanye uzalishaji; kuendelea kufuta leseni zote zisizoendelezwa na zilizoisha muda wake ili maeneo hayo yatolewe kwa wachimbaji wengine; kuendelea kutatua migogoro katika maeneo mbalimbali; kuboresha huduma katika masoko ya madini nchini; kudhibiti mianya ya utoroshaji wa madini kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali; na kuendelea kusajili mialo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu nchini.

#### Kuimarisha Ufuatiliaji na Ukaguzi wa Usalama, Afya, Mazingira na Uzalishaji wa Madini kwa

#### Wamiliki wa Leseni

**145.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuwa na uchimbaji madini salama, endelevu na unaozingatia utunzaji wa mazingira, Tume ya Madini itaendelea kufanya kaguzi za kimazingira ikiwa ni pamoja na ukaguzi wa miundombinu ya migodi kama vile mabwawa ya kuhifadhia topesumu, mashimo ya uchimbaji, maeneo ya kutunzia miambataka; maghala na stoo za kuhifadhia baruti, shughuli za ukarabati wa mazingira migodini, uchimbaji salama hususan kwa wachimbaji wadogo pamoja na ukaguzi wa mitambo ya uchenjuaji madini. Aidha, Tume itaendelea kusimamia utekelezaji wa

mipango ya uendelezaji migodi na ufungaji migodi kwa wamiliki wa leseni kubwa na za kati; na kubuni miradi ya mfano ya uchimbaji madini salama na utunzaji wa mazingira kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

**Kuendelea Kuboresha Mazingira ya Kuwawezesha Wananchi Kufaidika na Rasilimali Madini**

**146. *Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Madini itaendelea kutenga na kugawa maeneo kwa wachimbaji wadogo nchini, kusimamia ushirikishwaji wa wananchi (*Local Content*) kwenye shughuli za madini kwa mujibu wa Sheria, kuhakikisha kampuni za uwekezaji katika Sekta ya Madini zinatumia malighafi zinazozalishwa nchini pamoja na huduma zinazotolewa na watanzania, na kusimamia utekelezaji wa miradi ya *CSR*.

**Kuelimisha Umma na Kuboresha Upatikanaji wa Taarifa Mbalimbali kwa Wadau wa Sekta ya Madini**

**147. *Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Madini itaendelea kutoa taarifa na elimu kwa umma kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu Sekta ya Madini ikiwa ni pamoja na Sheria na Kanuni mbalimbali za usimamizi wa shughuli za utafutaji, uchimbaji, biashara ya madini, utunzaji wa mazingira na ulipaji wa kodi na tozo. Utoaji wa elimu husika na uhamasishaji utafanyika kupitia vyombo vya habari, semina, tovuti ya Tume ya Madini (*www.tumemadini.go.tz*), maonesho, makongamano pamoja na midahalo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

**Kuboresha Ushirikiano Kati ya Tume ya Madini na Wadau Mbalimbali katika Uendelezaji wa Sekta ya Madini**

**148. *Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha ushirikiano na wadau wengine, Tume ya Madini itaendelea kuzihusisha mamlaka nyingine za Serikali zinazofungamana na sekta katika utekelezaji wa majukumu ikiwa ni pamoja na Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (*NEMC*), Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (*TASAC*), Mamlaka ya Mapato

Tanzania (*TRA*), Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)*, Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini *(TARURA)*, Taasisi za Fedha, pamoja na wadau wengine wa ndani na nje ya nchi ili kuhakikisha changamoto mbalimbali zikiwemo za kisheria, mitaji, upatikanaji wa vibali, tozo na kodi ambazo zimekuwa zikiwakabili wachimbaji nchini zinatatuliwa kwa wakati na kwa maridhiano.

**Kuendeleza Rasilimaliwatu na Kuboresha Mazingira ya Kufanyia Kazi**

**149. *Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Madini itaendelea kuimarisha utendaji kazi wake kwa lengo la kuisimamia ipasavyo Sekta ya Madini nchini kwa kuboresha mazingira na vitendea kazi na kuwaongezea ujuzi na weledi watumishi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu ili kuimarisha utendaji kazi wa Tume.

**(b) Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST)**

**150. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2022/2023, Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) inatarajia kutekeleza shughuli zifuatazo:

**Kufanya Tafiti za Jiosayansi na Kuboresha Kanzidata ya Taifa ya Taarifa za Miamba na Madini.**

**151. *Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza kipaumbele hicho *GST* itafanya yafuatayo: utafiti wa jiolojia na jiokemia katika *QDS* mbili (2) mpya (203 na 204) zilizopo mikoa ya Pwani na Dar es Salaam; kuhuisha ramani katika *QDS* 175 (Njombe) na 176 (Ruvuma) katika skeli ya 1:100,000; kufanya tafiti maalum tano (5) za jiosayansi; tafiti tano (5) za kina kwenye madini ya viwandani, *helium*, vito, dhahabu na madini ya kimkakati kama vile nikeli *(nickel)* na kinywe *(graphite)*; kutoa ushauri elekezi; kuhamisha mfumo wa utunzaji taarifa kutoka mfumo wa nakala mango kwenda tepe *(digitization)*; kukusanya na kufanya uchambuzi wa taarifa za utafutaji na uchimbaji madini nchini; kuhuisha kanzidata ya rasilimali madini zinazopatikana nchini na kitabu cha Madini Yapatikanayo Tanzania.

**Kuwaendeleza Wachimbaji Wadogo kwa Kufanya Tafiti za Jiosayansi**

**152.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuwaendeleza wachimbaji wadogo na wa kati wa madini, *GST* itafanya utafiti wa jiosayansi na kutoa mafunzo kwa lengo la kutambua tabia za mbale katika maeneo mawili (2) ya wachimbaji wadogo yaliyopo Mikoa ya Morogoro na Iringa. Aidha, *GST* kwa kushirikiana na *STAMICO*, itafanya utafiti wa jiosayansi kwa lengo la kubaini uwepo wa madini katika eneo moja (1) lililotengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

**Kuboresha Huduma za Maabara**

**153.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha huduma za maabara, *GST* itafanya yafuatayo: kufanya uchunguzi kwa kuzingatia matakwa ya ithibati *(accreditation)*; kuboresha maabara ya Geita na kuanzisha maabara Chunya kwa lengo la kusogeza huduma karibu na wachimbaji na watafutaji wa madini; kutengeneza vyungu vya kuyeyushia sampuli *(crucibles)* 300,000 na *cupels* 50,000 kwa ajili ya kuyeyusha dhahabu; kufanya uchunguzi wa sampuli za udongo, miamba au madini 17,000; kuandaa sampuli rejea *(reference materials)* za dhahabu, shaba, *silver*, zinki, chuma na *cobalt*; na kufanya ukarabati wa mashine ya kupimia sampuli (*Induced Coupled Plasma - ICP)*.

**Kuratibu Taarifa za Majanga ya Asili ya Jiolojia na Kuelimisha Wananchi Namna Bora ya Kujikinga nayo**

**154.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na majanga ya asili ya jiolojia kama vile matetemeko ya ardhi, maporomoko ya ardhi, na milipuko ya volkano, GST inakusudia kufanya mambo yafuatayo: kukusanya takwimu kutoka vituo vitano (5) vya kudumu vya kupimia matetemeko ya ardhi vilivyoko Arusha, Dodoma, Geita, Mtwara na Mbeya ili kujua matukio mbalimbali ya mitetemo; kuchakata takwimu zilizokusanywa kutoka katika vituo hivyo na kuhuisha ramani inayoonesha vitovu vya matetemeko ya ardhi nchini; kuunganisha vituo viwili (2) vya kupimia mitetemo vilivyopo Dodoma na Arusha katika mfumo mubashara *(real time)*; kutoa elimu kwa Umma

juu ya namna bora ya kujikinga au kupunguza athari za majanga ya asili ya jiolojia; na kusimika kituo kimoja kipya mkoani Kigoma cha kuratibu ukanda wa Bonde la Ufa Mkondo wa Magharibi.

**Kuimarisha Uwezo wa Taasisi katika Kutoa Huduma**

**155. *Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha uwezo wa Taasisi katika kutoa huduma, *GST* inakusudia kufanya yafuatayo: kuboresha mifumo ya uchakataji, uhifadhi na usambazaji wa taarifa za jiosayansi kuhusu upatikanaji wa madini; kuwawezesha watumishi kupata mafunzo ya muda mfupi na mrefu; kuboresha mazingira ya utendaji kazi na maslahi ya watumishi; kutangaza *(marketing)* bidhaa na huduma zitolewazo na *GST*; na kukamilisha kufanya mapitio na maboresho ya Muundo wa Taasisi ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya *GST*.

**(c) Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*)**

**156. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2022/2023, *STAMICO* inatarajia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:

**Kuongeza Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ya Shirika hadi Kufikia Shilingi Bilioni 70**

**157. *Mheshimiwa Spika*,** ili kufikia lengo hilo shirika litatekeleza kazi zifuatazo: kuendelea kutangaza huduma za uchorongaji zinazofaywa na shirika; kuanza uzalishaji wa kibiashara katika mradi wa makaa ya mawe ya kupikia (*coal briquettes)*; kuendelea na mradi wa kuuza vilipuzi na kemikali za madini; na kusimamia miradi ya uwekezaji.

**Kuendelea na Uzalishaji Mkubwa katika Eneo la Kabulo-Kiwira**

**158. *Mheshimiwa Spika*,** katika kutekeleza kipaumbele hicho, shirika litafanya kazi zifuatazo: kukamilisha ukarabati wa miundombinu ya migodi ikiwemo reli na barabara; kununua vifaa vya uchimbaji ili kuongeza ufanisi wa mradi; kufanya

utafiti ili kuongeza mashapo yanayotarajiwa kuchimbwa; pamoja na kutafuta masoko makubwa ndani na nje ya nchi.

**Kuendeleza na Kuongeza Uzalishaji wa Makaa ya Kupikia *(Coal briquettes)***

**159. *Mheshimiwa Spika*,** katika kutekeleza kipaumbele hicho, shirika litafanya kazi zifuatazo: kuanza uzalishaji kwa kutumia mitambo miwili mikubwa yenye uwezo wa kuzalisha tani 20 kwa saa itakayosimikwa Pwani na Kabulo; na kununua mitambo miwili mingine mikubwa yenye uwezo wa kuzalisha tani 20 kwa saa kwa kila mtambo ambapo mmoja utasimikwa Dodoma kwa ajili ya kanda ya kati na mwingine utasimikwa katika eneo litakaloonekana lina uhitaji wa nishati hiyo; na kufanya kampeni ya uhamasishaji wa matumizi ya nishati hiyo.

**Kuimarisha Shughuli za Uchorongaji**

**160. *Mheshimiwa Spika*,** katika kutekeleza kipaumbele hicho, shirika litafanya kazi zifuatazo: kuendelea kuzitangaza shughuli za uchorongaji zinazofanywa na shirika; kutafuta kandarasi nyingine mpya; na kununua mitambo ya uchorongaji *(rigs)*, magari saidizi *(supporting vehicle)*, *low bed vehicle*, magari manne (4) na *water bowser*.

**Kuratibu Shughuli za Uchimbaji Mdogo na Kuimarisha Vituo vya Mfano**

**161. *Mheshimiwa Spika*,** katika kutekeleza kipaumbele hicho, shirika litafanya kazi zifuatazo: kuendelea kutekeleza mkakati wa kuendeleza uchimbaji mdogo nchini pamoja na mpango wa mafunzo kwa wachimbaji wadogo nchi nzima; kununua mitambo mitano (5) ya uchorongaji maalum kwa ajili ya wachimbaji wadogo *(Shallow Holes Drilling Rigs – DD/RC 0-100 Meters)*; kuongeza uwezo wa vituo vya mfano vilivyopo Lwamgasa, Katente na Itumbi kwa kuimarisha miundombinu iliyopo; kuanza ujenzi wa vituo viwili vipya vya mfano katika Mkoa wa Tanga (chokaa) na Lindi (chumvi); na kuwasaida wachimbaji wadogo kupata mikopo kutoka taasisi za kifedha.

**Kuendeleza Mali na Leseni za Shirika**

**162.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika kutekeleza kipaumbele hicho, shirika litafanya kazi zifuatazo: kuendeleza leseni za madini mbalimbali zinazomilikiwa na shirika; na kuanzisha mgodi wa kuchimba dhahabu wa Kigosi kwa kuanza uchorongaji na utafiti kwa ajili ya kuhakiki mashapo yaliyopo.

**Kuendelea Kutoa Elimu Juu ya Afya na Utawala Bora**

**163.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika kutekeleza kipaumbele hicho, shirika litafanya kazi zifuatazo: Kutoa mafunzo mbalimbali kwa watumishi juu ya maambukizi ya VVU, UVIKO - 19 pamoja na Magonjwa Sugu Yasiyoambikiza; kutoa huduma za lishe kwa wafanyakazi wenye maambukizi ya VVU; kutoa elimu katika masuala ya rushwa, maadili na utawala bora kwa watumishi; na kuandaa michezo mbalimbali ili kuhamasisha wafanyakazi kujijengea afya bora.

**Kuboresha Mazingira ya Kazi kwa Watumishi**

**164.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika kutekeleza kipaumbele hicho, shirika litafanya kazi zifuatazo: kulipa madeni ya wafanyakazi; kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi; kuwapatia watumishi vitendea kazi; na kujenga jengo la ofisi ya shirika Dodoma.

**(d) Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI)**

**165*. Mheshimiwa Spika*,** kazi zitakazotekelezwa na *TEITI* katika mwaka 2022/2023 ni kama ifuatavyo: kukamilisha na kutoa kwa umma ripoti ya malipo ya kodi na tozo yaliyofanywa na Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia kwa Serikali kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2020/2021; kuendelea kuelimisha umma juu ya matumizi ya takwimu zinazotolewa kwenye ripoti za *TEITI* ili kuhoji uwajibikaji wa Serikali; kuendelea kuelimisha kampuni za madini, mafuta na gesi asilia juu ya majukumu yao ya kuweka wazi majina ya wamiliki wa hisa kwa ajili ya kuanzisha Rejista ya Taarifa; kujumuisha taarifa za

wachimbaji wadogo na fidia zilizolipwa kutokana na athari za mazingira katika ripoti za *TEITI*; na kuendelea kutekeleza vigezo vya *EITI* vya kuweka wazi mikataba *(Contract Disclosure)* na kuandaa Rejista ya uwekaji wazi wa majina ya wamiliki wa hisa katika kampuni za madini, mafuta na gesi asilia *(beneficial ownership disclosure)*.

### (e) Kituo cha Jemolojia Tanzania (*TGC*)

**166. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Kituo cha Jemolojia Tanzania kinatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:

#### (i) Kuendelea kutoa mafunzo

**167. *Mheshimiwa Spika,*** *TGC* katika kutekeleza kipaumbele hicho itafanya yafuatayo: kuendelea kutoa mafunzo ya ngazi ya stashahada katika teknolojia ya vito na usonara *(Gem and Jewellery Technology)*; kuanzisha mafunzo ya astashada ngazi ya *VETA* katika fani za ukataji, ung'arishaji madini ya vito na uchongaji vinyago; kutoa mafunzo ya muda mfupi (mwezi 1 hadi 6) katika fani za utambuzi wa madini ya vito, usonara, utengenezaji wa vinyago vya miamba na vito na usanifu madini ya vito; itahamasisha kuhusu uongezaji thamani madini ya vito katika shule za msingi na sekondari; kuanzisha karakana za uchakataji madini; kutoa semina elekezi mbalimbali ikiwemo kujikinga na maambukizi ya VVU na magonjwa Yasiyoambukizwa kwa watumishi na wanafunzi na kuzuia vitendo vya rushwa na ufisadi kwa watumishi na wanafunzi.

#### (ii)Uzalishaji wa bidhaa

**168. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kituo kimepanga kuongeza uzalishaji wa bidhaa mbalimbali zitokanazo na madini ya vito na miamba zikiwemo vinyago, mikufu, hereni na bidhaa nyingine za urembo na mapambo zitokanazo na rasilimali madini.

**(iii) Kuimarisha Shughuli za *TGC***

**169. *Mheshimiwa Spika*,** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, *TGC* imetengewa fedha za maendeleo kwa ajili ya mradi wa upanuzi wa miundombinu mbalimbali ya kutolea mafunzo ikiwemo karakana za mafunzo na uchakataji madini, madarasa, maabara za madini ya vito na bidhaa za usonara, maktaba, mabweni na kantini. Kituo pia, kimepanga kufanya ununuzi wa magari manne (4), mitambo ya kuchakata madini na vifaa mbalimbali kwa ajili ya mafunzo. Aidha, Kituo kimepanga kuendelea kuwajengea uwezo watumishi kwa kuwapeleka kwenye mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi hususan katika nchi zilizobobea kwenye teknolojia za uongezaji thamani madini zikiwemo Thailand, India, Sri Lanka, Marekani na China.

**E. SHUKRANI**

**170. *Mheshimiwa Spika,*** kwa dhati kabisa nipende kukiri kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imeonesha juhudi kubwa katika kuhakikisha kuwa uchumi wa nchi yetu unaimarika. Ni imani yangu kuwa kwa kasi kubwa ya utendaji kazi anayoendelea nayo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, nchi yetu itaendelea kupiga hatua katika kuimarisha ustawi wa kila mtanzania na taifa kwa ujumla.

**171. *Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii pia kumshukuru Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, kwa maelekezo na miongozo mbalimbali katika kusimamia utendaji wa shughuli mbalimbali kwa manufaa ya watanzania wote. Aidha, nimshukuru Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) kwa hotuba yake nzuri ya bajeti ambayo imetoa mwelekeo wa shughuli za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**172. *Mheshimiwa Spika,*** kipekee nitumie fursa hii kumshukuru Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo

Kiruswa (Mb.) kwa namna anavyonipa ushirikiano katika kusimamia Sekta ya Madini. Amekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kuwa Sekta ya Madini inakuwa na tija.

**173. *Mheshimiwa Spika,*** kwa dhati kabisa niwashukuru Bw. Adolf Hyasinth Ndunguru, Katibu Mkuu, na Bw. Msafiri Lameck Mbibo, Naibu Katibu Mkuu kwa namna wanavyosimamia vyema utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, niwashukuru Dkt. Abdulrahman Shabani Mwanga, Kamishna wa Madini, Profesa Idris Suleiman Kikula, Mwenyekiti wa Tume ya Madini, Profesa Justinian Rwezaula Ikingura, Mwenyekiti wa Bodi ya *GST*, Meja Jenerali (Mstaafu) Michael Wambura Isamuhyo, Mwenyekiti wa Bodi ya *STAMICO*, Dkt. George Mofulu, Mwenyekiti wa Bodi ya *TGC,* Makamishna wa Tume ya Madini na wajumbe wa Bodi zote kwa kusimamia kwa umakini na weledi uendeshaji wa Sekta ya Madini.

**174. *Mheshimiwa Spika,*** vilevile, niwashukuru Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi wa Idara, Wakuu wa Vitengo, pamoja na Wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa na kwa kujituma bila kusukumwa katika kutekeleza majukumu ya Wizara ya Madini jambo linaloifanya Sekta ya Madini izidi kuimarika na kustawi.

**175. *Mheshimiwa Spika,*** niwashukuru pia wadau wa Sekta ya Madini wakiwemo watafutaji, wachimbaji, wenye mitambo ya uchenjuaji pamoja na wafanyabiashara wa madini kwa kuendelea kutekeleza shughuli zao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za nchi. Utekelezaji wa shughuli zao kwa mujibu wa sheria unarahisisha usimamizi wa shughuli hizo. Aidha, nizishukuru Taasisi za Fedha hususan mabenki kwa kuendelea kuwapa mikopo wachimbaji, vyombo vya ulinzi na usalama kwa kutuhakikishia usalama kwenye maeneo yenye shughuli za madini bila kusahau vyombo vyote vya habari kwa ushirikiano waliotupatia katika kuitangaza Sekta ya Madini.

**176. *Mheshimiwa Spika,*** shukrani zangu za pekee na za dhati naomba nizitoe kwa mara nyingine tena kwa wananchi wema wa Bukombe ambao kwa muda wote wameendelea

kunivumilia na kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu ya kitaifa kama Waziri. Aidha, niwashukuru kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo ya Jimbo. Naomba niwahakikishie kuwa nitazidi kuwatumikia kwa uaminifu na kasi zaidi kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia.

**177. *Mheshimiwa Spika,*** naomba sasa nichukue fursa hii kumshukuru kwa dhati mke wangu mpendwa Benadetha Clement Mathayo pamoja na watoto wangu wapendwa Elshadai, Elvin, Elis, Abigael, Amon, Abishai na Moses kwa kunivumilia, kuniombea kwa dhati kwa Mwenyezi Mungu, na kuniunga mkono katika utekelezaji wa majukumu yangu ya ubunge na uwaziri katika kujenga na kutetea maslahi ya Taifa letu.

## F. HITIMISHO

***178. Mheshimiwa Spika,*** ili Wizara iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyopangwa, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liridhie na kupitisha makadirio ya shilingi 83,445,260,000.0 kwa ajili ya matumizi ya Wizara na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kwa mchanganuo ufuatao:-

(i) Shilingi 22,000,000,000.0 ikiwa ni fedha za maendeleo; na

(ii) Shilingi 61,445,260,000.0 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Kati ya fedha hizo, shilingi 20,609,600,000.0 ni kwa ajili ya Mishahara na shilingi 40,835,660,000.0 ni Matumizi Mengineyo.

**179. *Mheshimiwa Spika,*** kwa mara nyingine naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Majedwali na vielelezo mbalimbali kwa ajili ya kutoa ufafanuzi wa masuala na takwimu muhimu kuhusu Sekta ya Madini vimeambatishwa pamoja na hotuba hii. Aidha, hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ya Madini kwa anuani ya *www.madini.go.tz.*

**180. *Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini. Kwa niaba yake Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Seif Gulamali.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, utangulizi. Awali ya yote naomba kutoa pole kwako wewe binafsi, Wabunge, familia, wananchi wa Mkoa wa Rukwa na Taifa kwa ujumla kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama Mbunge, Mwenyezi Mungu aipumzishe Roho ya marehemu mahali pema penponi - Amina.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, napenda kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Kamati kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Madini - Fungu 100 kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, naomba Taarifa hii yote ya Kamati iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara ya Madini kati ya tarehe 13 hadi 19 Machi 2022 katika Mkoa wa Dodoma, Dar Es Salaam

na Mbeya. Ambapo Kamati ilikagua jumla ya miradi mitatu kama ifuatayo:

(i) Mradi wa ujenzi wa jengo la Tume ya Madini - Dodoma (Namba ya Mradi 1119);

(ii) Mradi wa makaa ya mawe ya kupikia *(Coal Briquette)* Msasani - Dar Es Salaam (Namba ya Mradi 1119);

(iii) Mradi wa Kituo cha Umahiri cha Madini Chunya-Mbeya (Namba ya Mradi 1119);

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu miradi hiyo inaonekana katika Taarifa ya Kamati ukurasa wa pili hadi ukurasa wa nane.

Mheshimiwa Spika, maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotembelewa na Kamati:

(i) Kwa kuwa mradi wa makaa ya mawe ya kupikia *(coal briquette)* ni moja kati ya miradi yenye faida kiuchumi na kimazingira ni vema Serikali ianze kuutekeleza haraka, kikamilifu na kibiashara ili kuleta tija.

(ii) Tafiti zifanyike ili mashine zinazotumika kutengeneza makaa ya mawe ya kupikia zianze kutengenezwa hapa nchini ili kupunguza gharama za uwekezaji wa mradi kwa kutumia wataalam wa ndani kutoka *SIDO*, *VETA* na kadhalika.

(iii) Mradi wa ujenzi wa jengo la Tume ya Madini, kutokana na miradi hii kuchelewa kutokana na sababu mbalimbali kama zilivyoainishwa:-

(a) Serikali ione umuhimu wa mradi huu na kuhakikisha fedha za kutekeleza mradi zinatoka kabla ya mwaka huu wa fedha haujaisha;

(b) Taratibu za manunuzi na taratibu zinazotaka kampuni iliyoshinda tenda kuweka dhamana *(security bond)* ziangaliwe ili zisiwe kikwazo katika utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Kituo cha Umahiri.

(a) Kutokana na gharama za ujenzi wa Kituo kuwa ni kubwa, ipo haja ya Serikali kuangalia miradi yote ambayo fedha zinapatikana kutoka nje kuitazama vema masharti ya mikataba yake kabla ya kusaini,

(b) Karakana ya kituo iwekwe mashine zinazohitajika kwa ajili ya kufanya mafunzo kwa vitendo kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Bajeti. Uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Kwa taarifa ya utekelezaji Kamati ilichambua maeneo yafuatayo:

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara. Jukumu kuu la Wizara ya Madini ni kusimamia maendeleo ya sekta ya madini nchini kwa kuweka mifumo madhubuti inayosimamia utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini na kuhakikisha mchango wa sekta ya madini kwenye Pato la Taifa unaongezeka.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilijiwekea malengo au vipaumbele Saba ambavyo kwa uchambuzi wa Kamati kwa kiasi kikubwa utekelezaji umekuwa na mafanikio.

Mheshimiwa Spika, Wizara imefanikiwa kuimarisha usimamizi na ukaguzi kwenye maeneo ya uchimbaji, masoko ya madini, vituo vya uuzaji wa madini pamoja na mipaka ya nchi. Juhudi hizo zimesaidia kwa kuimarisha mchango wa sekta ya madini kwenye Pato la Taifa kutoka wastani wa asilimia 6.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2020 hadi kufikia wastani wa asilimia 7.3. Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua hii muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zoezi la kudhibiti utoroshwaji wa madini linaloendelea kufanyika limesaidia kwa kupunguza utoroshaji wa madini kutoka thamani ya Shilingi Trilioni 5.3 kwa

mwaka 2020/2021 hadi kufikia madini yenye thamani ya Shilingi Bilioni 501.2 mwaka 2021/2022 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 2. Kamati inasisitiza juhudi za kudhibiti utoroshaji wa madini ziendelee ili nchi iweze kunufaika na rasilimali hii.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka 2021/2022 kuhusu ukusanyaji wa maduhuli; kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ya Madini (Fungu 100) ilipangiwa kukusanya maduhuli ya Shilingi 696,441,871,667.00. kufikia Februari 2022 jumla ya Shilingi 422,512,319,079.00 sawa na asilimia 61.6 za makadirio ya makusanyo zimekusanywa. Kamati imefanya uchambuzi wake na kubaini makusanyo madogo ni kutoka *STAMICO* ambayo imekusanya asilimia 47 la lengo kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 3. Kamati inasisitiza *STAMICO* iongeze bidii ili iweze kufikia lengo la makusanyo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Upatikanaji wa Fedha kufikia Februari, 2022; Kamati imefanya uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Madini (Fungu 100) ambayo katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya Shilingi 66,816,467,000.00 kama mchanganuo wake unavyoonekana kwenye kielelezo Na.4.

Mheshimiwa Spika, kufikia Februari, 2022, Wizara ilipokea jumla ya Shilingi 36,665,203,816.00 sawa na asilimia 50.4 ya bajeti yote iliyoidhinishwa. Uchambuzi wa Kamati umebaini upatikanaji mdogo wa asilimia 20.7 ni katika fedha za miradi ya maendeleo. Ni rai ya Kamati kuwa fedha za Miradi ya Maendeleo zitoke zote kabla ya mwaka huu wa fedha kuisha ili miradi iliyopangwa iweze kutekelezwa. Ni rai ya Kamati kuwa Wakandarasi wajitahidi kuwasilisha nyaraka hizo kwa wakati ili fedha zitoke kwa wakati na miradi iliyopangwa iweze kutekelezwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa utekelezaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati kwa mwaka 2021/ 2022; katika Taarifa ya Kamati kuhusu uchambuzi wa bajeti ya mwaka 2021/2022 ya Wizara ya Madini (Fungu 100), Kamati

ilitoa jumla ya maoni 13. Kamati imebaini kwa kiasi kikubwa Wizara imetekeleza maoni, ushauri na mapendekezo hayo ya Kamati. Kwa maeneo ambayo bado hayajatekelezwa kikamilifu au utekelezaji wake unaendelea, Kamati itayasisitiza katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Madini (Fungu 100) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; uchambuzi wa malengo ya Wizara kwa mwaka fedha 2022/2023. Kamati imefanya uchambuzi wa taarifa ya Wizara kuhusu makadirio ya mapato na matumizi yake ya mwaka wa fedha 2022/2023 na kubaini kuwa bajeti hii ya Wizara imezingatia mambo mbalimbali, kama vile Mpango wa Taifa wa Tatu wa Maendeleo wa miaka Mitano 2021/2022 - 2025/2026 ukusara wa 96 na Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya Mwaka 2020 – 2025 ukurasa wa 108 – 110. Jumla ya vipaumbele Saba vimepangwa kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati ni kuwa vipaumbele hivi vitekelezwe kikamilifu kama ilivyokuwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ili sekta ya madini iendelee kutoa mchango mzuri katika uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli mwaka 2022/2023; katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Madini (Fungu 100) inakadiria kukusanya jumla ya Shilingi 894,278,406,800.00. Mchanganuo wake ni kama unavyoonekana kwenye kielelezo Na.5.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi kwa kufanya ulinganisho wa makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na mwaka wa fedha 2021/2022 na kubaini kuwa, makadirio ya makusanyo yameongezeka kwa asilimia 28 kama inavyoonekana kwenye kielelezo Na. 6.

Mheshimiwa Spika, ongezeko zaidi la makusanyo linaonekana kupitia *GST* kwa asilimia 125, Tume ya Madini kwa asilimia 26 na *STAMICO* kwa asilimia 52.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Mwaka wa Fedha, 2022/2023; katika Mwaka wa Fedha, 2022/2023, Wizara ya Madini, Fungu 100 inakadiria kutumia jumla ya Sh.83,445,260,000 kati ya fedha hizo Sh.40,835,660,000 sawa na asilimia 49 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Wizara. Sh.20,609,600,000 sawa na asilimia 25 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara na Taasisi zake na Sh.22,000,000,000 sawa na asilimia 26 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambazo zote ni fedha za ndani kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.7. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya ulinganisho kati ya Mwaka 2020/2021, 2021/2022 na 2022/2023 na imebaini kuwa ujumla wa bajeti umeongezeka kwa asilimia 24.9, ongezeko zaidi linaonekana katika miradi ya maendeleo asilimia 46.7, kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 8. Kamati inaipongeza sana Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuona umuhimu wa kuendelea kuongeza bajeti ya Wizara hii yenye mchango mkubwa katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa bajeti ya Wizara dhidi ya bajeti ya Taifa. Kamati haikuishia hapo ilifanya uchambuzi zaidi kwa kulinganisha mapendekezo ya bajeti ya Wizara kwa mwaka 2022/2023 dhidi ya bajeti kuu ya Taifa na kubaini kuwa bajeti ya Wizara ni asilimia 0.20 ya bajeti kuu ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, bajeti hii imeongezeka kutoka asilimia 0.18 katika Mwaka wa Fedha, 2021/2022 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 9. Kamati inaendelea kuipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza bajeti ya Wizara hii muhimu yenye mchango mzuri kwenye uchumi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa ujumla kuhusu sekta ya madini:-

(a) Mkakati wa kuendeleza madini *(Mining Development Strategy);* ili nchi iweze kunufaika ipasavyo na

rasilimali ya madini suala la kuwa na mkakati wa kuendeleza madini hayo *(Mining Development Strategy -MDS)* ni muhimu sana. Kamati inatambua bado nchi yetu haina mkakati huo. Katika kuchambua Kamati imepitia mikakati ya kuendeleza madini ya nchi na maeneo mbalimbali kama vile *Ontario Mineral Development Strategies, Northwest Territories Minerals Development Strategies* na *Yukon Mineral Development Strategies* na kuona namna zilivyojipanga katika kuhakikisha rasilimali ya madini inakuwa na manufaa kwa ustawi wa wananchi, lakini pia kunakuwa na mazingira mazuri ya uwekezaji.

Kamati inaona ipo haja ya Serikali kupitia mkakati wa kuendeleza madini wa nchi mbalimbali hususani zilizofanya vizuri ili kuweza kuiga yale mazuri kulingana na mazingira ya nchi yetu.

(b) Ukomo wa matumizi ya makaa ya mawe katika uzalishaji wa umeme; Kamati inatambua kuwa nchi yetu ina rasilimali ya kutosha ya makaa ya mawe ambayo kiuhalisia bado hayajatumika kikamilifu. Kamati pia inatambua kuwa Sera ya Dunia na hususani mkataba wa Paris wa mwaka 2015 *(The Paris Climate Agreement,* 2015) ni kuhakikisha makaa ya mawe ambayo ni chanzo cha nishati chenye kaboni nyingi zaidi kinafikia ukomo wa matumizi ikiwa ni hatua muhimu ya kufikia upunguzaji wa hewa chafu ili kupunguza ongezeko la joto duniani hadi kufikia $1.5^{0}C$.

Kwa mujibu wa ripoti maalum ya *Global and Regional coal phase - out requirements of the Paris Agreement: Insight from the IPCC Special Report* ya Septemba, 2019 inaonesha kuwa makaa ya mawe yanayotumika katika uzalishaji wa umeme yanachangia kwa kiasi kikubwa katika kutoa hewa chafu ambayo ni hatari kwa mazingira. Mojawapo ya mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti hiyo kukomesha makaa ya mawe duniani kote ifikapo mwaka 2040 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 10.

Mheshimiwa Spika, maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Maoni ya jumla:-

(a) Kutokana na maeneo mengi ya uzalishaji wa madini kuwa na miundombinu isiyokidhi mahitaji Kamati inashauri kuwa miundombinu hususani barabara za maeneo ya migodi kama Barabara ya Kiwira - Kabulo iboreshwe ziweze kupitika kwa wakati wote.

(b) Ili kuendana na mkakati wa dunia wa kuhakikisha inasitisha matumizi ya makaa ya mawe Wizara iandae *Coal Utilization Master Plan* kwa haraka, ili makaa ya mawe yaanze kutumika ipasavyo kabla ya kufikia ukomo mwaka, 2034.

(c) Ni vyema ujenzi wa vituo vya umahiri ukafanyika kwa kutumia mfumo wa *force account* ili kupunguza gharama bila kuathiri ubora unaotakiwa.

(d) Ili nchi iweze kunufaika na rasilimali ya madini Wizara ihakikishe uandaaji wa mkakati wa kuendeleza madini *(Mineral Development Strategies)* kama nchi nyingine zilivyofanya.

Mheshimiwa Spika, mbili, Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)*:-

(a) Uzalishaji wa makaa ya mawe ya kupikia *coal briquette* uwe wa kibiashara na uanze kwa haraka hasa katika Mikoa ya Pwani na Songwe kama ilivyopangwa.

(b) *STAMICO* iendelee kuongeza juhudi katika kulipa madeni ambayo *STAMIGOLD* inadaiwa kwa kuwa kati ya Shilingi bilioni 21.32, ni Shilingi bilioni 1.14 pekee zimelipwa kufikia Februari, 2022. Aidha, Serikali ione namna ya kuchukua deni hilo ili wazabuni waweze kupata haki na utaratibu ufanyike ili *STAMICO* iweze kuilipa Serikali taratibu.

(c) *STAMICO* iwezeshwe kimtaji ili kuweza kuendeleza Mgodi wa Kigodi. Aidha, kwa siku za mbele ione namna ya kuingia ubia na wawekezaji.

(d) Uunganishaji wa Mgodi wa *STAMIGOLD* Biharamulo katika Gridi ya Taifa ukamilike ili kupunguza

gharama za uzalishaji kwa mgodi kutokana na matumizi ya mafuta ya dizeli katika kuendesha mitambo.

(e) Wizara ione umuhimu wa kutoa kipaumbele katika uzalishaji wa madini chumvi kupitia *STAMICO* hasa ikizingatiwa kuwa uwekezaji wake ni mdogo lakini wenye faida na tija kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tatu, Tume ya Madini;

(1) kutokana na umuhimu wa Tume ya Madini katika kuhakikisha mchango wa sekta ya madini katika pato la Taifa Kamati inashauri mgawanyo wa fedha za matumizi mengineyo *(OC)* uendane na ukubwa wa kazi katika kila mkoa zilipo ofisi za madini. Hii itasaidia katika kuisimamia sekta kwa uchumi wa Taifa letu.

(2) Kamati inarudia ushauri ambao iliutoa mwaka 2020 kuhusu wajibu wa makampuni ya uchimbaji katika jamii inayowazunguka. Bado baadhi ya makampuni yamekuwa hayatimizi wajibu wao kikamilifu na hivyo kuzorotesha mahusiano na jamii. Ni rai ya Kamati kuwa suala hili lisimamiwe kikamilifu ili kuboresha mahusiano kwa mustakabali mzima wa ukuaji wa sekta.

(3) Tume ifanye mapitio ya leseni na kama itabainika kuwa zipo leseni hazifanyi kazi, basi zigawiwe kwa watu wengine watakaoweza kuzifanyia kazi au kuwekeza ili Serikali kuendelea kupata mapato yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nne, Wakala wa Jiolojia Nchini GST:-

(1) Wizara ione namna ya kuunda Bodi ya Usajili ya Wajiolojia *(Geologist Registration Board)* kama ilivyo kwa wanasheria ili kusimamia taaluma hii muhimu nchini.

(2) Utafiti wa rasilimali madini tulizonazo ni jambo la muhimu sana. Kamati imebaini kuwa Sera ya Madini ya Mwaka, 2009 bado haijaeleza vizuri umuhimu wa kufanya

utafiti. Ipo haja ya kujipanga kwa kuirejea Sera hii ili kuweza kufanya utafiti na kujua rasilimali tulizonazo hivyo kwenda sambamba na dunia ambayo inatumia akili mnemba *(artificial intelligence)* kufanya tafiti zake.

(3) *GST* iwezeshwe kutekeleza majukumu yake muhimu ikiwa ni pamoja na kuongezewa watumishi wenye taaluma maalum *(rare professionals)*, kuboreshwa miundombinu ya utafiti na kuongezwa bajeti kwa ajili ya kufanya utafiti ili kuendeleza sekta ya madini.

(4) Uundwe Mfuko maalum wa *GST* ambao utachangiwa na vyanzo mbalimbali kwa ajili ya kusaidia Wakala kufanya utafiti endelevu.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Uhamasishaji uwazi na uwajibikaji wa rasilimali madini, mafuta na gesi asilia *(TEITI)*:-

(1) *TEITI* iharakishe kuanzisha kanzidata *(Database)* ya wamiliki wa migodi kwa masilahi mapana ya nchi.

(2) *TEITI* iwezeshwe kifedha ili kuweza kusimamia kikamilifu jukumu lake la kuhakikisha kuwa mapato yatokanayo na rasilimali madini, mafuta na gesi asilia yanahakikiwa na kutumika kwa manufaa ya wananchi wote.

(3) Kamati ya *TEITI* ambayo ndio ina wajibu wa kutekeleza majukumu ya Taasisi iundwe haraka.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Jiomolojia Tanzania – *TGC*. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga shilingi bilioni saba kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya *TGC*. Kamati inasisitiza miradi hii isimamiwe kikamilifu ili iweze kutekelezwa kama ilivyopangwa kwa masilahi mapana ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Hitimisho; kwa mara nyingine napenda kuchukua fursa hii kukushukuru sana wewe Spika wetu; Naibu Spika, Mheshimiwa Azan Zungu; na Wenyeviti

wengine wote wa Bunge kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu. *(Makofi)*

Kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini kwa ushirikiano wao wakati wote wa kutekeleza majukumu ya Kamati na kushiriki vizuri katika uchambuzi wa bajeti ya Wizara hii. Kwa heshima kubwa naomba majina yao yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Waziri wa Madini Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko na Naibu Waziri Mheshimiwa Steven Lemomo Kiruswa pamoja na Watendaji wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Adolph Ndunguru kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiutoa kwenye Kamati wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Joyce Mwihambi, *ndc.*

Namshukuru pia Mkurugenzi wa Idara ya Kamati ya Bunge, Ndugu Athuman Brambat Hussein na Kaimu Mkurugenzi Msaidizi sehemu inayosimamia Kamati yetu Ndugu Msigwa Dickson Bisile kwa ushirikiano na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yetu bila mkwamo. Kipekee zaidi nawashukuru sana Makatibu wa Kamati Ndugu Pamela Pallangyo, Ndugu Onesmo Laulau na Ndugu Hosiana John na Msaidizi wa Kamati Ndugu Rukia Shabani kwa uratibu mzuri wa shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha taarifa hii kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini Fungu 100 kwa Mwaka wa Fedha, 2022/2023 kama yalivyowasilishwa na Mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Makamu Mwenyekiti kwa Wasilisho hilo. Sasa kabla hujatoka hapo hebu tafuta karatasi yako iliyokuwa inazungumza kuhusu Sehemu ya Pili ya Uchambuzi wa Bajeti. Tunatafuta sehemu ambayo inazungumzia utoroshaji wa madini, ukitafuta Kielelezo Na.2 itakurahisishia. Umeshakipata Kielelezo Na.2 rudi kwenye maelezo ya hapo juu yanayoanza Mheshimiwa Spika, Wizara imefanikiwa. Umepapata juu tu ya hicho Kielelezo Na.2 umeshayaona? Umekiona Kielelezo Na.2 kuna maelezo sasa, hapo juu yanayoanzia Mheshimiwa Spika umeshafika? Sawa sasa juu ya hicho Kielelezo kuna maelezo yanayosomeka hivi ngoja nikusomee kuna maelezo yanasomeka hivi:-

Wizara imefanikiwa kuweka mifumo madhubuti halafu imeendelea ikataja Mikoa hapo na Mwanza umeshuka kutoka thamani ya Shilingi trilioni 5.3 umepaona? Juu tu ya hicho Kielelezo Na. 2. Pengine niletee hiyo karatasi yake yenye Kielelezo Na. 2 na inayotangulia mbele sasa. Sawa wewe niletee hiyo yenye Kielelezo Na. 2 ili nijue umesoma nini hapo?

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, sawa tutawasilisha hii taarifa niliyosoma hapa ni *Summary* ya Taarifa yetu na tuliomba hapa kwamba Taarifa yote iingizwe kwa hiyo tutawasilisha Kielelezo hicho.

**SPIKA:** Hapana Kielelezo mimi ninacho hapa, nataka tu kujua wewe unacho hapo kwenye hiyo *summary* au huna?

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, hapana.

**SPIKA:** Huna.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ukurasa Na. 5.

**SPIKA:** Kuna kitu cha kurekebisha kidogo hapo ndio maana nimeku...

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, iko wapi? *Yes,* hii hapa nimepata.

**SPIKA:** Umepata sasa ukurasa Na. 13 nafikiri unatumia sasa Kitabu si ndio?

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ndio.

**SPIKA:** Hapo chini unaona maelezo hayo yanasema Shilingi trilioni 5.3.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, *Yes*.

**SPIKA:** Umeyaona?

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ndio.

**SPIKA:** Yanapaswa kuwa Shilingi bilioni 5.3 kwa sababu ndio yaliyopo kwenye Kielelezo na sio trilioni.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, sawa.

**SPIKA:** Pia ukurasa unaofuata sasa hapo baada ya mwaka 2020/2021 yenye thamani ya Shilingi bilioni 501.2 inapaswa iwe Shilingi milioni 500 kwa sababu ndio kinachoonekana hapo.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Shilingi bilioni 500.

**SPIKA:** Ndio sasa isome hivyo sawa sawa ili Kitabu chako kirekebishwe.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Wizara imefanikiwa kuweka mifumo madhubuti inayosimamia utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini ambayo imesaidia kudhibiti utoroshwaji wa madini. Utoroshwaji wa madini ya aina mbalimbali kama dhahabu, vito, mchanga na madini ya viwandani vilivyokuwa katika Mikoa ya Mbeya, Morogoro, Manyara, Dodoma, Lindi, Geita, Kilimanjaro, Dar es Salaam na Mwanza umeshuka kutoka thamani ya shilingi bilioni 5.3. *(Makofi)*

**SPIKA:** Soma tu inavyosomeka Shilingi bilioni 5.3 halafu ili umalizie marekebisho hapo.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha, 2020/2021 hadi kufikia madini yenye thamani ya Shilingi bilioni...

**SPIKA:** Milioni.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, shilingi milioni 501.

**SPIKA:** Sawa, yaani unarekebisha taarifa yako uliyosema iingie kwenye taarifa rasmi za Bunge imekosewa maelezo wakati kwenye Kielelezo iko sawasawa.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, *yes*.

**SPIKA:** Kwa hiyo, ndio hicho tulitaka urekebishe hapo.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru tutarekebisha haya maelezo ya maandishi. Ahsante. *(Makofi)*

**TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MADINI (FUNGU 100) KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

***[Inatolewa Chini ya Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020]***

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, Awali ya yote naomba kutoa pole kwako wewe binafsi, Wabunge, Familia, Wananchi wa Mkoa wa Rukwa na Taifa kwa ujumla kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa Mhe. Irene Alex Ndyamkama (Mb). **Mwenyezi Mungu aipumzishe Roho ya Marehemu Mahali Pema Penponi Amina.**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020[1], naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini **(Fungu 100)** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

[1] Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020

**Mheshimiwa Spika,** Majukumu ya Kamati kuhusiana na Uchambuzi wa Bajeti ya kila mwaka ya Wizara inazozisimamia yameelekezwa katika Fasili ya 7(1)(a) ya nyongeza ya Nane ya Kanuni za kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza jukumu hili, Kamati ilikagua baadhi ya miradi iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 na pia ilichambua taarifa za utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka huo.

### 1.1 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo Iliyotengewa Fedha

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya Ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara ya Madini. Ziara hizo zilifanyika kati ya tarehe 13 hadi 19 Machi 2022 katika Mkoa wa Dodoma, Dar Es Salaam na Mbeya. Jumla ya miradi mitatu ifuatayo ilitembelewa na kukaguliwa na Kamati:-

a) Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Tume ya Madini - Dodoma (Namba ya Mradi 1119);

b) Mradi wa Makaa ya Mawe ya Kupikia (*Coal Briqquette*) – Msasani, Dar Es Salaam (Namba ya Mradi 1119); na

c) Mradi wa Kituo cha Umahiri cha Madini Chunya, Mbeya (Namba ya Mradi 1119)

### 1.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

#### a) Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Tume ya Madini - Dodoma (Namba ya Mradi 1119)

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 13 Machi 2022, Kamati ilitembelea Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Tume ya Madini uliopo Mtaa wa Uzunguni Dodoma. Mradi unatekelezwa na Mkandarasi MCB Co.Ltd kufuatia mkataba wa tarehe 07 Januari, 2021 kati ya Tume ya Madini na mkandarasi huyo. Aidha, mradi unasimamiwa na TBA kama msimamizi mshauri.

**Mheshimiwa Spika**, gharama za ujenzi wa mradi ni **Shilingi 4,211,002,617.00.** Kati ya fedha hizo**, Shilingi 4,069,855,737.00** sawa na **asilimia 96.6** ni kwa ajili ya Mkandarasi na **Shilingi 141,146,880.00** sawa na **asilimia 3.4** ni kwa ajili ya Mshauri Msimamizi. Kulingana na mkataba, kipindi cha utekelezaji wa mradi ni miezi 12 kuanzia tarehe ya kusainiwa. Hivyo mradi ulitakiwa kukamilika na kukabidhiwa Tume ya Madini tarehe 28 Januari, 2022. Kamati ilielezwa kuwa, kutokana na changamoto za mvua nyingi pamoja na taratibu za ununuzi kwa mkandarasi kuchelewa, mradi ulichelewa kuanza hivyo kutokamilika kwa wakati. Kufikia tarehe 13 Machi, 2022 wakati Kamati inatembelea, mradi ulikuwa umefikia **asilimia 48** na Mkandarasi aliomba kuongezewa muda wa mkataba kwa siku 278 lakini Mshauri Msimamizi wa ujenzi amefanya tathmini na kupendekeza kuongezwa siku 119 na Tume ya madini imeridhia.[2]

**Mheshimiwa Spika**, Kufikia Machi 2022 Mkandarasi ameshalipwa kiasi cha **Shilingi 822,441,038.82** sawa na **asilimia 20.2** ya Shilingi **4,069,855,737.00** za gharama za mkandarasi na **Shilingi 70,573,440.00** sawa na **asilimia 50** ya **Shilingi 141,146,880.00** ambazo ni malipo ya Msimamizi Mshauri.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa, pamoja na sababu zilizoelezwa, lakini pia kuchelewa kwa mradi kumesababisha na kutotolewa kwa fedha kwa wakati, taratibu za manunuzi ambazo huchukua takribani siku 14 – 20 kukamilika pamoja na utaratibu unaotaka Kampuni iliyoshinda Tenda kuweka dhamana (*Security Bond*). **Kamati inaona kuna haja na umuhimu wa kuhakikisha kuwa fedha zinatolewa kwa wakati. Vilevile, upo umuhimu wa kuhakikisha taratibu za manunuzi na masharti yanayohitaji uwekaji wa dhamana (*Security Bond*) kwa Taasisi za Umma hayawi kikwazo katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo nchini.**

[2] Taarifa ya Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Tume ya Madini Makao Makuu hadi Machi, 2022 kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini

**b) Mradi wa Makaa ya Mawe ya Kupikia (*Coal Briqquette*) – Msasani, Dar Es Salaam (Namba ya Mradi 1119)**

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 14 Machi, 2022, Kamati ilitembelea Mradi wa Makaa ya Mawe ya kupikia unaotekelezwa na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) katika eneo la Msasani, Dar Es Salaam. Mradi unahusika na kutengeneza mkaa usiokuwa na moshi (*smokeless briquette)*, harufu, wala hewa chafu na wenye kuwaka kirahisi, lengo ni kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa nishati mbadala ili kupunguza ukataji wa miti ambao umeleta madhara makubwa kwenye mazingira. Mradi unaendelea vizuri kufuatia utafiti kati ya STAMICO, TIRDO na COSTECH.

**Mheshimiwa Spika**, gharama za awali za kutekeleza mradi huo ni **Shilingi 270,000,000.00** ambazo wakati Kamati inatembelea Mradi huu zilikuwa zimepokelewa zote kwa asilimia 100. **Kamati inapongeza Serikali kwa hatua hii.**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mipango mbalimbali ya ya baadae ya STAMICO, Kamati imebaini changamoto zifuatazo:-

a) Bado mradi huu haujaanza kutekelezwa kibiashara kwani bidhaa haijaanza kuuzwa kwa jamii licha ya faida zake;

b) STAMICO bado haijawa na Mkakati madhubuti wa kuhakikisha inalifikia soko la wateja hasa katika Mkoa wa Dar es Salaam ambako ndiko matumizi ya mkaa wa kawaida ni makubwa kwa takribani **asilimia 60** ya mkaa wote unaotumika nchini; na

c) Ipo haja ya kuhusisha Sekta Binafsi ili kuanzisha viwanda kutokana na mradi kuwa wa gharama nafuu.

**c) Mradi wa Kituo cha Umahiri cha Madini – Chunya (Namba ya Mradi 1119)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea Mradi wa ujenzi wa Kituo cha umahiri Chunya ambacho ni sehemu ya mradi

mama unaohusisha vituo vingine vya umahiri vya Songea na Mpanda. Mradi huu ulikuwa wenye jumla ya gharama za **Shilingi 3,652,529,697.00** ikiwa ni pamoja na VAT, ambapo kwa Kituo cha umahiri Chunya, mradi ulikuwa na gharama za **Shilingi 1,019,424,954.25.** Gharama hizo zinajumuisha ujenzi wa Jengo Kuu, karakana, kibanda cha mlinzi, uzio, uwekaji wa *pavements* pamoja na ununuzi wa samani mbalimbali. Wakati Kamati inatembelea mradi, kiasi cha **Shilingi 876,789,297.29** sawa na **asilimia 86.01** kilikuwa tayari kimelipwa[3].

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu ulianza kutekelezwa na M/S SUMA JKT *Construction Company Limited* tarehe 13 Julai, 2018, ukisimamiwa na Y&P *Architects* kwa muda wa miezi 6 hivyo ulitarajiwa kukamilika tarehe 13 Januari, 2019. Hata hivyo, mradi haujakamilika kwa wakati kutokana na sababu mbalimbali mojawapo ikiwa ni mkataba wa msimamizi kuisha na kushindwa kukubaliana katika kuongeza muda wa usimamizi. Wizara ya Madini iliomba wataalamu kutoka Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kupitia Kitengo chake cha Ushauri Majenzi (*MoD Consulting Unit*) kusimamia umaliziaji ili kuhakikisha vituo vya umahiri katika miji tajwa vinakamilika. Hivyo, mradi ulifanyiwa ongezeko la muda wa kukamilika rasmi tarehe 24 Julai, 2021. Kwa sasa mradi upo katika kipindi cha matazamio ambacho kitakamilika tarehe 24 Julai, 2022.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliona kazi mbalimbali za ujenzi zilizofanyika katika Kituo cha Umahiri Chunya pamejengwa Jengo Kuu la Ofisi lenye vyumba vya Ofisi mbalimbali na chumba madhubuti cha kuhifadhia madini (*Strong Room*), masijala, chumba cha TEHAMA, chumba cha mikutano. Tayari jengo limewekewa mfumo wa maji, umeme, mawasiliano, CCTV kamera na samani. Imejengwa pia karakana yenye sehemu ya wazi kwa ajili ya kuchakata madini, kibanda cha mlinzi, uzio na mnara wa maji safi.

---

[3] Taarifa ya Mradi wa ujenzi wa Vituo vya Umahiri Songea, Mpanda na Chunya: Sehemu ya Mradi ya Chunya

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini changamoto zifuatazo;-

i) Gharama kubwa zimetumika kutekeleza mradi ambayo kwa maoni ya Kamati hailingani na thamani ya jengo na hii inachangiwa kwa kiasi kikubwa na chanzo cha fedha za mradi na masharti yake; na

ii) Miundombinu isiyokidhi mahitaji kama ya maji safi na majitaka kutokana na usanifu duni.


iii) Hakuna mfumo wa maji salama kutoka Mamlaka ya Maji; na

iv) Eneo la mradi ni oevu na linajaa maji nyakati za masika

v) Hakuna mifumo ya maji taka.

**Mheshimiwa Spika**, wastani wa upatikanaji wa fedha kwa miradi hiyo mitatu (3) ambayo Kamati iliitembelea ni **asilimia 38** kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.1.

**Kielelezo Na. 1: Hali ya Upatikanaji wa Fedha kwa Miradi iliyotembelewa na Kamati**




***Chanzo: Taarifa za Miradi za Wizara (Machil 2022) na Usanifu wa Kamati***

### 1.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotembelewa na Kamati

a) Kwa kuwa **Mradi wa Makaa ya Mawe ya Kupikia (*Coal Briquette*)** ni moja kati ya miradi yenye faida kiuchumi na kimazingira:-

i)Ni vyema Serikali ianze kuutekeleza haraka, kikamilifu na kibiashara ili kuleta tija;

ii) Kutokana na gharama za utekelezaji wa mradi wa aina hii kuwa ni za wastani, ipo haja sasa kwa Serikali kushirikisha Sekta Binafsi ili ziweze kutekeleza miradi ya aina hii katika maeneo mbalimbali nchini; na

iii) Tafiti zifanyike ili mashine zinazotumika kutengeneza makaa ya mawe ya kupikia zianze kutengenezwa hapa nchini ili kupunguza gharama za uwekezaji wa mradi kwa kutumia wataalam wa ndani kutoka SIDO, VETA n.k.

b) **Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Tume ya Madini**

Kutokana na Mradi hii kuchelewa kutokana na sababu mbalimbali kama zilivyoainishwa:-

i) Serikali ione umuhimu wa mradi huu na kuhakikisha fedha za kutekeleza mradi zinatoka kabla ya Mwaka huu wa Fedha haujaisha; na

ii) Taratibu za manunuzi na taratibu zinazotaka Kampuni iliyoshinda Tenda kuweka dhamana (*Security Bond*) ziangaliwe ili zisiwe kikwazo katika utekelezaji wa mradi.

c) **Mradi wa Kituo cha Umahiri**

i) Kutokana na gharama za ujenzi wa Kituo kuwa ni kubwa ipo haja ya Serikali kuangalia miradi yote ambayo fedha zinapatikana kutoka nje kuitazama vyema masharti ya mikataba yake kabla ya kusaini;

ii) Changamoto ya miundombinu ya maji na majitaka, mkakati ufanyike haraka kuondoa changamoto hizi; na

iii) Karakana ya Kituo iwekwe mashine zinazohitajika kwa ajili ya kufanya mafunzo kwa vitendo kwa wachimbaji wadogo.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA BAJETI

### 2.1 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI PAMOJA NA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa Bajeti na Majukumu ya Wizara ya Madini **(Fungu 100)** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ulijikita katika maeneo makuu manne (4) ambayo ni:-

a) Utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

b) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kuhusu ukusanyaji wa Maduhuli;

c) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kuhusu upatikanaji wa fedha; na

d) Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati kwa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

#### 2.1.1 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara

**Mheshimiwa Spika** jukumu kuu la Wizara ni kusimamia maendeleo ya Sekta ya Madini nchini kwa kuweka mifumo madhubuti inayosimamia utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini ili kuhakikisha mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa unaongezeka.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wizara ilijiwekea vipaumbele saba (7) vifuatavyo ambavyo pia vimeelezwa na Waziri mwenye dhamana: -

i) Kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa;

ii) Kuwaendeleza wachimbaji wadogo na kuwawezesha wananchi kushiriki katika uchumi wa madini;

iii) Kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini;

iv) Kuhamasisha biashara na uwekezaji katika Sekta ya Madini;

v) Kusimamia mfumo wa ukaguzi wa shughuli za migodi;

vi) Kuzijengea uwezo taasisi zilizo chini ya Wizara ili ziweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi; na

vii) Kuendeleza rasilimaliwatu na kuboresha mazingira ya kufanya kazi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa vipaumbele umekuwa na mafanikio. Katika kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa, Wizara imefanikiwa kuimarisha usimamizi na ukaguzi kwenye maeneo ya uchimbaji, masoko ya madini, vituo vya uuzaji wa madini pamoja na mipaka ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, juhudi hizo zimesaidia katika kuimarisha mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa kutoka wastani wa **asilimia 6.5** katika kipindi kama hicho mwaka 2020 hadi kufikia wastani wa **asilimia 7.3**.[4] Mwenendo huu wa

[4] Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022: Utekelezaji Katika Maeneo ya Vipaumbele uk.6

mchango unatoa mwelekeo chanya kuwa Sekta ya Madini itaweza kuchangia **asilimia 10** ya Pato la Taifa ifikapo mwaka 2025. **Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua hii muhimu.**

**Mheshimiwa Spika**, Wizara imefanikuwa kuweka mifumo madhubuti inayosimamia utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini ambayo imesaidia kudhibiti utoroshwaji madini. Utoroshaji wa madini ya aina mbalimbali kama dhahabu, vito, mchanga na madini ya viwandani yaliyokamatwa katika mikoa ya Mbeya, Morogoro, Manyara, Dodoma, Lindi, Geita, Kilimanjaro, Dar es Salaam na Mwanza umeshuka kutoka thamani ya **Shilingi Trilioni 5.3** Mwaka 2020/2021 hadi kufikia madini yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 501.2** Mwaka 2021/2022 sawa na kushuka kwa **asilimia 90.6** kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.2. **Kamati inatoa pongezi kwa Wizara na inasisitiza juhudi za kudhibiti utoroshaji wa madini ziendelee ili nchi iweze kunufaika na rasilimali hii**.

**Kielelezo Na. 2: Takwimu za Matukio ya utoroshaji Madini Nchini**

| Mwaka | Idadi ya Matukio | Kiasi | | | Thamani ya Madini | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Gramu | Cubic Metres | Karati | USD | TZS |
| 2014/2015 | 11 | 394,540.40 | - | 161.01 | 34,127.83 | 34,670,794.00 |
| 2015/2016 | 22 | 32,747.45 | - | 502.3 | 1,479,450.78 | 151,338,373.84 |
| 2016/2017 | 15 | 1,941,100.55 | - | 412.16 | 119,193.31 | 44,873,540.00 |
| 2017/2018 | 21 | 76,634,783.13 | - | 270.21 | 2,827,863.46 | 568,403,232.00 |
| 2018/2019 | 41 | 86,981,053.91 | - | 5,439.51 | 15,115,852.85 | 1,636,646,197.08 |
| 2019/2020 | 98 | 13,371,037.37 | 14.5 | 1,284.56 | 62,284.38 | 4,576,365,579.94 |
| 2020/2021 | 87 | 1,416,781.52 | 48.5 | 2.84 | - | 5,308,703,518.14 |
| 2021/2022 | 46 | 20,346,872.14 | 12 | 1.42 | - | 501,223,895.65 |
| **Jumla** | **341** | **201,118,916.46** | **75** | **8,074.01** | **19,638,772.62** | **12,822,225,130.64** |

***Chanzo: Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022***


### Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka 2021/2022 kuhusu ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara ya Madini **(Fungu 100)** ilipangiwa kukusanya maduhuli ya **Shilingi 696,441,871,667.00.** Kati ya makadirio hayo, **Shilingi 650,010,001,000.00** sawa na **asilimia 93.3** zilipangwa kukusanywa kupitia Idara na Vitengo vya Wizara kwa ajili ya kuwasilishwa Hazina. Aidha, makusanyo kupitia Taasisi kwa ajili ya matumizi ya Taasisi hizo yalijumuisha **Shilingi 45,362,835,564.00** sawa na **asilimia 6.5** kupitia STAMICO, **Shilingi 889,035,100.00** sawa na **asilimia 0.1** kupitia GST na **Shilingi 180,000,003.00** sawa na **asilimia 0.03** kupitia TGC ambayo hubaki kwa ajili ya matumizi ya Taasisi hizo (*Retention*).

**Mheshimiwa Spika,** kufikia Februari, 2022, Jumla ya **Shilingi 428,779,255,318** sawa na **asilimia 61.6** za makadirio ya makusanyo zimekusanywa. Kamati imefanya uchambuzi wake na kubaini kuwa, kati ya makusanyo hayo, Wizara imekusanya **Shilingi 406,639,669,735.00** sawa na **asilimia 62.6** ya lengo. Aidha, kwa upande wa Taasisi, STAMICO imekusanya **Shilingi 21,307,968,770** sawa na **asilimia 47**, GST **Shilingi 691,858,813.00** sawa na **asilimia 77.8** na TGC **Shilingi 139,758,000.00** sawa na **asilimia 77.6** kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 3.

**Kielelezo Na. 3: Ukusanyaji wa Maduhuli kufikia Februari, 2022**

| WIZARA YA MADINI - FUNGU 100 BAJETI 2021/2022 | | | |
|---|---|---|---|
| CHANZO | MAKADIRIO | MAKUSANYO | ASILIMIA |
| IDARA NA VITENGO | 650,010,001,000 | 406,639,669,735 | 62.6 |
| STAMICO | 45,362,835,564 | 21,307,968,770 | 47.0 |
| GST | 889,035,100 | 691,858,813 | 77.8 |
| TGC | 180,000,003 | 139,758,000 | 77.6 |
| JUMLA | **696,441,871,667** | **428,779,255,318** | **61.6** |




**Chanzo: Randama ya Wizara ya Machi 2022 na usanifu wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilihoji sababu za STAMICO kutofikia wastani wa makusanyo na ilielezwa kuwa ni kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo

i) Kuchelewa kupatikana kwa mitambo ya miradi ya *coal briquette,*

ii) Changamoto ya UVIKO 19 katika nchi inapotengenezwa mitambo kwa ajili ya mgodi wa Buhemba na Buckreef na hivyo kuchelewa kuanza kwa biashara ya huduma ya uchorongaji katika miradi hiyo; na

iii) Kuchelewa kwa malipo ya kazi za uchorongaji kwa mujibu ya mikataba ya uchorongaji ambapo uchorongaji unafanyika kwanza na malipo hufuata baada ya kazi.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Wizara kuisimamia STAMICO kikamilifu ili iweze kufikia malengo ya makusanyo ipasavyo**

### 2.1.2 Uchambuzi wa Upatikanaji wa Fedha kufikia Februari, 2022


**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Madini **(Fungu 100)** ambayo katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi 66,816,467,000.00**. Kati ya Fedha hizo, **Shilingi 51,816,467,000.00** sawa na **asilimia 77.6** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida zenye kujumuisha **Shilingi 33,335,660,000.00** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Shilingi 18,480,807,000.00** kwa ajili ya Mishahara ya watumishi wa Wizara na Taasisi zake. Aidha, **Shilingi 15,000,000,000.00** sawa na **asilimia 22.4** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ambazo zote ni fedha za ndani.

**Mheshimiwa Spika,** kufikia Februari, 2022, Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 36,665,203,816.00** sawa na **asilimia 50.4** ya bajeti yote iliyoidhinishwa[5]. Uchambuzi wa Kamati umebaini kati ya fedha hizo zilizopokelewa, Matumizi Mengineyo ni **Shilingi 21,395,781,833.10** sawa na **asilimia 64.2**, Mishahara **Shilingi 12,169,421,982.96** sawa na **asilimia 65.8** na **Miradi ya Maendeleo Shilingi 3,100,000,000.00** sawa na **asilimia 20.7** kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.4.

**Kielelezo Na 4: Upatikanaji wa Fedha kufikia Februari, 2022**

| AINA | BAJETI | KILICHOPOKELEWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| MAENDELEO | 15,000,000,000 | 3,100,000,000 | 20.7 |
| OC | 33,335,660,000.00 | 21,395,781,833.10 | 64.2 |
| MISHAHARA | 18,480,807,000.00 | 12,169,421,982.96 | 65.8 |
| **JUMLA** | **66,816,467,000.00** | **36,665,203,816** | **54.9** |

[5] Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022: Fedha zilizopokelewa kufikia Februari 2022 uk.3




***Chanzo: Taarifa ya utekelezaji ya Wizara (Machi 2022) na Usanifu wa Kamati***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini sababu mbalimbali zinazochangia kuchelewa kupatikana kwa fedha za Miradi ya Maendeleo ikiwemo ya kuchelewa kuwasilisha nyaraka mbalimbali za mikataba, hati za madai (*certificate*), na ankara za malipo (*invoice*). **Ni Rai ya Kamati kuwa, Wakandarasi wajitahidi kuwasilisha nyaraka hizo kwa wakati ili fedha zitoke kwa wakati na miradi iliyopangwa iweze kutekelezwa kikamilifu.**

### 2.1.3 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Maoni na Ushauri uliotolewa na Kamati kwa mwaka 2021/2022

**Mheshimiwa Spika**, katika Taarifa ya Kamati kuhusu uchambuzi wa Bajeti ya Mwaka 2021/2022 ya Wizara ya Madini **(Fungu 100),** Kamati ilitoa jumla ya maoni 13 ili kuboresha utendaji kazi wa Wizara na Serikali kwa ujumla. Kamati imepitia Taarifa ya utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati na kubaini kwa kiasi kikubwa Wizara imetekeleza Maoni, Ushauri na Mapendekezo hayo ya Kamati. Kwa maeneo ambayo bado hayajatekelezwa kikamilifu au utekelezaji wake unaendelea Kamati itayasisitiza katika Taarifa hii likiwemo suala la STAMICO kuwezeshwa ili kuweza kujiendesha kibiashara na Wajibu wa Makampuni ya Uchimbaji kwa Jamii zinazowazunguka.

### 2.2 Uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Madini (Fungu 100) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini **(Fungu 100)** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha uliopita (2021/2022)[6].Uchambuzi ulijielekeza katika maeneo yafuatayo:-

a) Uchambuzi wa Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

b) Uchambuzi wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

c) Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi Mwaka wa Fedha 2022/2023

d) Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa

e) Uchambuzi wa Ujumla kuhusu Sekta ya Madini

#### 2.2.1 Uchambuzi wa Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa Taarifa ya Wizara kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi yake kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na kubaini kuwa, Bajeti hii ya Wizara imezingatia mambo mbalimbali kama vile Mpango wa Taifa wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26[7] na Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya Mwaka 2020 - 2025[8]. Na katika mipango hiyo, vipaumbele saba (7) vya Wizara kwa Mwaka 2022/2023 pia vilikuwa vipaumbele katika Mwaka wa Fedha 2021/2022. Vipaumbele hivyo ni pamoja na:-

[6] Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2022

[7]https://www.mof.go.tz/docs/news/Mpango%20wa%20Tatu%20wa%20Maendeleo%20wa%20Taifa%20wa%20Miaka%20Mitano%20202122-202526%20.pdf (Uk. 96)

[8]Ilani ya Chama cha Mpainduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 (Uk. 108 -110).

i) Kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa;

ii) Kuwaendeleza wachimbaji wadogo na kuwawezesha wananchi kushiriki katika uchumi wa madini;

iii) Kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini;

iv) Kuhamasisha biashara na uwekezaji katika Sekta ya Madini;

v) Kuzijengea uwezo taasisi zilizo chini ya Wizara ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi;

vi) Kusimamia mfumo wa ukaguzi wa shughuli za migodi; na

vii) Kuendeleza rasilimaliwatu na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi.

**Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kuwa vipaumbele hivi vitekelezwe kikamilifu kama ilivyokuwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ili Sekta ya Madini iendelee kutoa mchango mzuri katika Uchumi wa Taifa letu.**

**2.2.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli Mwaka 2022/2023**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Madini **(Fungu 100)** inakadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 894,278,406,800.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 822,028,205,000.00** sawa na **asilimia 92** zitakusanywa kupitia Idara, Vitengo vya Wizara na Tume ya Madini na zitawasilishwa Hazina**.** Aidha**, Shilingi 72,250,201,800.00** sawa na **asilimia 8** zitakusanywa na kutumika na Taasisi zilizo chini ya Wizara kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 5.

**Kielelezo Na: 5: Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli 2022/ 2023**

| Maduhuli yatakayokusanywa na Kuwasilishwa Hazina | | |
|---|---|---|
| **CHANZO** | **2022/2023** | **ASILIMIA** |
| **WIZARA** | 10,002,000.00 | **0.0** |
| **TUME YA MADINI** | 822,018,203,000.00 | **92.0** |
| **Jumla Ndogo** | **822,028,205,000** | **92.0** |
| **Maduhuli yatakayokusanywa na Kutumika na Taasisi** | | |
| **CHANZO** | **2022/2023** | **ASILIMIA** |
| **STAMICO** | 69,000,000,000.00 | **7.7** |
| **GST** | 2,000,800,000.00 | **0.2** |
| **TGC** | 201,675,000.00 | **0.0** |
| **Jumla Ndogo** | **71,202,475,000.00** | **8.0** |
| **JUMLA KUU** | **893,230,680,000.00** | **100** |

***Chanzo: Randama ya Wizara ya Machi 2022 na Usanifu wa Kamati***

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya ulinganisho wa makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na 2021/2022 na kubaini kuwa, makadirio ya makusanyo yameongezeka kutoka **Shilingi 696,441,872,667.00** Mwaka 2021/2022 hadi kufikia **Shilingi 894,278,406,800.00** Mwaka 2022/2023 ambayo ni ongezeko la **Shilingi 196,788,807,333.00** sawa na **asilimia 28** kama inavyoonekana kwenye Kielelezo na. 6.

**Mheshimiwa Spika,** Ongezeko zaidi la makusanyo linaonekana katika taasisi za Wizara zifuatazo:-

a. GST kwa **asilimia 125** kutoka **Shilingi 889,035,100.00** hadi kufikia **Shilingi 2,000,800,000.00** ;

b. Tume ya Madini kutoka **Shilingi 650,000,000,000.00** hadi kufikia **Shilingi 822,018,203,000**

c. STAMICO kutoka **Shilingi 45,362,835,564.00** kufikia **Shilingi 69,000,000,000.00**

**Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa sababu zilizofanya ongezeko la makadirio ya makusanyo hususan kwa Taasisi zilizotajwa ni pamoja na:-

**a) GST:** Kuboreshwa kwa huduma za ushauri elekezi katika nyanja za jiolojia, jiokemia na jiofizikia baada ya kupata vitendea kazi vipya; kuboreka kwa huduma za maabara baada ya ununuzi wa mashine za kisasa za maabara na kuanza kwa mradi wa uzalishaji wa vyungu vya kuyeyushia sampuli za dhahabu kwa lengo la kuuza.

**b) Tume ya Madini**: Kuongezeka kwa mapato yatokanayo na madini ujenzi na madini ya viwandani; uingizaji wa madini katika masoko ya madini nchini kutoka nchi nyingine; kuboreshwa kwa mfumo wa usimamizi na ukusanyaji wa maduhuli; na kudhibiti kikamilifu biashara haramu ya madini inayohusisha utoroshaji wa madini.

**c) STAMICO**: Kupata ongezeko (*extension of an addendum*) la kufanya uchorongaji zaidi katika Mgodi wa Dhahabu wa Geita (GGM) na Buckreef; kununua mitambo nane (8) mipya ya uchorongaji; na kuongeza uzalishaji katika mradi wa *coal briquette* kwa kuagiza mitambo miwili ya kuzalisha tani 20 kwa saa kila mtambo.

**Kielelezo Na. 6: Ulinganisho wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na 2022/2023**


| **Maduhuli ya kuwasilishwa Hazina** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **CHANZO** | **2021/2022** | **2022/2023** | **ONGEZEKO** | **ASILIMIA** |
| **WIZARA** | 10,002,000 | 10,002,000 | - | - |
| **TUME YA MADINI** | 650,000,000,000 | 822,018,203,000 | 172,018,203,000.0 | 26 |
| **Jumla Ndogo** | **650,010,002,000** | **822,028,205,000** | **172,018,203,000.0** | **26** |
| **Maduhuli ya kutumika na Taasisi** | | | | |
| **CHANZO** | **2021/2022** | **2022/2023** | **ONGEZEKO** | **ASILIMIA** |
| **STAMICO** | 45,362,835,564 | 69,000,000,000 | 23,637,164,436.0 | 52 |
| **GST** | 889,035,100 | 2,000,800,000 | 1,111,764,900.0 | 125 |
| **TGC** | 180,000,003 | 201,675,000 | **21,674,997.0** | 12 |
| **Jumla Ndogo** | **46,431,870,667** | **71,202,475,000** | **24,770,604,333.0** | **35** |
| **JUMLA KUU** | **696,441,872,667** | **893,230,680,000** | **196,788,807,333.0** | **28** |

***Chanzo:Randama ya Wizara 2022/2023 na Usanifu wa Kamati***

### 2.2.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi Mwaka wa Fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara ya Madini **(Fungu 100)** inakadiria kutumia jumla ya **Shilingi 83,445,260,000.00.** Kati ya Fedha hizo **Shilingi 40,835,660,000.00** sawa na **asilimia 49** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Wizara, **Shilingi 20,609,600,000.00** sawa na **asilimia 25** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zake na **Shilingi 22,000,000,000.00** sawa na **asilimia 26** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ambazo zote ni fedha za ndani, kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 7.

**Kielelezo Na. 7: Mchanganuo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**




**Chanzo: Randama ya Wizara 2022/2023 na Usanifu wa Kamati**


**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi kwa kulinganisha bajeti ya Wizara kati ya Mwaka wa Fedha 2021/2022 na 2022/2023 na imebaini kwa ujumla bajeti imeongezeka kwa **asilimia 24.9** kutoka **Shilingi 66,816,467,000.00** Mwaka 2021/2022 hadi kufikia **Shilingi 83,445,260,000.00** Mwaka 2022/2023. Ongezeko zaidi linaonekana katika maeneo yafuatayo:-

a) Miradi ya Maendeleo kutoka **Shilingi 15,000,000,000.00** Mwaka 2021/2022 hadi kufikia **Shilingi 22,000,000,000.00** Mwaka 2022/2023 sawa na ongezeko la **asilimia 46.7.**

b) Matumizi Mengineyo yameongezeka kutoka **Shilingi 33,335,660,000.00** hadi kufikia **Shilingi 40,835,660,000.00** sawa na ongezeko la **asilimia 22.5**

c) Mishahara kutoka **Shilingi 18,480,807,000.00** hadi kufikia **Shilingi 2,128,793,000.00** sawa na ongezeko la **asilimia 11.5** kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 8. **Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kuona umuhimu wa kuendelea kuongeza bajeti ya Wizara hii yenye mchango mkubwa katika Pato la Taifa.**

**Kielelezo Na. 8: Ulinganisho wa Bajeti Kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na 2022/2023**




**Chanzo: Randama ya Wizara 2022/2023 na Usanifu wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua zaidi kwa lengo la kufahamu ni katika maeneo gani ongezeko la fedha za Miradi ya Maendeleo inaenda na ilielezwa kuwa fedha hizo zinaenda katika Taasisi mbalimbali kama STAMICO kununua mitambo miwili maalum ya uchorongaji kwa lengo la kuimarisha huduma kwa wachimbaji wadogo na kuendeleza Mradi wa Makaa ya Mawe ya Kupikia (*Coal Briqquette*); GST Kununua vifaa vya jiosayansi; na TGC kwa ajili ya upanuzi wa miundombinu na kukiendeleza kituo.

### 2.2.4 Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haikuishia hapo ilifanya uchambuzi zaidi kwa kulinganisha Mapendekezo ya Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2022/2023 dhidi ya BajetI Kuu ya Taifa na kubaini kuwa, Bajeti ya Wizara ni **asilimia 0.20** ya Bajeti Kuu ya Taifa. Aidha, bajeti hii imeongezeka kutoka asilimia 0.18 katika Mwaka wa Fedha 2021/2022. Ongezeko zaidi linaonekana katika Fedha za Matumizi Mengineyo (OC) kutoka **asilimia 0.80** hadi kufikia **asilimia 0.91** na Miradi ya Maendeleo kwa fedha za ndani kutoka **asilimia 0.14** hadi kufikia **asilimia 0.18** kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 9**. Kamati inaendelea kuipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza Bajeti ya Wizara hii muhimu yenye mchango mzuri kwenye uchumi wa nchi.**

**Kielelezo Na. 9: Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti Kuu ya Taifa 2021/2022 na 2022/2023**

| AINA | BAJETI TAIFA | BAJETI MADINI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| OC | 4,189,190,000,000.00 | 33,335,660,000.00 | 0.80 |
| MISHAHARA | 8,155,090,000,000.00 | 18,480,807,000.00 | 0.23 |
| MAENDELEO NDANI | 10,722,989,000,000 | 15,000,000,000 | 0.14 |
| MAENDELEO NJE | 4,254,626,000,000 | 0 | - |
| DENI LA SERIKALI | 10,663,278,000,000.00 | 0 | - |
| **JUMLA** | **37,985,173,000,000.00** | **66,816,467,000.00** | **0.18** |
| **ULINGANISHO WA BAJETI TA WIZARA DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2022/2023** | | | |
| **AINA** | **BAJETI TAIFA** | **BAJETI MADINI** | **ASILIMIA** |
| OC | 4,493,500,000,000.00 | 40,835,660,000.00 | 0.91 |
| MISHAHARA | 9,740,800,000,000.00 | 20,609,600,000.00 | 0.21 |
| MAENDELEO NDANI | 12,122,100,000,000 | 22,000,000,000 | 0.18 |
| MAENDELEO NJE | 3,399,200,000,000 | 0 | - |
| DENI LA SERIKALI | 11,308,400,000,000.00 | 0 | - |
| **JUMLA** | **41,064,000,000,000.00** | **83,445,260,000.00** | **0.20** |

**Chanzo: Taarifa ya Mapendekezo ya Mfumo wa ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2022/23 na Randama ya Wizara ya Madini 2022/23**

**2.2.5 Uchambuzi wa Ujumla kuhusu Sekta ya Madini**

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wa Bajeti ya Wizara na Taasisi zake masuala mbalimbali yafuatayo yalibainika:-

**a) Mkakati wa Kuendeleza Madini (*Mining Development Strategy*)**

**Mheshimiwa Spika,** Ili nchi iweze kunufaika ipasavyo na Rasilimali ya Madini, suala la kuwa na Mkakati wa kuendeleza madini hayo (*Mining Development Strategy -MDS*) ni la muhimu sana. Kamati inatambua bado nchi yetu haina Mkakati huo na katika vikao vya uchambuzi wa bajeti Kamati ilihoji suala hili na kuarifiwa kuwa Wizara ipo kwenye Mchakato wa kuandaa. Katika kuchambua, Kamati imepitia Mikakati ya Kuendeleza Madini ya nchi na maeneo mbalimbali kama vile Ontario (*Ontario's Mineral Development Strategy*)[9], Northwest (*Northwest Territories Mineral Development Strategy*)[10] na Yukon (*Yukon Mineral Development Strategy*)[11] na kuona namna zilivyojipanga katika kuhakikisha rasilimali ya madini inakuwa na manufaa kwa ustawi wa wananchi lakini pia kunakuwa na mazingira mazuri ya uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** Ikumbukwe kuwa Mkakati wa Kuendeleza Madini unasaidia Taifa kutambua kiasi cha madini ambacho nchi imebarikiwa lakini pia kuweka mipango na mikakati maduhubuti pamoja na kuwajibika ili kuhakikisha rasilimali inakuwa endelevu na inatumika kwa ustawi wa wananchi na Taifa kwa ujumla. **Kamati inaona ipo haja ya Serikali kupitia Mkakati wa Kuendeleza Madini wa nchi mbalimbali hususan zilizofanya vizuri ili kuweza kuiga yale mazuri kulingana na mazingira ya nchi yetu.**

[9] https://www.mndm.gov.on.ca/sites/default/files/mndm_mds_english_2015.pdf
[10] https://www.iti/gov/nt.ca/sites/iti/files/nwt_mineral_development_strategy.pdf
[11] https://yukon.ca/sites/yukon.ca/files/emr/emr-yukon-mineral-development-strategy-recommendations.pdf

**b) Ukomo wa Matumizi ya Makaa ya Mawe katika uzalishaji wa umeme**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kuwa nchi yetu ina rasilimali ya kutosha ya Makaa ya Mawe ambayo kiuhalisia bado hayajatumika kikamilifu. Kamati pia inatambua kuwa Sera ya Dunia na hususan Mkataba wa Paris wa Mwaka 2015 (*The Paris Climate Agreement, 2015)* ni kuhakikisha makaa ya mawe ambayo ni chanzo cha nishati chenye kaboni nyingi zaidi kinafikia ukomo wa matumizi ikiwa ni hatua muhimu ya kufikia upunguzaji wa hewa chafu ili kupunguza ongezeko la joto duniani hadi 1.5°C.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Taasisi ya *Climate Analytics* kupitia Ripoti Maalumu ya *Global and Regional coal phase-out requirements of the Paris Agreement: Insights from the IPCC Special Report* ya Septemba 2019 inaonesha kuwa, makaa ya mawe yanayotumika katika uzalishaji wa umeme yanachangia kwa kiasi kikubwa katika kutoa hewa chafu ambayo ni hatari kwa mazingira. Mojawapo ya mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti hiyo ni kuwa kutokana na ukweli kuwa tayari zipo teknolojia zinazoweza kuchukua nafasi ya makaa ya mawe, awamu ya kumaliza matumizi ya makaa ya mawe imeonekana ni chaguo nafuu na rahisi kupunguza uzalishaji. Ripoti hiyo pia imesema kutokana na utafiti uliofanyika, inaonesha kuwa makaa ya mawe yanahitaji kukomeshwa duniani kote kufikia 2040 ili kutimiza ahadi zilizotolewa mjini Paris[12] kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 10.

**Mheshimiwa Spika,** naomba ninukuu matokeo ya utafiti huo **"***Based on regional pathways for the five regions considered by the Special Report on Global Warming of 1.5°C by the Intergovernmental Panel on Climate Change (IPCC SR1.5), the main findings are"*

[12] https://climateanalytics.org/mediareport_coal_phase_out_2019.pdf

- *Regardless of the region, coal use for power generation needs to peak by 2020, and be reduced quickly afterwards;*

- *Unabated coal-fired power generation globally should be reduced to 80% below 2010 levels by 2030 and phased out before 2040, some 10 years earlier than previous estimates;*

- *Most reductions in coal in the power sector need to happen by 2030, when the share of coal in electricity generation should not exceed 13% anywhere, and be around 6% globally; and*

- *Between 2030 and 2040 all the regions should phase out of coal. The first regions to phase out are the OECD, Eastern Europe and Former Soviet Union countries - by 2031, followed by Latin America by 2032, Middle East and Africa by 2034, and finally non-OECD Asia by 2037, completing a global coal phase-out before 2040.*

| Region | Phaseout Date |
|---|---|
| OECD | 2031 |
| Non OECD Asia | 2037 |
| Latin America | 2032 |
| Middle East and Africa | 2034 |
| Eastern Europe and Former Soviet Union | 2031 |

**Chanzo: *Climatic Analyst Journal, 2019***

**Mheshimiwa Spika**, kama nchi bado hatujatumia rasilimali hii ipasavyo. Tanzania ikiwa ni moja ya nchi za Afrika inatarajiwa kufikia 2034 iwe imesitisha matumizi yake.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi huo na yale yaliyobainika katika Uchambuzi wa Bajeti, Kamati inatoa Maoni, Ushauri na mapendekezo yafuatayo:-

### 3.1 Maoni ya Jumla

a) Kutokana na maeneo mengi yenye uzalishaji wa madini kuwa na miundombinu isiyokidhi mahitaji. **Kamati inashauri kuwa, miundombinu na hususan barabara za maeneo ya migodi kama barabara ya Kiwira- Kabulo iboreshwe ili ziweze kupitika wakati wote;**

b) Ili kuendana na Mkakati wa dunia wa kuhakikisha inasitisha matumizi ya Makaa ya mawe ( *phase coal out of the electricity sector in line with the 1.5°C in the Paris Agreement*) Wizara iandae ***Coal Utilization Master Plan*** kwa haraka ili makaa ya mawe yaanze kutumika ipasavyo kabla kufikia ukomo 2034;

c) Ni vyema ujenzi wa Vituo vya Umahiri ukafanyika kwa kutumia mfumo wa *Force ccount* ili kupunguza gharama bila kuathiri ubora unaotakiwa; na

d) Ili nchi iweze kunufaika na rasilimali ya madini, Wizara iharakishe uandaaji wa Mkakati wa Kuendeleza Madini (*Mineral Development Strategy*) kama nchi nyingine zilivyofanya.

### 3.2 Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)

**Mheshimiwa Spika**, katika utendaji wa STAMICO,Kamati inashauri yafuatayo:-

a) Uzalishaji wa Makaa ya mawe ya kupikia (*Coal Briquette*) uwe wa kibiashara na uanze kwa haraka hasa katika Mikoa ya Pwani na Songwe kama ilivyopangwa;

b) STAMICO iendelee kuongeza juhudi katika kulipa madeni ambayo STAMIGOLD inadaiwa kwa kuwa kati ya **Shilingi Bilioni 21.032** ni shilingi **Bilioni 1.14** pekee zimelipwa kufikia Februari, 2022. Aidha, Serikali ione namna ya kuchukua deni hilo ili wazabuni waweze kupata haki na utaratibu ufanyike ili STAMICO iweze kuilipa Serikali taratibu;

c) STAMICO iwezeshwe kimtaji ili kuweza kuendeleza Mgodi wa Kigodi. Aidha, kwa siku za mbele ione namna ya kuingia ubia na wawekezaji;

d) Uunganishaji wa Mgodi wa STAMIGOLD Bulyanhulu katika Gridi ya Taifa ukamilike ili kupunguza gharama za uzalishaji kwa mgodi kutokana matumizi ya mafuta ya dizeli katika kuendesha mitambo; na

e) Wizara ione umuhimu wa kutoa kipaumbele katika uzalishaji wa madini ya chumvi kupitia STAMICO hasa ikizingatiwa kuwa uwekezaji wake ni mdogo lakini wenye faida na tija kubwa.

### 3.3 Tume ya Madini

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na umuhimu wa Tume ya Madini katika kuhakikisha mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa. Kamati inashauri:-

a) Mgawanyo wa fedha za Matumizi Mengineyo (OC)uendane na ukubwa wa kazi katika kila Mkoa zilipo Ofisi za Madini hii itasaidia katika kuisimamia sekta kwa uchumi wa Taifa letu;

b) Kamati inarudia ushauri ambao iliutoa Mwaka 2020 kuhusu wajibu wa Makampuni ya Uchimbaji katika Jamii inayowazunguka. Bado baaadhi ya Makampuni yamekuwa hayatimizi wajibu wao kikamilifu na hivyo kudhorotesha mahusiano na jamii. **Ni Rai ya Kamati kuwa suala hili lisimamiwe kikamilifu ili kuboresha mahusiano kwa mustakabali mzima wa ukuaji wa Sekta;** na

c) Tume ifanye mapitio ya Leseni na kama itabainika kuwa zip hazifanyi kazi basi zigawiwe kwa watu wengine watakaoweza kuzifanyia kazi/kuwekeza ili Serikali kuendelea kupata mapato yake.

### 3.4 Wakala wa Jiolojia Nchini (GST)

a) Wizara ione namna ya kuunda Bodi ya Usajili ya Wajiolojia (*Gelologist Registration Board*) kama ilivyo kwa wanasheria ili kusimamia taaluma hii muhimu nchini;

b) Utafiti wa Rasilimali madini tulizonazo ni jambo la muhimu sana. Kamati imebaini kuwa Sera ya Madini ya 2009 bado haijaeleza vizuri umuhimu wa kufanya utafiti. Ipo haja ya kujipanga kwa kuirejea Sera hii ili kuweza kufanya utafiti na kujua rasilimali tulizonazo hivyo kuenda sambamba na dunia ambayo inatumia akili mnemba (*artificial intellegency*) kufanya tafiti zake;

c) GST iwezeshwe kutekeleza majukumu yake muhimu ikiwa ni pamoja na kuongezewa watumishi wenye taalum maalum (*Rare professionals*), kuboroshewa miundombinu ya utafiti na kuongezewa bajeti kwaajili ya kufanya utafiti ili kuendeleza ya Sekta.; na

d) Uundwe Mfuko Maalum wa GST ambao utachangiwa na vyanzo mbalimbali kwaajili ya kusaidia Wakala kufanya utafiti endelevu.

### 3.5 Taasisi ya Uhamasishaji, Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI)

a) TEITI iharakishe kuanzisha Kanzidatat (*Database*) ya wamiliki wa Migodi kwa maslahi mapana ya nchi;

b) TEITI iwezeshwe kifedha ili kuweza kusimamia kikamilifu jukumu lake la kuhakikisha kuwa mapato yanayotokana na rasilimali madini, mafuta na gesi asilia yanahakikiwa na kutumika kwa manufaa ya wananchi wote; na
c) Kamati ya TEITI ambayo ndiyo ina wajibu wa kutekeleza majukumu ya Taasisi iundwe haraka.

### 3.6 Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC)

Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga **Shilingi Bilioni 7** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya TGC. Kamati inasisitiza Miradi hii isimamiwe kikamilifu ili iweze kutekelezwa kama ilivyopangwa kwa maslahii mapana ya nchi.

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine napenda kuchukua fursa huu kukushukuru sana Spika wetu Mhe. DKt. Tulia Ackson (Mb), Naibu Spika Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb) na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini kwa ushirikiano wao wakati wa kutekeleza majukumu ya Kamati na kushiriki vizuri katika uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dunstan Luka Kitandula, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb – M/Mwenyekiti
3. Mhe. Alaudin Hasham Salim, Mb
4. Mhe. Amina Bakari Yussuf, Mb
5. Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb
6. Mhe. Hamis Mwagao Tabasam, Mb
7. Mhe. Iddi Kassim Iddi, Mb
8. Mhe. Jesca David Kishoa, Mb

9. Mhe. Jesca Jonathan Msambatavangu, Mb
10. Mhe. John Marko Sallu, Mb
11. Mhe. Juliana Didas Masaburi, Mb
12. Mhe. Katani Ahmad Katani, Mb
13. Mhe. Kenneth Ernest Nollo, Mb
14. Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb
15. Mhe. Dkt. Mathayo David Mathayo, Mb
16. Mhe. Mussa Omari Salim,Mb
17. Mhe. Musukuma Joseph Kasheku, Mb
18. Mhe. Nicodemas Henry Maganga, Mb
19. Mhe. Nusrat Shaaban Hanje, Mb
20. Mhe. Saada Mansour Hussein, Mb
21. Mhe. Robert Chacha Maboto, Mb
22. Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya, Mb
23. Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb
24. Mhe. Ameir Abdallah Ameir, Mb
25. Mhe. Josephine Johnson Genzabuke, Mb
26. Mhe. Mohamed Said Issa, Mb
27. Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara, Mb

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru sana Waziri wa Madini Mhe. Dotto Mashaka Biteko(Mb) na Naibu Waziri Mhe. Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa (Mb) pamoja na Watendaji wote wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndg. Adolf Ndunguru kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiutoa kwa Kamati wakati wote.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Joyce Mwihambi (*ndc*). Namshukuru pia Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Brambat Hussein (*ndc*) na Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Sehemu inayosimamia Kamati yetu Ndg. Mswige Dickson Bisile kwa ushirikiano na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yetu bila mkwamo. Kipekee zaidi nawashukuru sana Makatibu wa Kamati Ndg. Pamela Pallangyo, Ndg. Onesmo Laulau na Ndg. Hosiana John na Msaidizi wa Kamati Ndg. Rukia Shaban kwa uratibu mzuri wa

shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha Taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini (Fungu 100) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja .
**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Dunstan Luka Kitandula
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI**
29 APRILI, 2022

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti kwa Wasilisho hilo kwa niaba ya Kamati, tunakushukuru sana Mheshimiwa Seif Gulamali.

Waheshimiwa Wabunge kuna orodha hapa ya wachangiaji kabla sijaanza hii orodha kuna wageni naambiwa wengine wameongezeka wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo wageni 100 kutoka Chuo cha Mipango Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wageni kutoka Arusha wa Mheshimiwa Hussein Nassor Amar naambiwa wengine walikuwa hawajafika sasa wasimame wote kwa pamoja, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninayo hapa majina ya Wabunge wanaotaka kuchangia, kwa hivyo tutaanza uchangiaji wetu, tutaanza na Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo na Mheshimiwa Qwaray ajiandae.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kushukuru sana kwa kupata fursa ya kuweza kuchangia na kutoa mchango wangu wa mawazo kwenye Wizara hii ya Madini. Nitajielekeza kwenye maeneo matatu;

moja, kwenye dhana ya kuhamisha madini ya *tanzanite* kwenda Mererani; pili, changamoto zake halafu; na tatu, kwenye mapendekezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dhana nzima ya kuondoa madini ya *tanzanite* na kutaka yauzwe Mererani peke yake inahusisha maeneo mawili. Eneo la kwanza, utoroshaji na kwenye utoroshaji wa madini sina mashaka kabisa kwa sababu kwenye eneo la Mererani ambako Serikali imejenga ukuta ndio eneo ambalo kuna ulinzi wa uhakika, kuna vyombo vyote vya ulinzi na usalama, kuna Jeshi la Wananchi, kuna Usalama wa Taifa, kuna TAKUKURU, kuna Polisi na kuna Wizara yenyewe ya Madini. Kwa hiyo, dhana ya utoroshaji na changamoto hiyo kwa muktadha wa Mererani haipo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasi hatutaki madini haya yauzwe Arusha peke yake, tunataka yauzwe Mererani, Arusha, Mwanza, Zanzibar na kwenye masoko yote ambayo yapo kwa mujibu wa sheria ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa changamoto; tuna changamoto ambazo tumezipata kutokana na maamuzi hayo ya Serikali. Changamoto ya kwanza, mapato ya Serikali yameshuka. Kabla ya maamuzi haya, kipindi kama hiki tulikuwa tunapata kiasi cha Shilingi bilioni 1.3 kwenye Soko la Madini la Arusha. Hiyo ni kwa madini yote, lakini kwa *Tanzanite* peke yake ilikuwa ni shilingi milioni 800. Leo tumepeleka Mererani kipindi kama hicho tunapata shilingi milioni 339. Kwa hiyo, changamoto ya kwanza Serikali imepata hasara, tumepoteza mapato.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya pili, katika Soko la Madini la Arusha, tuna maeneo kama *NSSF, PSSF* na *AICC* ambayo ni majengo ya Serikali. Serikali ilikuwa inapata kodi kupitia wafanyabiashara ya madini, ambapo kwa mwezi tulikuwa tunapata shilingi milioni 128. Hadi kipindi cha sasa tumepotezza kiasi cha shilingi bilioni 1.152 ya pango kwenye taasisi hizi za Serikali. Kwa hiyo, unaona maamuzi haya

tuliyoyafanya yametuletea changamoto kubwa ya kukosa mapato kwa pande zote.

Mheshimiwa Spika, pia tuna changamoto kwenye upande wa ajira. Tumekosa ajira 403 kwa wale ambao wote ambao walikuwa wanafanya biashara hizo kwenye masoko yetu ambayo yapo hapa. Tumepata changamoto kwa ma-*broker* wetu; ma-*broker* 2,500 mpaka 300 wamepata changamoto kubwa sana kwa sababu asilimia karibu 80 ya madini yanayouzwa kwenye masoko ya Arusha yanatokana na *Tanzanite.*

Mheshimiwa Spika, pia tulikuwa na mashine 427 kwenye Soko la Madini la Arusha, sasa hivi Mererani zimekwenda mashine 48 tu ambayo ni sawa sawa na asilimia kama 11.24. Kwa hiyo, unaona mashine ambazo zimebaki hazitumiki watu wamekosa ajira kwenye maeneo hayo, lakini pia na changamoto nyingine nyingi kwa mapana yake.

Mheshimiwa Spika, kutaka tu madini ya *Tanzanite* yauzwe Mererani peke yake, una-*monopolize* soko lenyewe, inasababisha kushuka kwa thamani, kwa sababu kunakuwa hakuna ushindani. Leo ukiuza madini Mererani, ukiuza Arusha, ukiuza Mwanza, ukiuza Zanzibar na maeneo mengine ya Tanzania, itasaidia sana kwa wafanyabiashara hao kushindana kutafuta wanunuzi nje ya nchi na mwisho wa siku faida itakuwa ni kubwa zaidi na mapato pia yataweza kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, pia kitendo cha kuruhusu wageni kutoka nje ya nchi kwenda moja kwa moja Mererani kununua madini, kwanza ni hatari kwa usalama wa nchi yetu, lakini pia inaondoa fursa kwa watu mbalimbali walio katika nchi ya Tanzania kuweza kunufaika na madini hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, baada ya kusema hayo, nilikuwa na mapendekezo yafuatayo kwa Wizara yetu ya Madini na Serikali kwa ujumla. La kwanza, sisi hatuna tatizo kabisa, tunataka Serikali ikusanye kodi na tunataka kodi zote

zilipwe pale Mererani; walipe kama ni mrabaha, *inspection fee,* baada ya kulipa kama ambavyo wanaruhusiwa leo, wakishalipa wapeleke madini yao India, Marekani na maeneo mengine, waruhusiwe pia kupeleka na Tanzania kwa sababu ni sehemu ya dunia ambayo inachanganya Arusha, Mwanza, Zanzibar, na Mererani kwenyewe.

Mheshimiwa Spika, tunao mfano, tuna madini kama haya yanaitwa *pink ruby* ambayo yanapatikana kule Thailand peke yake. Madini haya yanayopatikana kule pamoja...

*(Hapa kengele ililila kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, naamini hiyo ni kengele ya kwanza.

**SPIKA:** Kengele ni moja tu. Malizia sentensi yako.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, tunaamini kwamba madini haya yakiruhusiwa kuuzwa kwenye masoko mbalimbali itatusaidia sana.

Kwanza yatatoka kwa mchimbaji, yatakwenda kwa *broker,* baadaye yatakwenda kwa *dealer* na baada ya hapo yataongeza mzunguko ndani ya nchi yetu na pia yatafika huko duniani.

Mheshimiwa Spika, pia tunaomba...

**SPIKA:** Ahsante sana. Muda wako umeisha.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** ...tuweze pia kuanzisha maonesho ya madini, ili madini yetu haya ya *Tanzanite* na madini mengine tuwe na maonesho yake pale Arusha, dunia nzima iweze kuyaona, na mwisho wa siku iweze kutusaidia kuitangaza Tanzania, na kuleta watalii ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, kwenye kumalizia…

**SPIKA:** Mheshimiwa Gambo, sasa nimeshakwambia umalizie sentensi, umeongeza hoja nyingine, nimekusikiliza, sasa naomba ukae, tayari. Ahsante sana, shukrani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, ajiandae.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nadhani nina dakika kumi, kwa hiyo, nitakuwa na kengele mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni hivi, kwanza kabisa huyu Mbunge ambaye amemaliza kusema nitumie dakika yangu moja kuwasaidia wanaopanga mambo ya madini. *Tanzanite* tulijaribu kuweka *Centre* kubwa iwe Arusha na tukaweka mitambo ya kuchonga na kuongeza thamani. Sasa ukisema madini yale yasiende Arusha, basi ile mitambo ya *gemology* yote inakuwa *redundant.* Ni hilo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa kwanza kabisa kwenye hii Wizara, naunga mkono tupitishe bajeti, wafanye kazi. Kama kawaida yangu, mimi natoa mawazo mapana zaidi. La kwanza ni kwamba, naomba hii Wizara ifanye kazi na Benki Kuu na tuweze kuanza kuwa na *gold reserves.* Maana ya kuwa na *gold reserves,* yaani kutunza dhahabu kwenye Benki Kuu yetu, kwa sababu kubwa tatu. Kwanza kunaimarisha sarafu yetu ya shilingi, halafu inasaidia mfumuko wa bei, na tatu ndiyo *reserve* ambayo inaaminika haina *risk* ya aina yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuthibitisha hiyo *point,* angalieni wakubwa duniani *reserves* walizonazo. Wa kwanza ni Mmarekani dunia nzima ana *gold reserve* tani 8,133; wa pili ni Mjerumani, ana *reserve* ya *gold* tani 3,359; wa tatu ni Italy;

wa nne ni France; wa tano ni Urusi, ana tani 2,302; na wa sita ni China, ana tani 1,948. Sasa hawa wakubwa ambao wana uchumi mkubwa, wanalinda uchumi wa nchi zao kwa kuwa na *gold reserves,* kwa nini sisi Tanzania tusifanye hivyo? Hilio ndilo pendekezo na ombi langu la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa linganisha na nchi zinazotuzunguka. Msumbiji ambao tunawazidi uchumi, wana *gold reserve* ya tani 3.94; Burundi ambao tunawazidi, *reserve* yao ni *0.03 tons;* Kenya ambao wanatuzidi uchumi, wao wana *reserve* ya *0.02 tons.* Kwa hiyo, ni kwamba kwa kuwa tunakuwa na *refinery* nzuri sana kule Geita ambayo tutaweza kufanya *purification* ya *gold* kufikia *99.99.* Kwa hiyo, ni muda muafaka sasa sisi kuwa na *gold reserves* zetu. Pendekezo langu la kwanza hilo.

Mheshimiwa Spika, la pili, tumeambiwa kwamba, baada ya *Covid* kuja sasa ndiyo tunapata takwimu sahihi. Wanasema uchumi ulishuka ukafika *4.8,* sasa tuko *4.9.* Ni lazima turudi *seven* twende *eight* na ikiwezekana *ten percent.*

Ndugu zangu Watanzania, uchumi usipokua kwa kadiri ya kiwango cha 8%, 10%, 10% na kuendelea hatuwezi kufuta umasikini nchini. Kwa hiyo, kitu kitakachotusaidia hapa ni kwenye sekta za uzalishaji muhimu; kilimo, uvuvi na ufugaji. Kingine ambacho kitatusaidia, ni lazima twende kwenye uchumi wa gesi, tupende tusipende, twende huko. Cha tatu, ni kwenye madini sasa. Haya Mheshimiwa Waziri ameyasema, sawa, tuendelee; ni dhahabu, vito na *gemstones,* lakini kwa miaka 20 inayokuja hapa duniani, madini yanayotakiwa hatujaanza kuyachimba sisi. Kwa hiyo, *geological survey* aliyokuwa anaiongea, tuipatie hii kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, *geological survey* ya Dodoma kabla ya mwaka 1961 wa Uhuru, ndiyo ilikuwa *geological survey* kubwa ambayo nchi nyingine walikuwa wanaleta watu wao kufanya mafunzo hapa. Tuiwezeshe hiyo. *Geological survey* kwangu mimi ni muhimu kuliko hii Tume ya Madini, ni muhimu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa madini ambayo tunapaswa kuyashughulikia kwa ajili ya kutoka *4.9%* twende *8% economic growth rate,* twende *10%,* twende kwenye *helium.* Sikumsikia Waziri anaongelea *helium gas.* Hii gesi haiko Nishati. Kwa taratibu za nchi yetu, *helium* inasimamiwa na Wizara ya Madini, kama sijakosea. Sasa hivi hii *helium* ambayo iko nyingi huko Rukwa, *global demand,* duniani zinatumika *six billion cubic feet.* Duniani wanahitaji *six billion cubic feet of helium per annum* na *growth* yake itafika mpaka *10%. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka kesho soko la *helium* litakuwa na thamani ya *16 billion US Dollars* na mtumiaji mkubwa ni *NASA,* anatumia *100,000,000 cubic feet per annum.*

Kwa hiyo, naomba twende kwenye *helium* tuiendeleze. Hata hivyo, na yenyewe itakuwa kama ile ya *LNG* amabyo inabidi tuipeleke kwenye kimiminika *(liquid).* Tui-*liquefy* ile kule Lindi mpaka kwenye *temperature* ya *-161.5,* hiyo ni *LNG,* lakini *helium* ya Rukwa ni lazima tui-*liquefy* iende *-2.69 degrees celsius.* Haya siyo mambo ya mzaha. *Minus! (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa madini yanayohitajika duniani yatatumika kwenye magari, kwenye *aerospace, military, clean energy* na *fourth industrial revolution.* Wachina wamesema kufika mwaka 2025 wanataka kuachana na magari ya mafuta, wanahitaji madini. Madini ambayo yatahitajika kwa miaka 20 inayokuja, naomba niyataje; ni *cobalt, chromium... (Makofi)*

Aah, msipige makofi yasikike vizuri. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ni *cobalt, chromium, lithium, palladium, nickel, zink, manganese, gallium, germanium, indium.* Halafu na hii *platinum group elements* pamoja na *rea earth elements.* Kwa hiyo, naomba tukawekeze huko. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, madini mengine ambayo tunapaswa kuwekeza ni ya kutengeneza mbolea. Tunasema

mbolea, mbolea; *geological survey* ipewe kazi ya kutafuta madini mbali ya *natural gas,* lakini kuna madini mengine kama *potassium salts,* kama ile ya Minjingu Phosphate, ni kazi ya madini hii.

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho tunapaswa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili imeshagonga. Ahsante sana.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Spika, haya ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma na Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, ajiandae.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Wizara hii ya Madini. Kwanza kabisa nampongeza sana Waziri pamoja na timu yake kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii. Kwa niaba ya wananchi wote wa Mkoa wa Manyara namshukuru sana Rais, Mama yetu mpendwa, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia maombi ya soko la madini kubaki pale Mererani. Kwa nini tunasema kwamba, soko la madini libaki pale Mererani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati wanagawanya Mkoa huu wa Manyara kutoka Mkoa wa Arusha, waliangalia vigezo vingi sana na ndiyo maana Wilaya ya Simanjiro imeendelea kubaki Mkoa wa Manyara badala ya Mkoa wa Arusha kwa sababu kijiografia Wilaya yetu ya Simanjiro iko karibu sana na Mkoa wa Arusha, lakini waliangalia ni vigezo gani au ni shughuli gani za kiuchumi zinazoweza kubeba mkoa kwa mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wetu wa Manyara, mkoa wetu unabebwa na madini ya *Tanzanite;* mkoa wetu unabebwa na shughuli za kilimo; na mkoa wetu unabebwa na Hifadhi ya Wanyama ya Tarangire. Hivyo basi, busara ya Serikali ya Awamu ya Tatu chini ya Mheshimiwa Benjamin William Mkapa waliona kabisa ni muhimu suala zima la madini ya *Tanzanite* yabaki eneo la Manyara. Hivyo basi, tunaishukuru sana Serikali kwa kuendelea kubakiza soko hili katika eneo la Mererani na tunaendelea kuwaomba libaki pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Serikali ni kwamba, lile soko la eneo la *Tanzanite City* limeshatengwa, mfumo wa maji umekamilika, mfumo wa umeme umekamilika, barabara zimechongwa, lakini bado kazi ya ujenzi haijaanza. Kuna uzio umewekwa pale wa bati, lakini hayo mabati yameanza kudondoka. Tunaomba kujua, ni lini Serikali itaenda kuanza ule ujenzi mara moja ili kuwatoa hofu wafanyabiashara wa Mererani? Kwa hiyo, Waziri anapokuja kuhitimisha, naomba sana atueleze, ni lini ujenzi utaanza pale ili wafanyabiashara wafanye kazi zao wakiwa na matumaini makubwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, soko hili kuwa pale Mererani inatusaidia kuendeleza Mji wa Mererani, inasaidia vijana wengi kupata ajira pale Mererani, na kusaidia mapato makubwa kubaki katika Mkoa wa Manyara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la wageni kufika Mererani usalama wao umeboreshwa sana. Kwanza wageni wengi wanatua katika uwanja wa ndege wa *KIA* ambapo ni kilometa 20 tu kufika Mererani. Kwa hiyo, wafanyabiashara wa madini wa Mererani wanaendelea kuomba kwamba soko hili libaki pale, lakini Serikali itukamilishie mara moja ujenzi huu ili soko lile liweze kufanya kazi kwa ubora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi la pili. Wamama wengi katika eneo lile la Mererani wanajishughulisha sana na uchimbaji wa madini. Wako wamama wanamiliki migodi na wako ambao ni wachimbaji wadogo wadogo. Changamoto wanazokutananazo wamama hawa ni ukosefu wa mikopo.

Naiomba Serikali sasa ione namna ya kuwawezesha akinamama, wale wachimbaji wadogo wadogo ili waweze kujishughulisha kikamilifu na waweze kujikwamua kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini tunasema haya? Shughuli ya madini ya *Tanzanite* upatikanaji wake kwanza kwa sababu hawana vifaa vya kutambua kwamba eneo hili ndiyo kuna madini, hiyo inawakosesha wamama wengi wanapoteza hela nyingi wakiwa wanachimba yale madini halafu hawafanikiwi. Serikali ione namna ya kuwapatia vifaa na wataalam pamoja na mitaji ili wale wamama wanapochimba madini yale wawe na uhakika wa kupata madini na waweze kujinyanyua kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala la usafiri. Katika lile eneo la ukuta wa Mererani ambalo tunasema geti la Magufuli, tuna usafiri wa bodaboda mle ndani; tuna wamama ambao wanafanya biashara ya Mamantilie, tuna wamama ambao wanabeba matunda kichwani wakiwa wanaenda kuwauzia wachimbaji wadogo wadogo mle kwenye eneo la ukuta, lakini changamoto kubwa ni bodaboda zinazotumika mle ndani, wanalipishwa shilingi 2,000 kuwapeleka na shilingi 2,000 kurudi; wanapoingia tu getini, kitu ambacho kinasababisha wale akinamama wanashindwa kufanya zile biashara ili kujikwamua kiuchumi kwa sababu wanatumia zaidi ya Shilingi 8,000 hadi shilingi 10,000 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ione namna ya kuongea na wamiliki wa usafirishaji, yaani magari, ili magari yaruhusiwe kufanya kazi kule ndani ya ukuta; wamama hawa waweze kupata usafiri ili waweze kujikwamua kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, naiomba Serikali; kuna hawa wafanyakazi wa migodi ambao wanafanya mkataba kati ya wamiliki wa migodi pamoja na wale wafanyakazi wa migodi. Wale wafanyakazi wa migodi wana changamoto nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri hili anafahamu ni kwa namna gani wale wachimbaji wadogo wadogo ambao wanazama kwenye mashimo wanakosa haki zao za msingi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Muda umeisha?
Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Nassor Amar na Mheshimiwa Asia Abdulkarim Halamga, ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Wizara hii ya Madini mimi ni Mjumbe wa Kamati.Kwanza nianze kwa kumuunga mkono mjumbe aliyemaliza kuzungumza dadaangu tulivyopitisha hii Sheria ya kurudisha masoko kwenye maeneo husika sisi watu wa Geita ndiyo tulileta hiyo hoja humu mwaka 2017/2018 na Bunge lako Tukufu likatupitishia Sheria.

Mheshimiwa Spika, sisi watu wa Geita ni wanufaika namba moja, na watu wa Simanjiro ningewashauri waje wajifunze kwetu, kwasababu tunakusanya pale sokoni takriban bilioni tatu. Kwa hiyo ningeomba tu kila mtu amepewa neema tofauti, na Mheshimiwa aliyezungumza hii hoja aridhike maana ana utalii mwingi. Arusha ni sehemu ambayo ina utalii mwingi, tusioneane wivu tuache na hii miji midogo nayo ikue kwa kukusanya *Service Levy*.

Mheshimiwa Spika, suala la pili nilikuwa naomba kushauri kuhusiana na suala la *refinery.* Mheshimiwa Waziri anafahamu tumetengeneza *refinery* kubwa sana Geita pamoja na Mwanza na sisi Kamati tulienda kutembelea. Hata hivyo, ninaona kama tumewaingiza chaka wale waliowekeza

ile biashara pale. Kwa mwenendo tunaoenda nao sisi wazoefu wa ile biashara; ningependa Mheshimiwa Waziri unisikilize vizuri; hii dhahabu mpaka inaenda kwenye *refinery* unakuwa umeshatozwa mirabaha ya kutosha, wewe unafahamu; lakini ukifika pale ukishafanya tena usafi ule unatakiwa ulipe tena asilimia sita.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani kulipa asilimia sita ilhali hii dhahabu naweza kuibeba nikaenda nayo nje kule Dubai nikaisafisha kwa 0.25. Kwa hiyo ninaona kabisa kwamba kama mnaweza kuja na Sheria kidogo ya kibabe kwamba usisafirishe mpaka ufanyie hapa lakini hebu jiulize ungekuwa wewe ndiye mfanyabiashara. Kwa hiyo ningeomba Serikali ione namna ya kushusha hata kama ni asilimia mbili ikawa kivutio; na hizi ndizo *attachment* za *Royal Tour* ya Mheshimiwa Rais kwamba watu wanapokuja hapa waje wajifunze vitu vingi tusiweke bei kubwa watu wakawa tena watoroshaji tukaanza kukamatana na kunyang'anyana ni vizuri tukatembea tukaiga kwenye hizo nchi ambazo tayari zina *refinery* na watu wanapeleka kwenda kusafisha.

Mheshimiwa Spika, suala lingine, ninashauri Mheshimiwa Waziri turudishe suala la minada ya madini. Tunapofanya minada ya madini tutaingiza watalii wengi sana kuja kununua kwenye masoko, na tutangaze tuna madini ya aina gani. Watu watakuja, asiponunua dhahabu asiponunua madini atanunua hata kinyago naona tutakuwa tunaendelea kum-*support* Mheshimiwa Rais katika ile filamu yake ya *Royal Tour*. Twende mbali zaidi kwamba Mheshimiwa Rais hakuweza kumaliza kuvitembelea vivutio ambavyo viko kwenye nchi yetu. Tutakapofanya hii minada wazungu watakuja na watu wengine wageni tutapata kipato kikubwa zaidi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba suala la minada pia liweze kurudishwa.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine, nimesikia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kwamba ana mpango wa kufungua duka sijui la vilipuzi. Nilikuwa naomba sana kuishauri Wizara; unajua kwanza Shirika letu la *STAMICO* ndiyo kwanza linaanza kupanda lina madeni na uwezo wake ni mdogo;

biashara inatakiwa iachiwe watu wa *Private Sector* kwa sababu kwenye *Private Sector* sisi tunapeana kukopeshana ninaweza nikachukua kilipuzi au nikachukua *carbon* nakudai inabidi nikasubirie mpaka uchome.

Mheshimiwa Spika, sasa ninyi watu wa *procurement* sijui ugavi sijui vitu gani tunaenda kuziteketeza hizi hela wakati shirika lenyewe halijasimama tuiachie *private sector* ifanye hizi biashara kuliko kuingia kwenye vitu ambavyo naona hatutafanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine nataka nichangie, nalo ni kuhusu dhahabu inayopelekwa sokoni. Mheshimiwa Waziri upatikanaji wa dhahabu wewe umetoka kwenye mkoa wa dhahabu ninaweza kuwa hata natembea nikakaokota barabarani pakuuza ni sokoni. Sasa, nikifika sokoni kumeanzishwa mtindo, kwamb watu wako tena wanataka mpaka niwe na risiti nilikoitoa dhahabu. Sisi lengo letu ni dhahabu na nchi yetu kimataifa ina dhahabu ambayo haina matatizo kwa nini tuanze kuhojiana? Kwa nini tusiachie uhuru watu ambao pengine wanapata dhahabu kwa njia kama za kuokota iweze kuuzwa pale sokoni?

Mheshimiwa Spika, la mwisho, mimi natoka mkoa wa Geita sisi ndiyo wanufaika namba moja wa *CSR*. Nimemuona mkuu wa Mkoa wa Mara anafukuzana na Afisa Mahusiano kwa sababu ya kutokutekelezeka kwa miradi. Sisi watu wa Geita ni waathirika wakubwa sana kwenye miradi ya *CSR,* na kumekuwa na mabishano kati ya mgodi na halmashauri nakuomba Waziri utakapohitimisha ili nisichukue shilingi yako uniambie ni lini uko tayari tuwaite *GGM* kwako na sisi Baraza tuje kwako ili uje utuwekee msimamo mzuri ili kazi zikaweze kwenda kutekelezeka nashukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hussein Nassor Amar atafatiwa na Mheshimiwa Asia Abdulkarim Halamga, Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka ajiandae.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia. Kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma, lakini

pia nimpongeze Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ambayo anaendelea kuifanyia nchi hii. Lakini pia nimpongeze Waziri wa Madini Mheshimiwa Doto Biteko pamoja na timu yote.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, kutokana na muda nataka nitoe ushauri kidogo kwenye Wizara hii, ushauri wangu wa kwanza ni pamoja na kwamba *plants* nyingi nchini zinaliingizia Pato la Taifa, *plants* nyingi za *VAT reaching* zinalipatia Taifa mapato makubwa sana; ikiwemo Nyangh'wale ambayo tuna *plant* zaidi ya 100. Uchenjuaji huu una sababisha uharibifu wa mazingira. Ushauri wangu kwamba *plant* zote nchini ikiwemo na *plant* za Nyangh'wale Serikali ielekeze kwamba kila *plant* ipande miti zaidi ya 200 ili kuepusha majanga ya uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu wa pili Mheshimiwa Waziri Doto Biteko, uunde tume ili iweze kwenda kwenye mgodi wetu wa Bulyanhulu kufanya uchunguzi wa uchimbaji unaoendelea kule chini. Inasemekana kwamba uchimbaji huu umeelekea zaidi kwenye upande wa Nyangh'wale na siyo Kahama. Watakapobaini kwamba ni kweli uchimbaji huu unaelekea Wilaya ya Nyangh'wale basi tukae chini ili tuweze kurekebisha ushuru ambao tulikuwa tukipata. Kutoka kwenye asilimia 100 Msalala walikuwa wakipata 67 na Nyangh'wale tulikuwa tunapata asilimia 33. Iwapo sasa hivi uelekeo huo utakuwa unaelekea Wilaya ya Nyang'wale itabidi tubadilishe. kwamba sisi tuchukue 67 na Msalala wachukue asilimia 33.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu mwingine ni kwamba, Wizara imeruhusu uchimbaji unaoitwa uchimbaji wa *rash* maeneo mbalimbali nchini. Sasa kwenye uchimbaji huu wa *rash* pamejitokeza vikundi ambavyo vinasimamia kukusanya mapato yanayopatikana pale. Kumejitokeza pia vijana ama wananchi fulani wachimbaji wanaojiita wababe wachimbaji ambao wamekuwa wakizivamia zile ofisi za *rash* ambazo zinakusanya mrahaba wa mawe. Kwa mfano kikundi cha akina mama wachimbaji wadogo wadogo wa Nyangh'wale walivamiwa na kufanyiwa usumbufu mkubwa

sana na vijana hawa. Kwa sababu Serikali imeruhusu ofisi hizi zisimamie *rash,* ninakuomba Mheshimiwa Waziri utoe tamko utundu huo na ujeuri huo unaofanywa na hao vijana uachwe kabisa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nashukuru kwamba hawa akina mama baada ya kuvamiwa namshukuru sana DC wangu pamoja na RMO wamelishughulikia jambo hili na limekaa vizuri wale akinamama wanaendelea na shughuli zao. Hongera sana Mheshimiwa DC kwa kulimaliza tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu mwingine, ni kwamba kuna wachimbaji ambao wanapeleka *carbon* zao kutoka Nyangh'wale kwenda kuchomea Geita mji *carbon* hizo zinapochomwa Geita na dhahabu inapopatikana, imekuwa kodi zote zinachukuliwa na Geita mji ikiwa mrahaba wa Serikali lakini pia *service levy,* Wilaya ya Nyangh'wale tunakuwa hatupati *service levy* kwa sababu wametoka Nyang'wale wameenda kuchomea *carbon* zao Geita. Takriban zaidi ya milioni 800 zimeng'ang'aniwa na Mji wa Geita. Tunakuomba Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko lisimamie hili ili tuweze kurudishiwa hizo milioni 800 ziweze kuleta maendeleo katika Halmashauri yangu ya Wilaya ya Nyang'wale.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Doto Waziri wa Madini, mwisho kabisa, pesa hizi zimekuwa zikiombwa na zimeleta mgogoro sana. Ni kwanini wanaenda kuchomea Geita? Ni kwa sababu wale wachimbaji wanakuwa hawana uwezo wa kuendesha shughuli zao, wanakwenda kukopa kwa wale matajiri walioko Geita, sasa badala ya kuchomea mzigo huu Wilayani Nyangh'wale, wanabeba ule mzigo kuupeleka Geita wanapochomea. Geita kule kwa wale matajiri wanalipa zile ...

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kanyasu.

## TAARIFA

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, namheshimu sana Mheshimiwa Hussein na natambua mchango wake. Lakini, kwa mujibu wa sheria ya *service levy* inalipwa pale ambapo mfanyabiashara anafanyia biashara yake na kwamba Halmashauri ya Mji wamekuwa wakitoza hivyo kwa sababu sisi hatukuwafata Nyangh'wale wanakuja wenyewe nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar unapokea taarifa hiyo?

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, taarifa hii siipokei. Namheshimu sana mdogo wangu Kanyasu. Wale wanapochukua *carbon* zao Wilayani Nyangh'wale kwenda kuchomea Geita ni kwa sababu wanapewa mikopo na wale matajiri waliopo Geita. Lakini kwa sababu *address* ni kwamba ametoka Nyangh'wale tunaomba ile *service levy* irudi kwetu Nyangh'wale vinginevyo Mheshimiwa Waziri basi uweke zuio la watu kubeba *carbon* kutoka Nyangh'wale ziende Geita zisiende Geita hizo *carbon* kwa hiyo tunaomba utusaidie hilo; kwa sababu wachenjuaji wengi wanapeleka Geita kwa sababu wanaenda kukopa kule. Iwapo Mheshimiwa anasema kwamba ni sheria basi hebu kuiangalia hii sheria, tuweke zuio ili *carbon* isitoke Nyangh'wale ichomewe pale pale Nyangh'wale na isiende Geita.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Asia Abdulkarim Halamga atafatiwa na Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magesa ajiandae.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri ambazo anazifanya katika nchi yetu. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri Doto Biteko na timu nzima ya Wizara ya

Madini kwa namna ambavyo tunaona wanavyochapa kazi na kuhakikisha kwamba rasilimali hii muhimu katika Taifa inaendelea kuwa ni chanzo cha mapato kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza ndugu Fabian Mshai RMO wa Mererani pamoja na timu nzima ya watumishi Mererani. Pia niishukuru na kuipongeza Serikali kwa kuamua sasa soko la Tanzanite litoke Arusha na kuletwa Mererani wilaya ya Simanjiro katika mkoa wa Manyara. Vilevile nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuja kulizindua soko la madini katika mji wa Mererani Simanjiro ndani ya mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi za kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuja kufungua soko hilo niendelee kumshukuru na kumpongeza kwa uzalendo wake Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan katika kutengeneza filamu ya *Royal Tour* ambayo moja ya maeneo ambayo yalitumika ni pamoja na mji wa Mererani katika machimbo yanayochimbwa Tanzanite tunamshukuru kwa uzalendo wake kwa kutangaza tanzanite ulimwenguni kote kwa sababu wapo watu waliokuwa wakipotosha tanzanite haitoki Tanzania, tanzanite haitoki Manyara.

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kulinda urithi wetu, wa nchi yetu ya Tanzania kwa kuitangazia dunia tanzanite ni ya Tanzania tanzanite inatoka Manyara, tanzanite inatoka Mererani.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, iliamuliwa kwamba sasa soko lijengwe Mererani tunaomba mchakato wa ujenzi wa soko ufanyike kwa haraka kwa sababu tayari maamuzi ya viongozi wetu wakuu wa nchi yalishafanyika na walishatoa maagizo. Ujenzi huo utasaidia sana kurahisisha ajira kwa vijana wengi. Sasa, tunaomba Wizara ya Fedha sasa taratibu zote zimeshakamilika michakato yote imeshakamilika iliamuliwa kutolewa bilioni 5 lakini kwa kuanzia ilitakiwa itolewe fedha kiasi cha bilioni 20.

Mheshimiwa Spika, unapotetea maslahi ya mkoa unaotoka, unapotetea maslahi ya vijana kuna wakati mwingine kidogo ... naomba niendelee

*(Hapa Mheshimiwa Asia A. Halamga aliacha kuongea kwa muda mfupi)*

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Halamga nakutunzia dakika zako pumua kidogo kaa kidogo achangie Mbunge mwingine utarejea kumalizia hoja yako.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, naomba niendelee

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, naomba niendelee niko vizuri kijana wako.

**SPIKA:** Haya ahsante sana.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante Wizara ya Fedha inaendelea kutucheleweshea kutoa fedha hiyo, ambapo inatakiwa itoke bilioni moja kwa ajili ya kuanza ujenzi. Tunaomba Wizara ya Fedha wasikwamishe jitihada za Mheshimiwa Rais na hiyo fedha itoke ili ujenzi uanze. Lakini pia tunaipongeza Wizara kwa sababu baada ya soko hilo kukamilika kule ndani kuna package za mafunzo mbalimbali juu ya uchakataji wa madini pamoja na upandishaji thamani vito kwa ajili ya vijana. Hivyo itasaidia kuendelea kutoa fursa za ajira kwa vijana wetu wengi.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Manyara ni mkoa uliobarikiwa kwa madini, yako madini ya aina mbalimbali. Tuiombe Wizara sasa kuendelea kufanya utafiti kwa sababu tunayo madini ya *grafit* yako wilaya ya Hanang, tunayo madini ya *green garnet* yapo Mererani, tunayo *Mabel* kwa ajili ya *tiles* yapo Simanjiro, tunayo *gold* inayopatikana Basutu, tunayo madini Babati vijijini, tunayo madini wilaya ya Mbulu. Mkoa mzima wa Manyara umejawa na rasilimali hii muhimu katika nchi yetu, tuombe Wizara itoe hela ya tafiti.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kwa kumalizia tunaiomba Serikali, kile kinachotokana na madini tuombe Serikali irudishe fedha kwenye jamii kwa maana ya huduma za afya, barabara pamoja na maji. Lakini pia Mji wa *Tanzanite City...*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** ahsante naunga mkono hoja kwa asilimia zote. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Masache Kasaka atafuatiwa na Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magesa, Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi ajiandae.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami kupata nafasi niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Madini.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake, kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya kuhakikisha kwamba sekta hii ya madini inazidi kukua siku hadi siku. Pia niipongeze Wizara kwa kazi nzuri ambayo inaendelea kuifanya katika kuwawezesha wachimbaji wadogo ili waendelee kushiriki kwenye uchumi wa madini ambao unawawezesha kushiriki kwenye uchumi huu na katika kujitafutia riziki na kuweza kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, lakini wachimbaji wadogo hawa wameweza kuendelea na kuwezeshwa katika kupata maeneo ya kufanyia kazi, kupata ama kupewa leseni kwa maeneo ambayo yanaonekana yana madini. Lakini pia tuwapongeze Wizara kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wameendelea kuifanya katika kutoa semina mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo tumeona kwamba kazi nzuri inaonekana kufanyika, na kazi hii

inayofanyika na Wizara inasababisha hata maduhuli ya Serikali kuongezeka. Tukiangalia mwaka wa fedha uliopita kiasi cha fedha ambazo kiliingizwa na mwaka huu wa fedha zaidi ya asilimia nne zimeongezeka. Hii ni kazi kubwa sana na kwa hiyo Wizara maana imechangia kwenye Pato kubwa la Taifa.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na kazi kubwa hii nzuri inayoendelea kufanyika tunawapongeza pia Wizara kwa kuhakikisha kwamba wanaendelea kuzishirikisha taasisi za kifedha ambazo zimeonana na wachimbaji wadogo ili kuhakikisha kwamba wanapata mikopo midogo midogo itakayowawezesha kupata vifaa na vifaa hivi vinawawezesha wao kuweza kurahisishia uchimbaji wao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na taasisi za kifedha kuwapatia wachimbaji wadogo lakini bado masharti ya taasisi hizi yamekuwa magumu kuwawezesha wachimbaji wadogo hawa kuweza kunufaika. Tuiombe Wizara, pamoja na kwamba wameendelea kufanya kazi kubwa katika hili lakini pia waendelee kuongea na taasisi za kifedha hizi ili benki na taasisi nyingine walegeze haya masharti waliyonayo ili kuwawezesha wachimbaji wengi wadogo hasa wale wa chini kabisa waweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, leo hii wachimbaji wadogo ambao wananufaika ni wale ambao wanaweza wakapata *mascaveta*, *mabuldoza* pamoja na ma-*tipper,* yale makubwa.

Mheshimiwa Spika, leo hii wachimbaji wadogo ambao wananufaika ni wale ambao wanaweza wakapata ma-*excavator, bulldozer* pamoja na *tipper* kubwa, lakini tunataka tushuke chini zaidi kwa wale wachimbaji wadogo ambao wanaweza wakapata fedha ya kuwanunulia makarasha, wakapata fedha ya kujenga *plant* na vitu vingine kama hivyo ili mzunguko huu wa fedha uweze kwenda kwa wachimbaji wengi zaidi na wao pia waweze kujiwezesha kiuchumi waweze kulipa kodi zitakazoisaidia nchi yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo pamoja na kuwezeshwa huko wachimbaji lakini taasisi ya *GST* iendelee kufanyakazi yake kuhakikisha kwamba inaendelea kufanya tafiti hizi na tafiti hizi ziweze kushuka kwa wachimbaji wengi wadogo na walio wa chini.

Mheshimiwa Spika, leo hii tafiti nyingi ambazo zinafanyika zinaishia kwenye makabrasha ofisini ninaomba sana taasisi ya *GST* iweze kufanya kazi hii na ihakikishe inatohoa kwenye lugha nyepesi na rahisi ambazo zitaweza kuwafikia wachimbaji wetu wa kule chini, ziweze kufika kwenye ngazi za Mkoa, kwenye ngazi za Wilaya na wachimbaji wetu wa kule Nyang'hwale wachimbaji wetu wa Chunya, wachimbaji wetu wa Matundasi Sangapi na maeneo mengine waweze kuzipata hizi na waweze kunufaika pamoja na hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona taasisi ya *GST* ilichukua ushauri wetu, mwaka jana tuliwaambia hapa waanzishe maabara kwenda kwenye Mikoa yetu, nashukuru sana nimeona kwenye taarifa hapa maabara hizo sasa zimeanza kuanzishwa tumeona Geita kule zimefunguliwa maabara hizi. Ninaomba sasa Serikali kwa kuwa imeanza kufungua maabara hizi na sisi watu wa Nyanda za Juu Kusini, watu wa Mkoa wa Mbeya na hasa Wilaya ya Chunya ambako ndio wachimbaji wakubwa sana wa dhahabu tuhakikishe kwamba maabara hizi sasa zinaenda kuanzishwa haraka zaidi ili wachimbaji wetu hawa wapeleke sampuli zao pale, wawe na uhakika na kile ambacho wanaenda kukichimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo pia hata ule uchorongaji, nimeona hapa wameagiza mashine za uchorongaji, mashine hizi zitakapofika tuhakikishe kwamba zinaweza kuwafikia wachimbaji wetu hawa.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wengi wanachimba sasa hivi katika hali ya kubahatisha hasa wale wachimbaji wadogo, leo *GST* wanasema kwamba wanaboresha

kanzidata yao ya miamba ni jambo zuri sana, lakini kuboresha peke yake haitoshi! Waboreshe hizi kanzidata na taarifa hizi za miamba ziweze kuwafikia wachimbaji wengi wadogo, wachimbaji hawa watakapoweza kupata taarifa ambazo ni nzuri na sahihi ndivyo watakavyoweza kuongeza uzalishaji wao na wakiongeza uzalishaji wao ndivyo ambavyo wataweza kulipa kodi kwa Serikali na Serikali itazidi kupata mapato na tutaona nchi yetu itazidi kupaa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia ...
**SPIKA:** Sekunde thelathini.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, basi nitaleta mchango wangu kwa maandishi lakini ninapongeza na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, atafuatiwa na Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira ajiandae.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Madini. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii ya leo aliyonipatia ya kuzungumzia Madini, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na timu yake nzima wakiwepo wataalam kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, tunaona kabisa kwamba mchango wa sekta hii sasa kutoka asilimia 6.3 katika kipindi kama hiki tumekwenda kwenye asilimia saba inaonesha kwamba lengo la Serikali ambalo lilikuwa kwenye mpango mzima kwamba mwaka 2025 tuwe na asilimia 10 linaweza likafikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwasababu lengo ni hilo na inaonekana kasi ni kubwa ningeomba sasa tuzidishe sasa tuizidi hiyo asilimia 10 ili ionekane kabisa kwamba tumefanya kazi nzuri Zaidi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi nitoe ushauri wa Serikali kama mchangiaji Profesa Muhongo alivyosema dunia sasa ipo kwenye *energy transition,* hapa kwenye *energy transition* maana yake tunakwenda kwenye yale madini mkakati, *critical minerals* na dunia ya sasa inakwenda huko. Kwa hiyo, niwaombe sana *GST* ambao ninaona hapa wamepewa fedha kama Shilingi Milioni Mia Moja Arobaini na Tatu tu, tuangalie namna gani tunaweza tukawaongezea ili waweze kuingia kwenye kutafiti hayo madini ambayo dunia ya sasa inakwenda.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninaangalia hapa Canada wana madini mengi ambayo sitaki niyataje, ni karibu 34 yanaonekana hapa kwenye hizo *critical minerals*, kwa hiyo niwaombe sana *GST* na Wizara kwa ujumla iwasaidie sana *GST* ili waweze kupita kwenye utafiti huu.

Mheshimiwa Spika, niliona imetajwa kidogo kwenye madini ya mkakati, lakini bado haitoshi kwasababu dunia inakwenda huko. Kama tulivyosikia China wanataka kutoa magari nilikuwa ninaona *Research* moja inaonesha kabisa kwamba gari la umeme linaweza kutumia kama kilo 200 hivi, lakini gari ambalo litakwenda kutumia hizi *critical minerals* zitatumia kama kilo 40, niliona mtu mmoja amefanya *reseach* kama hiyo. Kwa hiyo, ningeomba sana tuwaelekeze hawa *GST* wafanye utafiti wa kutosha ili dunia inapokwenda kubadilika na sisi tubadilike pamoja nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nijikite sasa kumpongeza Waziri kwa leseni za wachimbaji wadogo 4,490 ambazo zinaonekana kwenye hotuba yake. Hizi hata kwenye Jimbo langu la Busanda kuna watu wamefaidika na leseni hizi lakini niishauri Serikali katika kuwasaidia wachimbaji wadogo nimeona kabisa inaonesha *STAMICO* wamepitia vikundi vitano, vikundi vitano ndani ya nchi hii kama ndiyo vinaenda kutathminiwa maeneo yao kuonekana kuna madini kiasi gani ni vichache sana, iwezeshwe *STAMICO* kuhakikisha kwamba inaweza kupitia vikundi vingi.

Mheshimiwa Spika, hapa vinaonekana kwenye Randama Ukurasa Na. 11, vikundi vitano tu vimepitiwa, navyo vinaonekana vimepita Kilindi, Morogoro na Singida, kule kwangu Busanda ina maana hawakupita kipindi chote hiki na kuna wachimbaji wadogo wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nijielekeze kuonesha kwamba katika wachimbaji wadogo tunaowazungumzia hawa wamekuwa wanasuasua katika kutambua mchanga au mawe kwamba yana dhahabu kiasi gani, na wamekuwa wanatumia maabara hizi za watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri mamlaka inayosimamia maabara hizi, watu wetu wamekuwa wanakwenda kupima *PPM* kiwango cha dhahabu kwenye udongo au kwenye mawe wanaambiwa hapa kunaonekana kuna 18 kumbe amedanganywa, anachukua mtaji mzima kuendelea kufanya kazi kwenye eneo hilo Milioni Mia Tatu, Milioni Mia Nne, akienda kusafisha chenjua anakuta Shilingi Themanini matokeo yake anapata hasara ambayo kwa kawaida inaweza kumpotezea maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mamlaka inayohusika na maabara hizi ihakikishe kwamba inazipitia kuzikagua ili wananchi wetu wahakikishe kwamba wanapata faida badala ya kupata hasara kwa sababu wamedanganywa na matokeo yaliyofanyika kwenye maabara hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme wazi kwamba yapo maeneo mengi ambayo yameendelea kumilikiwa na watu, hawa watu wenyewe ukiwatafuta kwenye maeneo yetu wanaonekana siyo wakazi wa maeneo hayo kwa sababu ni haki yao kupata maeneo hayo lakini wananchi wetu wanahitaji kuchimba. Ninaomba maeneo hayo ambayo sasa yanamilikiwa na hayafanyiwi kazi Wizara iyashughulikie kuhakikisha kwamba yanaweza kutaifishwa yakarudishwa mikononi mwa wananchi ili waendelee kufanya uchimbaji mdogo mdogo kwa sababu asilimia 35 ya wachimbaji wetu ni wachimbaji wadogo, nao wanachangia pato hilo la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe angalizo kwamba tunaweza tukaiona Wizara hii inachangia sana kwasababu bei ya dhahabu imepanda, niwaombe sana Wizara tuhakikishe kwamba majadiliano *negation teams* zifanye kazi kwa haraka kuongeza watu wanaoendelea kuwekeza kwenye sekta hii. Kwa mfano, tuna *special mining license* mbili tu, ukiziona zimekuja mbili zimekuja kipindi hiki lakini za kwanza ambazo *special mining license* tumekuwa nazo zimepatikana nafikiri mwaka 2000, 2002 na 2003 kwa hiyo tuna miaka karibu 15 hadi 20 ambayo tulikuwa hatujatoa leseni za hivi karibuni.*(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana Mheshimiwa Kengele imeshagonga.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira Mheshimiwa Constantine John Kanyasu ajiandae.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwanza kabisa niende moja kwa moja kutokana na muda na nikuombe ikikupendeza basi unaweza kuniongeza dakika tatu ili niweze kuwasilisha hoja mahsusi.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya, pia nimpongeze Kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakiri kwamba Mheshimiwa Waziri huyu anafanya kazi kubwa sana akisaidiwa na Naibu Waziri wake, na viongozi wote wa Tume pamoja na Wizara wanafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo nijikite kwenye ukurasa wa 32 ambapo Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake

amezungumzia juu ya suala zima la *CSR.* Nitajikita kwenye suala zima la *CSR* lakini nitajikita kwenye suala zima la *local content* na nitajikita kwenye suala zima la fidia ambazo zinaendele kwenye maeneo ambayo tunatoka kwenye migodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mgodi wa Bulyanhulu ni mgodi unaopatikana katika Halmashauri ya Msalala, mgodi huu au maeneo haya ni maeneo ambayo yanachangia kiasi kikubwa kwenye Pato la Taifa hapa Tanzania. Mheshimiwa Waziri ametuambia hapa ni takribani zaidi ya Shilingi Bilioni 16 ambazo zimetolewa kama fedha ya *CSR* katika maeneo yetu na Msalala ikiwemo.

Mheshimiwa Spika, niseme tuna mgodi pale unaitwa Bulyankhulu, mgodi huu upo katika Jimbo langu la Msalala pia mgodi huu upo katika Jimbo la Mheshimiwa Waitara. ninakiri kwamba mgodi huu umeendelea kutumia fedha vibaya za *CSR* ambazo Mheshimiwa Waziri amezitaja hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri ya Geita wanapokea kiasi cha Shilingi Bilioni 10 kama fedha ya *CSR* lakini Bulyankhulu na *North* Mara, Bulyankhulu tunapokea Bilioni 2.5 tu fedha ya *CSR*. Leo Mheshimiwa Waziri amezungumzia hapa kwamba fedha hizi zimeenda kujenga barabara, zimeenda kusambaza maji, zimeenda kujenga miundombinu ya elimu. Nikuhakikishie katika Jimbo langu la Msalala ambapo makinikia mengi yanachimbwa barabara hakuna.

Mheshimiwa Spika, utaona malori na Malori ya makinikia yakisafirishwa, vumbi kali wananchi wanapata taabu lakini hakuna tunachonufaika juu ya uwepo wa barabara. *(Makofi)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, kama ni taarifa nilinde utaniongezea dakika.

**SPIKA:** Muda hauongezeki nadhani tulishaambiana humu ndani, muda wa taarifa ni wewe unaongezewa kwenye mchango wako Mheshimiwa Tabasam.

**TAARIFA**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba nataka kumwambia mchangiaji kwamba katika hiyo *CSR* ya mgodi huo wa *Barrick* walitakiwa watengeneze barabara ya lami inaanzia hapo Kakola inakuja mpaka Busisi hawajatekeleza hilo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa hiyo naomba niendelee.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2000 na 2003 mgodi ya Bulyankhulu uli-*declare* kwamba ulitumia kaisi cha Shilingi Bilioni 50 kwenye miradi ya maendeleo kwenye maeneo yale, walitumia fedha zilezile za *CSR* kujenga nyumba za watumishi Bugarama na Ilogi.

Mheshimiwa Spika, *TRA* waliwasamehe kodi...

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wenyewe wa kuchangia ni mfupi sana kwa Mbunge sasa taarifa zikiwa nyingi yeye mwenyewe atakuwa hamalizi, Mheshimiwa Waitara.

**TAARIFA**

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge

kwamba kule Nyamongo waliahidi kujenga Chuo cha *VETA* chenye hadhi ya Wilaya tangu mwaka 1995, hawajajenga mpaka leo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa hiyo nikuombe uniongezee dakika tano. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, walitumia fedha za *CSR* kujenga nyumba za wafanyakazi na waka-*declare* fedha zile kwamba wametumia kwenye kujenga miradi ya maendeleo, lakini cha kushangaza nyumba zile walianza kuuziwa tena watumishi na zile fedha hatujui mpaka leo zimeenda wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mgodi huo wa Bulyankhulu umekuwa ukilalamikiwa kila kona na tukisema hapa tunaambiwa jambo moja tu, kwamba mkisema mwekezaji huyu mkubwa tutakuwa *blacklisted*. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tunasema wananchi wa Jimbo la Msalala hasa Bulyankhulu, hatuko tayari kupata manyanyaso haya yanayoendelea kwa hofu ya kwamba tutafungiwa.*(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Mbunge lakini nafikiri hoja yako imeeleweka na Mheshimiwa Waziri ni muhimu, nafahamu sheria inaweka mwongozo lakini ni muhimu ninyi kama Wizara kufuatilia hizi fedha zinazotolewa zinafanya kazi gani, kwa sababu bila kuwa mnafahamu zinafanya kazi gani ndiyo hivyo mtu anaamua kupeleka kule anakotaka yeye na siko kule wananchi wanakotaka fedha zipelekwe. *(Makofi)*

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira atafuatiwa na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba ajiandae.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo kwa mara zote amekuwa akiibeba agenda la *local content* na akiendelea kusisitiza umuhimu wa kuongeza na kuimarisha ushiriki wa Watanzania kwenye sekta hizi za uziduaji ikiwemo na sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu nitajielekeza kwenye ule mradi wa Kabanga *Nickel* uliopo Wilayani Ngara Mkoani Kagera, hapa napenda nitambue jitihada kubwa sana za Mhashamu Baba Askofu Niwemugizi pamoja na Mbunge wa Jimbo la Ngara Kaka yangu Mheshimiwa Ndaisaba wamejitahidi sana kulisemea suala hili kwamba kwenye mradi huu wa Kabanga *Nickel* yanachimbwa yale madini lakini yatasafirishwa na kufanyiwa uchenjuaji Kahama, jambo ambalo tukirudi kwenye misingi ya *local content* itafifisha namna ambavyo wananchi wa Ngara na Mkoa mzima wa Kagera kwa ujumla watakavyonufaika na mradi huu wa Kabanga *Nickel. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa lugha nyingine ni kwamba Mkoa wa Kagera na Wilaya ya Ngara yatabaki mashimo wakati fursa zote ambazo ndiyo nyingi za wananchi wa Ngara na wananchi wa Kagera kwa ujumla kuweza kushiriki zitahamishiwa Wilayani Kahama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo ningependa kupata maelezo ya kina kutoka kwa Serikali kwanini wameamua kwenda kinyume na ambavyo inatakiwa kwamba katika mnyororo wa mradi, mnyororo mzima wa mradi unatakiwa ufanyike katika eneo la mradi. Kwanini katika mradi huu wa Kabanga *Nickel* Serikali imeamua kuchimba Wilayani Ngara ambako mradi ndiyo upo na

madini ndiko yalipo lakini kuwekeza *refinery* Wilaya ya Kahama Mkoa wa Shinyanga.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hilo litafifisha ushiriki wa wananchi wa Ngara, litafifisha ushiriki wa wananchi wa Kagera, litafifisha fursa za wanawake, vijana na jamii nzima ya Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili wote tunafahamu kwamba kuna kitu kinachoitwa *service levy* asilimia 0.3, hii *service levy* itakuwa inakwenda Kahama, sasa Je, Ngara watanufaika vipi na hii asilimia 0.3 ya *service levy*. Kwa hiyo, naomba nipate maelezo ya kuridhisha kutoka kwa Serikali kwanza kwanini wameamua kutowezeka *refinery* ifanyike pale pale Ngara. Pili, tutakapokuwa tunabeba haya madini na kuyasafirisha mpaka Kahama ni hasara gani ambayo itatokea katika uharibufu wa barabara zetu. Tatu, wananchi wa Ngara watanufaika vipi kutoka kwenye ile similia 0.3 ya *service levy* ambayo sasa italipwa Kahama.

Mheshimiwa Spika, labda Serikali ije na mpango madhubuti wa kuhakikisha kwamba Wilaya ya Ngara itapata asilimia fulani kutoka kwenye ile asilimia 0.3 ya *service levy. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo mimi nisiporidhika na majibu ya Serikali nitashika Shilingi ya mshahara wa Waziri. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Constantine John Kanyasu atafuatiwa na Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, Mheshimiwa Jumanne Kishimba ajiandae.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ninaomba pia kutumia nafasi hii kusema ninaunga mkono hoja, lakini kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake wote kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya.

Mheshimiwa Spika, mimi labda nianze kusema tunafanya vizuri sana na *CSR* kwetu hasa Jimbo langu la Geita Mjini, lakini pia tunafanya vizuri sana na *local content* kwa hiyo ni vizuri kule ambako bado wanapata shida wakaja kujifunza namna ambavyo tunafanya na hasa kwenye *local content* namna ambavyo wakulima wameshirikishwa katika maeneo mbalimbali ya Saraguro na Mgusu kwenye kushiriki kuhudumia mgodi, Mheshimiwa Waziri nakupongeza sana kwenye eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Mheshimiwa Waziri ulifanya ziara Geita na kwenye ziara hiyo tulikuwa na Kaimu Mkuu wa Mkoa, ulipokea malalamiko mbalimbali kutoka kwa wananchi wa Geita na Mheshimiwa Waziri naomba *ni-quote* sehemu ya hotuba ya Ndugu Paul Young alipokuwa kwenye *World of Engineers* huko Australia alisema ''*Mining sustainably within a community should provide relief from poverty, hunger and safety hood for local communities, this is not considered to be charity, it is about being a part of a community good health and educational aspiration''* na akamalizia kusema ''*however extraction of metals and mining of industrial minerals must be done sustainably, this means giving consideration to people, the environment and the economy, human aspect including heath, social and cultural element''*.

Mheshimiwa Spika, ipo shida nimelazimika *ku-quote* haya maneno ili Mheshimiwa Waziri aweze kunielewa. Ilikuja ziara ya Mawaziri wanane Geita, wananchi wakazungumzia mgogoro wa miaka 20 karibu na tatu kwa wananchi ambao wanaishi kwenye vigingi na mipasuko, Mheshimiwa Rais wa sasa akiwa Makamu wa Rais alishatoa maelekezo suala hili lishughulikiwe, Mheshimiwa Rais Hayati Magufuli alitoa maelekezo, Mawaziri wote tangu Profesa Muhongo na Mawaziri wengine na Mheshimiwa Biteko alitoa maelekezo ishughulikiwe.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa mitaa karibu saba wanaishi kwenye mgogoro wa mgodi wa vigingi kwa miaka 23 na matokeo yake wananchi hawa wanaishi kwa umaskini

mkubwa kwa sababu Serikali imeshindwa kufanya maamuzi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mitaa ninayozungumzia haina barabara, haina maji, haina shule, haina zahanati hawaruhusiwi kupima viwanja kwa sababu tu eneo wanaloishi ni ndani ya leseni ya mgodi. Maelekezo yametolewa na Serikali, Kamati imetoa maelekezo kwamba hawa wananchi wapimiwe mgodi unakataa. Vimefanyika vikao vya kila namna imeshindikana.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema jambo moja hapa, Mheshimiwa Waziri alizungumza na wafanyakazi wa *GGM* akasifia Serikali kwamba sasa 95 *percent* ya watumishi wa *GGM* wa menejimenti, niseme wameondoa 95 *percent* ni Watanzania, lakini wafanyakazi walimwambia kuwepo kwa sehemu kubwa ya waswahili kwenye menejimenti kumeongoza matatizo makubwa na urasimu kuliko ilivyokuwa Wazungu. Tatizo hili linakuja kwa sababu Waswahili hawafanyi maamuzi ya kum-*favor* mtanzania hata kama anaona sheria inaruhusu. Nazungumza hivi kwa sababu malalamiko ya watumishi wa *GGM* ni makubwa mno na uonevu ni mkubwa kuliko ilivyokuwa zamani wakati Wazungu ni wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa wananchi wanayo haki ya maeneo yao, lakini wamekataa wanasema sisi hatufanyi. Tumeshughulika na jambo hili kila mkutano, kila hotuba halifanyiwi maamuzi, namwomba Mheshimiwa Waziri...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Muda wake umeshaisha anamalizia sekunde thelathini.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Namwomba Mheshimiwa Waziri wapo watumishi pale wa mahusiano ambao wanazuia maelekezo ya Serikali achukue hatua, bila kuchukua hatua hatutafikia

suluhu ya wananchi hawa ambao wanailamu Serikali bila sababu ya msingi na sheria zipo wazi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba atafuatiwa na Mheshimiwa Jumanne Kishimba na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini ajiandae.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie katika Bajeti ya Wizara ya Madini. Kabla sijaanza mchango wangu nataka nimsaidie tu kaka yangu Iddi, Mbunge wa Msalala kwamba kifungu cha 105 cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2019 kinaelekeza *CSR* utekelezaji wake ni lazima mipango yote ipangwe na halmashauri ikishirikiana na mgodi na halmashauri ni lazima itengeneze *guideline* ya namna ya kutekeleza *CSR* na imeweka haki zote za Baraza la Madiwani na Halmashauri kutekeleza. Kwa hiyo kama hawafanyi hivyo ina maana wametoa hisani kama watu wengine na hisani hiyo ni lazima itozwe kodi kwa sababu hawajafuata utaratibu wa kisheria.

Mheshimiwa Spika, tarehe 22/04/2020 nilisimama ndani ya Bunge hili Tukufu, pamoja na kashikashi zote nilisimama kwa ajili ya kuwatetea wachimbaji wadogo wadogo ambao wakiwa wanachimba sehemu kubwa ya mapato yao ilikuwa inachukuliwa na mtu anayeitwa mwenye shamba na fedha nyingine anachukua mtu ambaye anaitwa msimamizi. Leo kwa kweli kwa mara kwanza niseme tu nimpongeze Mheshimiwa Waziri alisilikiza kilio change, ametekeleza na sasa hivi kwa mara ya kwanza mchimbaji mdogo anapochimba na kupata dhahabu asilimia 70 ya mapato inakuwa ya kwake, huyo anayeitwa mwenye shamba anapata asilimia 15 na huyo anayeitwa msimamizi anapata asilimia 15. Mimi najivunia kwa sababu hoja niliyoisimamia imetekelezwa kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuchukua maombi yangu ambayo niliyasema ndani ya Bunge hili mimi nina

mambo mawili ambayo nataka nimwombe Mheshimiwa Waziri ayasimamie. La kwanza, inaonekana kwamba asilimia kubwa ya watu ambao wana leseni za uchimbaji hawachimbi, wamezikalia leseni hizo. Hayo siyo maneno yangu, ripoti ya *CAG* inasema asilimia 58.3 ya watu wenye leseni za uchimbaji hawafanyi shughuli za uchimbaji, yaani ni leseni mfu.

Mheshimiwa Spika, vile vile ripoti hiyo inasema katika hiyo asilimia chache ambayo ya watu wanaochimba, asilimia 97 zaidi ya robotatu ya watu wanaochimba ni wachimbaji wadogo wadogo. Mheshimiwa Waziri naomba awanyang'anye leseni watu ambao wamezikalia leseni hizo na maeneo ya uchimbaji, hawafanyi shughuli za uchimbaji, badala yake wanawanyima fursa wachimbaji wadogo ambao wapo tayari kufanya shughuli za uchimbaji na wanajikuta wachimbaji wale wanachimba kwenye maeneo ambayo hayana *potential* ya kupata mali. Hilo moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu la pili kwa Wizara hii; *TRA* wanakwenda kwenye masoko ambayo wachimbaji hawa wanakwenda kuuza dhahabu, masoko ambayo yameanzishwa hivi karibuni. Wakifika pale wanamkuta mchimbaji anauza dhahabu yake, tuseme milioni 200 au milioni 300, Waheshimiwa msishangae milioni 200 au 300 kwa mchimbaji ni hela ndogo sana akiipata. Anakwenda mtu wa *TRA* pale anamtoza ushuru kwa ile milioni 300 pato ghafi ambalo mchimbaji yule amelipata bila kujali kwamba kuna gharama za uchimbaji, bila kujali mtu yule amepata hasara kiasi gani, bila kujali kwamba mtu yule amewekeza kiasi gani? Sasa hawa wachimbaji wadogo mtu anaweza akachimba hata miaka 10 hajakutana na mali, anazika mtaji ardhini zaidi ya mamilioni ya fedha. Anapopata bahati anakwenda kuuza dhahabu yake anategemea angalau aweze, kuna watu wapo kwenye machimbo kule wana miaka zaidi ya 10 hawajawahi kuonana na familia zao.

Mheshimiwa Spika, naomba nimwombe Mheshimiwa Waziri akae pamoja na watu wa madini, wasitafute *cheap*

*income,* hawa watu wana *struggle* kwenye machimbo na wenyewe waende kule wanakochimba wale watu. Wizara pia iliahidi kuwawezesha wachimbaji wadogo wadogo, nafahamu kwamba hii ni *private sector,* kuwapa mitaji mmoja mmoja ni vigumu, lakini ng'ombe anayekupa maziwa lazima umlishe, wenyewe wanakiri kwamba sekta ya madini ndiyo sekta inayolipa kuliko sekta nyingine yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Sekunde thelathini.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa faini aliyoitoza *NEMC* na Mheshimiwa Waziri kwenye Bonde la Mto Tigiti. Wametoza faini ya bilioni moja inaonekana ni kubwa, lakini kiuhalisia madhara makubwa yaliyopatikana kwa watu wale bado wanahitaji kulipwa fidia. Hatukubaliani kanda ya ziwa ndiyo inayoongoza... *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Jumanne Kishimba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, rafiki yangu daktari, ingawaje sasa hivi haonekani toka amepata uwaziri. Nawapongeza sana pamoja na wafanyakazi wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, dhahabu ni kama ilivyo *petrol* na *diesel,* sisi kwa sasa hivi tunavyo-*treat* dhahabu tunai-*treat* kama bidhaa ya viwandani. Utajiri wa Waarabu ni pale mafuta yanapopanda, anayenufaika ni nchi ile kwenye ile *difference* ya kile kilichopanda. Bei ya dhahabu kabla vita ya Ukraine haijaanza ilikuwa *ounce* moja dola 1,800, lakini

siku bomu limedondoka moja bei iliruka mpaka 2100, ongezeko la dola 300 ambayo sawasawa na dola 10 kwa gramu.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu hapa ambayo najaribu kuijenga, je, hiki kilichoongezeka ni mali ya nani? Kwa sababu yule mwenye mgodi alikuwa anachimba na anapata faida na hiki kilichopanda hakikupanda kwa gharama ya uzalishaji, kilipanda kwa hofu iliyoingia duniani. Kwa wenzetu fedha hizo ni mali ya Serikali asilimia 100. Nasema hivyo kwa sababu mwenye mgodi hawezi kulalamika kwa sababu yeye gharama ya dhahabu haitokani na bei unayouza, inatokana na wewe unavyoendelea. Kwa hiyo bomu lilipodondoka bei ya dhahabu ilipanda muda uleule na tofauti iliyopo hapo kwa uzalishaji wa dhahabu kwa Tanzania ambao ni karibu tani 45 kwa mwaka, ni sawasawa na dola milioni 40 kwa mwezi. Pesa hizo kwa *rate* ya leo ni sawasawa na bilioni 200 kwa mwezi. Ni tofauti ya bei iliyotokea baada ya bomu kudondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzetu Waarabu ndicho kinachowapa utajiri, hatajiriki *BP,* anatajirika yeye mwenye mali. Ni hesabu rahisi haiitaji elimu kubwa sana; ukiweka mpunga kwenye mashine ya mtu au ukaweka alizeti ukasuburi kuja kukamua, inapopanda bei ya alizeti anayenufaika au mpunga anayenufaika ni yule mwenye mpunga si mwenye mashine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuwaombe wenzetu wa wizarani kwasababu elimu hii ya madini najua wakati mwingine tukiongea elimu kuna kuwa na mvutano. Elimu hii ya madini ni mpya kwenye Idara zetu na kwenye shule zetu, kwa hiyo tuwaombe watalaam kama wanaweza kushauriana na hao wenye mgodi na hawawezi kukataa na hata tukiziacha hizi pesa, si kwamba mwenye mgodi atanufaika zitatengenezewa matumizi mengine ambayo yatazamia humo ndani. Kwa kawaida hizi pesa ni mali ya Serikali, zinaweza zikatusaidia mno. Zinatosha kabisa kutibu watu wetu bure kwa mwaka na kuwapa chakula cha mchana hata watoto wetu wa shule. Tuwaombe sana

wenzetu wa madini wafikirie sana suala hilo kama wanaweza kulipeleka linaweza likatusaidia hasa sisi tunaotoka maeneo ya madini.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kuchangia hayo tu. Baada ya mchango huo, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Phillip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa Wizara ya Madini, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza Mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Madini, kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Taifa letu katika kuboresha maisha ya wananchi na pia utayari wetu wa ushindani wa Kimataifa *(National Competitiveness).* Bajeti hii inaenda sambamba na dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio ya sekta ya madini, Serikali inashauriwa kuchukua hatua za kuimarisha zaidi sekta hii muhimu ili kukabiliana na athari za kiuchumi kutokana *Covid-19* na sasa vita vya Urusi na Ukraine. Kutokana na athari ya kiuchumi uliokumba dunia nzima, hii

inaweza kuwa fursa kwa Serikali kuvutia uwekezaji zaidi kwenye madini hasa dhahabu, madini ya chuma na madini ya *calcium carbonate, limestone* na *phosphate.* Dhahabu ina historia ya bei kutoyumba kwenye soko la dunia kwa vile mabenki yanatumia dhahabu kwenye kuwekeza na kutokana pia na kuyumba kwa thamani ya shilingi na hata dola ya Marekani, Serikali inaweza kutumia dhahabu kama mbadala wa kuwekeza amana zake.

Mheshimiwa Spika, vita vya Urusi na Ukraine vimesabisha upungufu mkubwa wa uzalishaji wa mbolea na hii ni fursa kwa Serikali kuwekeza kwenye viwanda vya mbolea kwa kutumia malighafi zinazopatikana hapa nchini kama vile *phosphates, calcium carbonate, limestone* na *natural gas.* Katika kipindi cha mtikisiko wa uchumi, bei ya madini ya chuma na hata makaa ya mawe haiyumbi na Serikali inaweza kupata mapato mengi katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali kuchukua hatua za makusudi na kuharakisha uwekezaji kwenye mradi wa chuma *(Liganga Iron Ore)* ikiwa ni pamoja na makaa ya mawe *(the Mchuchuma coal mining and power projects).* Mradi wa Liganga na Mchuchuma ulitarajia uwekezaji wa dola za Kimarekani bilioni tatu na kuzalisha ajira zaidi ya 30,000 na hii inaweza kuwa fursa nzuri katika hiki kipindi cha balaa la athari za *Covid-19* na vita vya Urusi na Ukraine.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mradi wa Liganga na Mchuchuma, napendekeza Serikali kuchukua hatua kuharakisha uwekezaji kwenye mradi wa madini ya *NIOBIUM* ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Kiwanda cha *Ferroniobium (FeNb)* ambacho kitakuwa cha kwanza Afrika na cha nne duniani. Kutokana na mahitaji makubwa ya ujenzi wa reli, madaraja na reli ya *SGR,* kuna mahitaji makubwa ya vifaa vya chuma ambavyo ni imara, lakini vyepesi na vyenye ubora wa Kimataifa. Kwa kutumia sheria zetu za uwekezaji, Serikali itumie fursa za kipindi hiki ili kuvutia wawekezaji kwenye madini ya viwandani ili yaongezwe thamani hapa kwetu na pia kuvutia malighafi ya madini toka nchi zingine ili yachakatwe hapa kwetu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imebahatika kuwepo kwa madini ya *NIOBIUM* ambayo inapatikana milima ya *Pandahill* Wilaya ya Mbeya na mahitaji ya *Ferroniobium (FeNb end product)* ni makubwa duniani na hapa kwetu pia.

Mheshimiwa Spika, Serikali inahitaji kujiwekekea mikakati ya haraka *(quick wins)* ili kuhakikisha inakabiliana na athari za kiuchumi kutokana *Covid-19* na sasa vita vya Urusi na Ukraine. Kwa kutumia rasilimali zetu za madini, Serikali inaweza kutengeneza fursa nyingi na kupitia Mradi wa *Niobium* na Kiwanda cha *Ferroniobium*, ajira 2,000 zitakazozalishwa wakati wa ujenzi na pia kutakuwepo ajira za kudumu zaidi ya 600 na *indirect jobs 7,000.* Mradi utazalisha mapato kila mwaka shilingi bilioni 500 *(US$ 220 million)* ambapo mapato kwa Serikali kila mwaka shilingi bilioni 50 *(US$ 22 million)* na uhai wa mgodi ni zaidi ya miaka 30. Hiki kitakuwa kiwanda cha kisasa cha kwanza Afrika *(Modern Manufacturing Plant and Smelter).* Pamoja na kuingiza teknolojia hii adimu na ujuzi *(skills transfer)* pia itachangia huduma za kijamii *(corporate social investment in community)* na chanzo cha fedha ya kigeni. Naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Madini Dkt. Doto Biteko na Naibu wake Dkt. Stephen Kiruswa na watendaji wote wa Serikali kwa kazi nzuri wanazofanya kwenye sekta ya madini na mimi nitachangia kwenye changamoto za wachimbaji wadogo wadogo wa madini ya *Tanzanite* nchini.

Mheshimiwa Spika, sekta ya madini ni moja ya sekta kubwa nchini inayoinua uchumi wa nchi. *Tanzanite* ni kati ya madini yanayolipatia Taifa pesa za kigeni na kuliingizia Taifa kipato. Madini ya *Tanzanite* hupatikana nchini Tanzania tu.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wa kigeni wamefanikiwa sana kunufaika na rasilimali hii ya Taifa letu. Kampuni ya nje ya *Tanzanite One* ni moja ya kampuni iliyofanikiwa kwa kuwa na vifaa vyenye ubora kwa wachimbaji wake.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wadogo wa *Tanzanite* wanakabiliwa na changamoto mbalimbali kubwa ambazo Serikali inapaswa kuzitatua ili kuwanufaisha na rasilimali hii ya Taifa lao.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa inayowasumbua wachimbaji wadogo wadogo wa madini ya *Tanzanite* ni matumizi ya teknolojia za kizamani, upatikanaji wa zana za kisasa za uchimbaji na mitaji midogo kwa kundi hili.

Mheshimiwa Spika, bei ya zana za uchimbani ni kubwa na vilevile hutozwa kodi kubwa. Hapa nchini Tanzania ni wafanyabiashara wachache wanajihusisha na biashara ya zana za uchimbaji kama vile vifaa vya kuchoronga miamba, vilipuzi miamba na kadhalika kutokana na kodi nyingi kwenye bidhaa hizi. Kwa hali ilivyo sasa hivi, vifaa hivi vikiingizwa nchini wachimbaji wadogo hushindwa kumudu gharama.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto nilizotaja hapo juu, naishauri Serikali yafuatayo; kwanza Wizara ya Madini kwa kushirikiana na Waziri wa Fedha washauriane na kuondoa kodi kwa wazawa wanaoagiza na kufanya biashara ya vifaa ili viingie kwa wingi, madini yachimbwe na wengi na kodi iongezeke kutoka kwenye mauzo ya *Tanzanite* badala ya ile ya kwenye vifaa.

Pili, Wizara ijadiliane na benki za biashara nchini ili zitoe mikopo ya mitaji na ya kununulia vifaa vya kuchimba *Tanzanite* kwa wachimbaji wadogo wadogo.

Tatu, Serikali kupitia taasisi zake iwasaidie wachimbaji wadogo wadogo wa *Tanzanite* kupata wataalamu na teknolojia za kisasa za kuchimba madini.

Mheshimiwa Spika, nne, Serikali ifanye tafiti za kina katika maeneo ya Mererani ili kujua maeneo yenye madini na kujua yapo umbali gani ili kurahisisha uchimbaji kwa

wachimbaji wadogo wadogo. Kwa kufanya hivi, itarahisisha uwekezaji na uchimbani na kuipatia Serikali kipato cha uhakika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA**: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa fursa hii ya kutoa mchango wangu katika hotuba ya makadirio na mapato ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2022/ 2023.

Pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kutayarisha na hatimaye kuiwasilisha hotuba hii katika Bunge lako tukufu kwa ufasaha na umakini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo nikianza na suala la wachimbaji wadogo; napenda kuipongeza Wizara kwa juhudi zake inayozichukua katika kuwaenzi wachimbaji wadogo. Hili ni kundi kubwa na ni muhimu katika nchi yetu. Kundi hili kwa muda mfupi limeonesha maendeleo katika kuchangiya pato la Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda kushauri Serikali mambo mawikli katika kundi hili; kwanza Serikali ioengeze jitihada ya kuwapatia mafunzo zaidi wchimbaji hawa ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Pili, nashauri Serikali iwapate bima za afya wachimbaji hawa ukizingatia kuwa kazi hii ni miongoni mwa kazi ngumu na za hatari. Naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kiruswa na mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI MADINI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kutumia dakika zangu tano

kuchangia kwa kifupi kuhusu hoja yetu ambayo imepokelewa na kujadiliwa na Bunge lako Tukufu.

Mhehimiwa Spika, kabla sijasema mambo mawili, matatu kwa hizi dakika tano, niruhusu kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kunipa nafasi hii ya kuwa Naibu Waziri wa Madini. Leo ni mara yangu ya kwanza kusimama kuchangia kwenye hoja ya bajeti yetu kwa mwaka huu 2022/ 2023 na nikiwa chini ya Waziri wangu mahiri Dkt. Biteko, niseme tu kwamba kazi tuliyopewa na Mama Samia tunaisimamia usiku na mchana kwa uadilifu mkubwa na kwa umahiri mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikushukuru pia wewe Mheshimiwa Spika pamoja na Naibu wako kwa ushirikiano mnaotupa na niwapongeze kwa sababu na ninyi mmeingia kwenye nafasi hizi hivi karibuni, lakini mnavyotuongoza tutafika salama. Mungu azidi kuwaongoza katika kutuendesha katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo yaliyosemwa katika mjadala wa bajeti yetu ni mambo ya msingi ambayo kwanza Kamati yetu ya Nishati na Madini imeyafunika kwa asilimia kubwa kupitia kwenye taarifa yake na nipende tu kusema kwamba haya yote yaliyosemwa na Kamati na sisi tumekuwa na desturi ya kusikiliza ushauri wao na kufanyia kazi kila aina ya ushauri na mwongozo wanaotupatia kwa kuchambua kila hoja na kuifanyia kazi. Haya yote tumeyapokea na kwa kumsaidia waziri tunakwenda kuyafanyia kazi na baadhi ya mambo yameshaanza kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni ya Waheshimiwa Wabunge katika maeneo mbalimbali ya ushauri waliotupa pia tumeyapokea na kuna eneo moja mahsusi ambalo nilipenda kuligusia zaidi nimwachie Waziri wangu atahitimisha yale mengine, ni eneo la wachimbaji wadogo. Ni kweli wachimbaji wadogo ndiyo kundi kubwa ambalo likiwezeshwa watakwenda kuinyanyua sekta ya madini ili iweze kuleta tija zaidi ya hapa tulipokwishafikia.

Mheshimiwa Spika, katika kutambua hilo sisi tumechukua juhudi za ziada kama Wizara na tutaendelea kuzifanyia kazi ya kuhakikisha kwamba tunaziwezesha hizi taasisi zetu zilizo chini ya Wizara hasa *GST* na *STAMICO* kwa kuwapa vifaa na kuendelea kuwaongezea rasilimaliwatu ili wafanye utafiti wa kina katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu yanapopatikana madini. Katika kufanya hivyo wataweza kubainisha maeneo mahususi yanayofaa kupewa wachimbaji wadogo, kwa sababu moja ya malalamiko ambayo yanajitokeza hapa ni kwamba mitaji inapotea wanawekeza katika maeneo ambayo ni ya kubahatisha.

Mheshimiwa Spika, sisi katika kutambua hilo *STAMICO* sasa hivi wao wameagiza mitambo mipya ambayo inakwenda kusaidia kwa bei punguzo, kuwasaidia wachimbaji wadogo kubaini madini yanayopatikana katika maeneo ambao wanapendelea kuchimba kwa aina ya madini ili waweze pia kupata dhamana katika mabenki yetu ambapo tumeshapata benki zaidi ya nne ambazo zimekubali kutoa mikopo ama ya fedha ama ya vifaa kwa wachimbaji wadogo; mabenki hayo ni *NBC*, *KBC* na *CRDB.* Hawa wote wameshasaini maridhiano na Wizara kupitia taasisi ya *STAMICO* kwamba wako tayari kutoa mikopo. Wachimbaji wadogo wanapoungana na kuunda vikundi vya uchimbaji wao wako tayari wakizingatia vigezo vya kuhakikishiwa na kudhaminiwa na Wizara kwamba wanayo maeneo yenye mashapu ya dhahabu au maeneo yenye madini ya vito, wapo tayari kuwakopesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya wachangiaji wanasema kwamba masharti ni magumu. Masharti siyo magumu ni suala tu la kufuata utaratibu, ni suala la tukufuata vigezo vya kawaida kabisa ambayo wakivifuata kimoja baada ya kingine na sisi tukiwa tumewapa taarifa za viashiria vya uwepo wa madini katika eneo husika watakwenda kupata hiyo mikopo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu naona muda ni mfupi sana nimalizie pia kwa hili suala *Local Content* na *CSR.*

Miongozo ya Wizara imewekwa bayana inadhihirisha kabisa kila mwekezaji anatakiwa aje na mpango wake wa *CSR* aje na mpango wake wa *Local Content* kwamba katika aina ya uchimbaji wanaofanya vifaa gani vinapatikana nchini na ataweka katika orodha ya *database* ambayo inaandaliwa na Wizara ataweka yaani ata- *float* yale mahitaji yote ambayo yeye anahitaji katika uchimbaji wake na watu wa ndani ndiyo wanaopewa kipaumbele na wale wengine yale yasiyopatikana nchini ndiyo yanayokwenda kuagizwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, *CSR* ni mwongozo ambao namshukuru Mheshimiwa Salome amelitolea ufafanuzi mzuri, ndivyo ilivyo, ni wao wenyewe ndiyo wanapambana kule katika halmashauri zao kwa sababu hawazingatii...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa mchango wako.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa kabla sijamwita mtoa hoja kanuni ya 34(2) naongeza nusu saa, Mheshimiwa Waziri wa Madini Mheshimiwa Dkt. Dotto Biteko, mtoa hoja, uje uhitimishe hoja yako.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii kuhitimisha hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini Mwaka wa Fedha 2022/2023. Wizara imepokea michango mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge ambayo wameitoa kwa kusema, pia tumepata ushauri na maoni ya mapendekezo kutoka kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati ya Madini ambayo kwa kweli ni muhimu sana kwetu.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla ushauri na maoni yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni ya msingi sana. Huo ni ushahidi mwingine kuwa Bunge lako ni Bunge ambalo kwa kweli linasimamia maslahi mapana ya wananchi wetu wa Tanzania. Ukiwasikiliza kwa kiwango kikubwa yale wanayoyazungumza ni yale ambayo ama yanaathiri uchimbaji ama biashara yenyewe ya madini na hivyo kufanya sekta hii isikue. Kwa hiyo, tumeyachukua kwa uzito mkubwa na sisi kama Wizara tutaenda kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba tu nifafanue kwa kifupi hoja mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezielezea. Nieleze kwamba Wizara ya Madini kwa vyovyote vile ili uweze kufanya maendeleo kwenye sekta na kuifanya sekta ikue haiwezi kuwa na *monopoly* ya mawazo au ya fikra, ni lazima ichukue mawazo ya Waheshimiwa Wabunge, mawazo ya wadau wengine waliomo kwenye sekta na kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mmeona hapa hoja zinazozungumzwa kwa kweli ni zile ambazo zinatufundisha au zinatuelekeza kwenye kuboresha zaidi, zinaweza kuzungumzwa kwa *tone* tofautitofauti lakini *bottom line* ya kila hoja iliyosemwa ni kuhakikisha kwamba manufaa ya madini haya yanakuwa kwa Watanzania na kwa nchi yetu na kwakweli ndiyo kiu yetu sisi Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, sasa limezungumzwa eneo la wachimbaji wadogo, nataka nilielezee hilo kwa kifupi tu. Ni kweli kwamba yapo maeneo watu wamepewa leseni na toka wamepewa leseni inawezekana hawafanyi chochote kwa namna ya kuonekana kwa macho, lakini uchimbaji wa madini wenyewe ulivyo si kila atakayepewa leseni leo leo ataanza kuchimba, mwingine ataanza kufanya utafiti, mwingine ataanza kutafuta hizo *data* na baadaye aanze kuchimba.

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie kwamba Wizara ya Madini toka tumeanza kuwapa nguvu wachimbaji wadogo hizo ndizo hatua tunazochukua. Tunapata lawama

hapa na pale kwamba tunafuta leseni, ni kwa sababu tunatekeleza maelekezo ya Bunge, lakini tunatekeleza maelekezo ya viongozi wetu kwamba ni lazima wachimbaji wadogo wapewe kipaumbele. Hivi nilivyosimama hapa tumeshafuta zaidi ya leseni mia mbili ambazo ni *dormant* na zipo nyingine nyingi zaidi ya 400 ambazo zina-*default notice, process* ya kufuta inaendelea.

Mheshimiwa Spika, *process* ya kufuta leseni ina lawama nyingi, sisi Wizara ya Madini tumekubali kubeba lawama hiyo kwa niaba ya wachimbaji wadogo, kwa sababu wapo watu wengine ambao ni kweli watashika yale maeneo kufanya udalali, nitakaa na leseni kutegeshea kuona ni nani anakuja. Wengine wanasubiri wachimbaji wadogo waende kwenye hile leseni wachimbe, halafu aseme hapa ni kwangu awaondoe wale wachimbaji wadogo. Nataka niwahakikishie wale wenye leseni kwamba wale ambao wanatekeleza matakwa ya sheria, Wizara tutawalinda lakini wale ambao hawatekelezi matakwa ya kisheria, maeneo hayo tutayachukua tuwapatie wale ambao wanahitaji kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo limeelezwa hapa kwa uchungu mkubwa ni jambo la *CSR*. Inawezekana kuna migodi mingine haifanyi vizuri. Nieleze kwa ujumla kwamba migodi mikubwa hii inatekeleza kwa kiwango kikubwa matakwa ya sheria ya kutenga fedha kwa ajili ya *CSR*. Sasa tunachogombea hapa siyo uwepo wa fedha, tunagombea matumizi ya fedha na nadhani hili ni jambo zuri. Tulikotoka tulikuwa tunagombea uwepo wa fedha zenyewe, sasa hivi hiyo siyo *story* tena, *story* ni namna gani hizo fedha zinavyotumika.

Mheshimiwa Spika, Sheria yetu ya Madini, *section* ya 105 imetoa utaratibu mzuri sana kama ambavyo Mheshimiwa Makamba ameeleza kwamba ni lazima mipango ile ya *CSR* ipelekwe kwenye Halmashauri. Kazi ya Halmashauri kubwa ya kwanza ni kuthibitisha au ku-*approve* hiyo mipango. Una-*approve* kwa kuangalia *value for money.* Kuna wakati fulani miradi mingine ilikuwa inatekelezwa; mfuko mmoja wa

*cement* unatekelezwa kwa *CSR* lakini mfuko wa *cement* unauzwa shilingi 80,000/=. Sasa kama hali ndiyo hiyo, kazi ya Halmashauri ni kuhakikisha kwamba mfuko wa bei ya soko ni huu au bidhaa inayotakiwa kununuliwa kwa ajili ya kutekeleza bei ni hii.

Mheshimiwa Spika, mgodi tuliokuwanao kwenye *framework*, mgodi ambao *CSR* yake unaweza kuiona kuanzia *day one,* ni migodi inayosimamiwa na Twiga, ukiwemo Mgodi wa Bulyanhulu pamoja na Mgodi wa *North Mara*. Hii *CSR* yake iko *packed* kwenye uzalishaji wa dhahabu. Kila wakia moja ya dhahabu unachukua dola sita unaziweka pembeni kwa ajili ya *CSR*.

Mheshimiwa Spika, hata *North Mara,* tunavyozumza, fedha zipo Shilingi bilioni 5,600 hazijafanyiwa kazi. Kuna Shilingi bilioni moja nyingine ya mwaka 2021 ipo haijafanyiwa kazi. Kinachotokea ni kwamba kuna matatizo ya usimamizi wa fedha za *CSR*. Kwa hiyo, kuna wakati mwingine tunafanya *auditing,* tunachukua muda mrefu na *auditing* hizo wanaoumia siyo sisi, ni wananchi, lakini kuja kumlaumu mgodi kama mtu ambaye hajatoa hizo fedha, na penyewe kwa kweli tuwatendee haki kidogo. fedha hizi wao wamezitoa na tayari ziko kwenye utaratibu wa kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, hata kule Bulyanhulu, tunazungumza kujenga barabara; ni kweli, mgodi umeshatenga Dola za Kimarekani milioni 40; na barabara ambayo tunabishana, tujenge kutokea Mwanza kuja Kakola au kutokea Kakola kwenda Kahama, hilo ndiyo bado tunabishana. Ila kazi ya mgodi, tayari hela zake ameshatenga, anasubiri uamuzi wetu wenyewe.

Nawaomba wale wote tuliopewa wajibu wa kusimamia mambo haya, tufanye haya mambo kwa haraka ili huduma zipatikane kwa wananchi ili imani ya wananchi kwamba sekta hii inawasaidia kwenye maisha yao iweze kupatikana.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nami nisingependa kuchukua muda mrefu, ni jambo lililozungumzwa kuhusiana na Merelani. Nimesikia *concern* ya Waheshimiwa Wabunge, lakini lazima tukubali, maeneo mengi yanayochimbwa madini, watu wamebadilisha maisha yao. Ukienda Mahenge, kabla hatujapasimamia vizuri na leo hali yake ni tofauti; ukienda Geita hali ni tofauti, ukienda Kahama hali ni tofauti, lakini bila kuficha Mererani hali yake ni tofauti sana.

Mheshimiwa Spika, hali ya Mererani ni mahali pa ukiwa. Watu wana hali ngumu, lakini watu wanapishana na magari, wanakuja Mererani, wanaondoka. Ndiyo Serikali ikaja na utaratibu kwamba tuongeze manufaa kwa kujenga soko Mererani. Nafurahi kwamba fedha zilizotengwa kwa ajili ya kujenga lile soko ni Shilingi bilioni tano na bilioni moja imeshatolewa kwa ajili ya kujenga lile soko.

Mheshimiwa Spika, yako matatizo tutakutana nayo kwenye kutekeleza, ni kwamba ni kweli pengine biashara itashuka, kutakuwa na *turbulence* ya hapa na pale, isituvunje moyo. Kazi yetu kama Serikali, yale yote aliyosema hata Mheshimiwa Gambo na Wabunge wengine wa Manyara, tutayaangalia yote kwa ujumla wake, tuje na utaratibu mzuri zaidi ambao utafanya sekta hii iweze kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie la mwisho kabisa kwamba, katika uchimbaji madini wanawake wamechangamkia fursa sana. Naomba nichukue nafasi hii niwapongeze sana wanawake wa Tanzania na ndiyo wamekuwa walipa kodi wakubwa sana.

Mheshimiwa Spika, Wizara tumeona hiyo ni fursa ya kuwatumia wanawake kwenye sekta ya madini. Tunataka tuwahamishe wanawake kwenye utoaji wa huduma kwenye midogo waende kwenye utendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi hii hatuwezi kuifanya wenyewe, tunahitaji Waheshimiwa Wabunge na wenyewe watusaidie. Kwa msingi huo, Wizara tumekaa, na tumeona kwamba tunahitaji tupate ma-*champion*

Wabunge wanawake watakaotusaidia kuhamasisha wanawake wengine kushiriki kwenye uchumi wa madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo tunaomba Waheshimiwa Wabunge wafuatao watukubalie, watusaidie kwenye jambo hili; Mheshimiwa Munde Tambwe, Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Janejelly Ntate James na Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga. Hawa wawe mabalozi wa wachimbaji madini wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. Naomba Bunge likubali kutupitishia makadirio ya fedha tulizoomba ili tukafanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsanteni sana. Tunaendelea na utaratibu wetu. Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 100 – Wizara ya Madini**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*......................Sh. 4,871,049,367

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki kina mshahara wa Waziri na kuna Mbunge anataka ufafanuzi, Mheshimiwa Nusrat Hanje.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kama nisiporidhika na majibu, nitashika mshahara wa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *GST* ndiyo *encyclopedia* ya madini kwenye Taifa letu, lakini kitengo hiki cha *GST* kinashughulika na kukusanya, kutunza, kuchakata na kusambaza taarifa, takwimu na *report* za madini kwa watu ambao wako kwenye sekta ya madini na Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa kuna ongezeko la makusanyo katika upande wa *GST* kwa asilimia 125 kutoka Shilingi milioni 889 mpaka Shilingi bilioni mbili. Hii inaonekana ni kwa sababu ya kuboreshwa kwa utoaji huduma katika upande wa *GST,* lakini ni kwa sababu walinunua vitendea kazi vipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu huu, *GST* kwenye Kitengo cha TEHAMA kuna pesa ndogo mno imewekwa. Bajeti nzima ya *GST* ni shilingi milioni 300 peke yake inapelekwa kwenye *ICT* kwa maana ya TEHAMA.

**MWENYEKITI:** Hoja yako!

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo na *commitment* ya Mheshimiwa Waziri kwamba ni kwa nini sasa wasiongeze pesa hizi au kwa nini asiweke *special treatment* kwenye upande huu kwa sababu hapa ndiyo kunakonunuliwa *servers;* na mpaka sasa hivi…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa subiri kidogo. Acha nikuongoze vizuri. Kwenye hoja hii ukiuliza kwa nini? Ni kama unauliza swali. Wewe unataka jambo fulani hivi mahsusi

ambalo halipo, yaani wewe unataka likae sawa sawa. Ndiyo kanuni zetu zinavyotaka. Ukisema kwa nini? Yaani ni kama vile umeondoka kwenye ile hoja, unataka akujibu kama swali. Umenielewa vizuri?

Haya tengeneza vizuri hoja yako.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba *commitment* ya Mheshimiwa Waziri kwenye namna ambavyo anaweza akaweka *special treatment* kwenye upande huu wa kuongeza pesa, kununua vifaa, kwa upande wa *ICT* kwa ajili ya *storage security*, *packages operation systems*, *software* na *fireworks* ambazo zitatusaidia kwenye kukusanya *data* za *ICT* kwa upande wa *GST*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri utakuwa umeielewa hoja yake. Anaomba *commitment*. Sasa sijui unaji-*commit* kwenye nini ambacho hajaomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge. Kwanza nieleze kwamba nia yetu kama Wizara ni kuhakikisha kwamba tunaijengea uwezo *GST* kwa sababu ndiyo tegemeo kubwa kwenye utafiti wa madini hapa nchini; na kwa namna yoyote ile itakavyokuwa ni lazima *GST* wafikie watu kwa ajili ya kutoa huduma. Ndiyo maana utaona sasa tunafungua ofisi kwenye Kanda, badala ya kuiweka tu hapa Dodoma, tunapeleka Geita, tunapeleka Chunya na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba atupitishie fedha hizi twende tukafanye kazi na sisi tuko *committed* kuongeza fedha mahali ambako tutakuwa tunaona kuna uhitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Nadhani ameelewa, amekaa bado. Kwa hiyo, tunaendelea na Mheshimiwa Agnes Marwa, naye anataka ufafanuzi.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nami namwomba Mheshimiwa Waziri aelezee kwa kina zaidi, *otherwise* nami nitashika shilingi kwenye mshahara wake. Ni kwa nini mikoa yenye madini hajaona haja ya kuwa na Balozi mwanamke wa Madini ukizingatia kuna changamoto nyingi sana za wanawake wachimbaji na hasa wachimbaji wadogo wadogo? Ni hayo tu. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Nadhani hiyo imeeleweka, lakini kwa sababu haiko hapa kwenye vifungu inaleta mtihani kidogo. Nadhani sasa tuelekee kwa Mheshimiwa Kasheku Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba ufafanuzi wa kina kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Wakati wa mchango wangu, nilichangia nikasema, Wabunge wengi tunaowakilisha maeneo yanayozungukwa na migodi mikubwa, tumekuwa na migogoro hasa ya mahusiano; na shida kubwa inakuwa, pengine Kamati ya Halmashauri inapotaka kukutana na uongozi, *MD* wa migodi, hawakubali kukutana na sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba kwamba sisi Halmashauri ya Geita kwa miaka sita tunaomba kukutana na *MD,* hatujawahi kukutana naye. Sasa naomba *commitment* ya Waziri kwamba kwa kuwa wenzangu wamenituma kama Baraza, unatoa *appointment* gani ya kuja kukuona ili kile kikao uki-*handle* utuwekee utaratibu mzuri?

**MWENYEKITI:** Sawa. Hilo nalo jamani haliko hapa kwenye vifungu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri mtajibizana baadaye kwamba lini mtaonana kwa ajili ya kuweka hiyo mipango mizuri kwa ajili ya Jimbo lake la Geita na Mkoa wa Geita kwa ujumla. *(Makofi)*

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Spika! Mheshimiwa Spika!

**MWENYEKITI:** Fungu linaafikiwa? Nani anayeita Mheshimiwa Spika?

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Kishimba.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kishimba.

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilitoa hoja hapa na ilikuwa hoja ya msingi kwa Taifa kwa sababu tuna shida ya pesa. Kwamba bei iliyoongezeka kwenye dhahabu bila gharama za uchimbaji, imeongezeka kama *boom,* ni pesa ya nani? Naona Mheshimiwa Waziri hakutoa kauli yoyote, ameinyamazia. Naomba mwongozo.

**MWENYEKITI:** Haya ngazi hii ukiomba mwongozo, maana yake nirudi pale juu. Kwa hiyo, utaniomba nikisharejea pale juu, nikisharudi kuwa Spika. Saa hizi ni Mwenyekiti.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.......Sh. 1,179,321,861
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*......Sh. 1,915,448,191
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*........................Sh. 650,020,594
Kifungu 1005 – *Legal Services Unit*........................Sh. 816,956,585
Kifungu 1006 – *Government Communication Unit*........................................Sh. 1,151,081,854
Kifungu 1007 – *Procurement Management Unit*................................................Sh. 624,909,390
Kifungu 1009 – *Management Information Systems Unit*.................................Sh. 747,080,000
Kifungu 2001 – *Minerals Division*........................Sh. 49,489,392,158

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 100 – Wizara ya Madini**

Kifungu 2001 – *Minerals Division*.......................Sh. 22,000,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 123 (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi na imekamilisha kazi yake.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge zima.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 – Wizara ya Madini Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Madini na Naibu Waziri wake; na pia na watendaji kazi wake kwenye Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu na viongozi wote. Tunawapongeza sana kwa sababu Bunge limepitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kama mlivyokuwa

mmeomba, na tunawatakia kila la heri katika utekelezaji wa yale mliyosema kwamba mnaenda kuyafanya na Bunge sasa limewapa hicho kibali. Kwa hiyo, tunawatakia kila la heri katika utekelezaji wa yale yote yaliyosemwa humu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nitumie fursa hii kusema kwamba Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 yamepitishwa na Bunge. *(Makofi)*

Pia nachukua fursa hii kuwapongeza sana Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kushirikiana na Wizara hii na kuhakikisha wanatuletea maoni hapa na mengine ambayo yameshafanyiwa kazi na upande wa Wizara. Kwa hiyo, tunawapongeza sana kwa kazi nzuri mliyoifanya mkiongozwa na Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Dunstan Kitandula na Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote kwa ujumla tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Vile vile Wabunge mliopata fursa ya kuchangia, nia yenu ni njema na mengine ambayo Mheshimiwa Waziri hajapata fursa ya kuyatolea maelezo hapa, utaratibu wetu wa kibunge ni kwamba yote yatatolewa ufafanuzi kwa maandishi. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba wakati wanayatafuta yale majibu kule, mengine watakuwa wanayafanyia kazi kama ilivyo kawaida.

Waheshimiwa Wabunge, tukiwa kwenye Kamati ya Matumizi alikuwa amesimama Mheshimiwa Kishimba, sasa nimpe fursa aseme jambo lake alililokuwa analiombea mwongozo. Mheshimiwa Kishimba.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Hoja yangu hapa niliyoileta ni kwamba bei ya dhahabu inapopanda, ilipanda kwa ajili ya tukio la vita. Kwa hiyo, yeye mwenye mgodi, ile siyo pesa yake kwa sababu

gharama yake ilikuwa vile vile na gharama yake pamoja na vitu vingine havikubadilika chochote.

Mheshimiwa Spika, bomu limedondoka leo Ukraine, bei ya dhahabu imeruka kwa dola 300. Kwa hiyo, hicho kilichoongezeka, kwa kawaida asilimia zote ni mali ya Serikali kama wenzetu Waarabu wanavyotajirika; bei ya mafuta inapopanda tunashuhudia nchi za Uarabuni ziki-*enjoy holiday* hiyo kwa ajili ya bei kupanda.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikaomba Mheshimiwa Waziri atupe ufafanuzi, kwa kuwa vitabu vigumu kubadilirisha ni Qurani na Biblia, lakini vitu vingine vyote vinaweza kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Kishimba wakati tukiwa kwenye Kamati ya Matumizi alikuwa anataka Mwongozo, lakini kwa maelezo aliyotoa hapa anataka ufafanuzi kutoka upande wa Serikali, na siyo mwongozo wangu. Kwa hiyo, kwa ngazi hii tuliyofikia hakuna hiyo sehemu ambayo Mheshimiwa Waziri anaweza akaanza kutoa ufafanuzi wa jambo hilo, basi kwa sababu Bunge pia linaendelea, tutatoa fursa jambo hili alilolisema Mheshimiwa Kishimba liletewe majibu; na kwa sababu ni swali mahususi, basi litajibiwa kama swali ili Wizara ipate nafasi ya kutoa ufafanuzi kuhusu hilo ambalo amelisema. Kwa hiyo, litapangiwa muda wa kutolewa ufafanuzi kama swali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna jambo hapa limetokea, lakini sasa kwa sababu na lenyewe limesemwa wacha nilitolee maelezo kwa kifupi.

Mheshimiwa Agness alisimama kuhusu hoja ya uteuzi wa Mabalozi na hapa sikumzuia Waziri kufanya, lakini kimsingi akija kuhitimisha hoja, anahitimisha kwa maana ya ile michango iliyotolewa hapa na Waheshimiwa Wabunge na siyo kuanzisha jambo jipya. Nadhani nilitoa maelezo kidogo

jana kuhusu kuanzisha jambo jipya ndiyo changamoto kama hizi zinatokea. *(Makofi)*

Nafikiri hoja ya msingi ilianzia kwa Waziri, kwa hiyo, hiyo lazima liwekwe sawa. Mheshimiwa Waziri ndiye aliyeanzisha hoja ya Mabalozi ambayo haikuwepo kwenye hoja yake wala kwenye michango ya Wabunge. Yeye akaianzisha, hoja ikawa ni mpya. Kwa kuwa ni hoja mpya, na Mbunge naye akashikia hapo kwenye hiyo hoja mpya. Kwa hiyo, hayo ndiyo ambayo nilikuwa natoa ufafanuzi jana.

Nitoe angalizo, ni muhimu sana na kwa sababu Mawaziri huwa wanafanya hivyo kwenye sekta zao kutoa fursa kwa watu fulani hivi kuwa wasemaji ama kuyasemea mambo fulani; kuna mabalozi hapa wa kodi na mambo kama hayo, nazo ni teuzi. Sasa mimi nawaomba sana, ili kuweka jambo vizuri hili alilolizungumza Mheshimiwa Agness, Waheshimiwa Mawaziri mnapoteua mabalozi muwe na vigezo mahususi vinavyojulikana ambavyo akitajwa mtu fulani itajulikana kabisa yule anazo sifa hizo ambazo mwingine hana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hizi nafasi za ubalozi kwa sababu siyo ubalozi kama anaoteua Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye anamteua ampendaye, ninyi upande wa Serikali mnavyowateua hawa mabalozi msiteue mwapendao, mwateue wenye vigezo vile ambavyo mmejiwekea kuhusu jambo lenyewe mahususi unalomteua balozi kwalo. Isije ikatokea kunatokea uteuzi wa urafiki, uteuzi wa namna ambayo inaleta maswali, hata wewe ukiambiwa kwa nini umemteua huyu, utasema nilimsikia anachangia Bungeni. Aah, hicho peke yake hakiwezi kuwa kigezo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nawaomba mjiwekee vigezo ninyi wenyewe, siyo kazi ya Bunge hiyo, lakini vigezo ambavyo ukitangaza mtu, kila mtu atajua huyu anavyo hivyo vigezo vya kuwa balozi ambapo mwingine hana. Kwa hiyo, hilo ni jambo la muhimu sana kwa upande wenu Serikali mnapoteua hao mabalozi kwenye sekta zenu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge na hili nilitolee maelezo kidogo. Kwa sababu tarehe ya Iddi haijajulikana bado, kwa sababu tunasubiri mwandamo wa mwezi, kwamba aidha mwezi utaandama Ramadhani 29 au Ramadhani 30. Kwa hiyo, kwa kuwa hatuna hakina na hakutatokea nafasi ya kuja tena hapa ili tuje tuahirishe Bunge kwa ajili ya siku mahususi baada ya Iddi kutokea; kwa kufuata mwongozo aliyeutoa Mufti unaashiria Iddi inaweza ikawa Jumatatu ama Jumanne. Kwa sababu hatufahamu, basi naahirisha Bunge mpaka siku ya Alhamisi saa tatu kamili asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 7.25 mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 5 Mei, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*